# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Nne - Tarehe 12 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 25

**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR (K.n.y. MHE. TAUHID C. GALLOS)** aliuliza:-

Mradi wa *TASAF* unasimamiwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Je, kwa upande wa Zanzibar, Mradi wa TASAF unasimamiwa na Wizara gani?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mradi wa *TASAF* unasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar. Mkurugenzi wa Uratibu katika ofisi hiyo ndiye anayehusika na uratibu wa shughuli zote za *TASAF* chini ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais Zanzibar.

TASAF imeingia mkataba wa makubaliano (MoU) na Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kujiridhisha kuwa utekelezaji wake unazingatia malengo ya mradi. Vilevile tuna Kamati za Uongozi Unguja na Pemba ambazo zinapitisha maombi ya miradi yote ya wananchi kutoka maeneo hayo.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Wabunge walioko Zanzibar hawaingii katika vikao vya *TASAF* ina maana hayo ndiyo makubaliano ya Serikali zote mbili?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo utaratibu Tanzania Bara Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Visiwani ni Wajumbe wa Kamati hizo kama hawaudhurii basi ni matatizo yanatokana na utaratibu. Lakini tutawasiliana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kuona kuwa Wabunge wanahusishwa katika Kamati zinazohusika.

Na. 26

**Huduma ya Maji Safi na Salama Vijijini**

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA** aliuliza:-

Mradi wa bomba la maji kutoka Ziwa Victoria mpaka Tabora linapitia Wilaya ya Uyui jirani na Jimbo la Igalula:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha huduma hiyo na Kata jirani za Kigwa na Igalula katika vijiji vya Kinamagi, Mbuyuni, Kigwa na katika kata ya Igalula vijiji vya Igalula Barazani na Igalula Stesheni ambako kuna kero kubwa ya maji.

(b) Je, ni lin i Serikali itavipatia huduma ya maji vijiji 48 Jimboni Igalula kati ya vijiji 54 vilivyopo umbali wa zaidi ya km.12.5 kutoka bomba linalotoka Ziwa Victoria.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Athuman Rashid Mfutakamba, Mbubge wa Igalula lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuvipatia maji vijiji vyote vilivyopo umbali wa kilomita 12 kutoka bomba kuu litakalopeleka maji mjini Tabora kutoka Ziwa Victoria.

Kwa sasa Serikali ipo kwenye utaratibu wa kumpata mtaalamu mshauri atakayefanya kazi ya usanifu wa mradi huo kwa ajili ya ujenzi.Makampuni yaliyowasilisha mapendekezo yao ya kiufundi na kifedha tarehe 27 Aprili,2013. Baada ya usanifu kukamilika na njia ya bomba kuu kujulikana,vijiji vitakavyopatiwa maji kutoka bomba hilo vitajulikana.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mpango wa Serikali kulingana na uwezo uliopo ni kuvipatia maji vijiji vilivyo umbali wa kilomita 12 kwa kila upande wa bomba kuu. Serikali itafanya utafiti wa kujiridhisha kama maji yaliyopo yataweza kuhudumia vijiji vilivyopo umbali wa zaidi ya kilomita 12.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri yanayotoa matumaini kwa wananchi wa Jimbo la Igalula.

Pamoja na hayo nina maswali madogo mawili ya nyongeza pamoja kupata maji kila mahala Jimboni Igalula lakini hakuna tone la maji ya kunywa.

Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia je inawezekanaje Kata hizo 10 zipunguze adha hii ya upungufu wa maji?

Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui Isikizya wananchi na Watumishi hawana maji kabisa sasa kuna mpango gani kwa wananchi na watumishi wa Isigizya Wilaya ya Uyui kuweza kupata huduma ya maji na kero hii iondokane ahsante?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mfutakamba, swali lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu suala la kuzipatia Kata zake miraji ya maji kwa kutengeza mabwawa ni kwamba Wizara ya Maji inachofanya ni kutoa mwongozo, kutoa fedha na kutoa ufundi kwa Halamsahuri zetu na mahali pengine.

Mipango inaanzia katika ngazi za vijiji, ngazi ya Kata na ngazi ya Wilaya na katika ngazi ya Wilaya Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani, ambao wanaweza kupitisha mipango na pale watakapokuwa wamepisha Serikali kupitia Wizara ya Maji itakuwa tayari kuwapa ufundi na kutoa fedha kwa kujenga mabwawa hayo.

(b) Kuhusu suala la matatizo ya maji katika Makao Makuu ya Wilaya ni kweli tunayo miji ya Makao Makuu ya Wilaya ipo mingi kwa Wilaya zote 136, na Miji mikubwa na midogo kwa kasi ina matatizo ya maji. Serikali ina mpango na imeanza mwaka huu kuainisha baadhi ya Miji kuipatia maji na baadae itaenda Mji baada Mji kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maji ya kutosha.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyo karibu na bomba vitapatiwa maji, sasa mpango huu wa maji unategemea kupelekwa mpaka Jimbo la Igunga ambalo ni kame. Lakini Jimbo la Igunga linapakana na vijiji karibu kabisa vilivyo na ukame mkubwa kama Kizonzo, Mseko na Malendi.

Je, Serikali inaweza kuviunganisha na vyenyewe katika huo mpango?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika,tunachosema ni kwamba Serikali itakuwa tayari kupeleka maji katika vijiji vyote ambavyo viko umbali wa kilomita 12 umbali wa bomba kuu maana awali ilikuwa ni kilomita 5.

Lakini cha pili ni kwamba ili tuvipelekee vijiji hivyo ni lazima sasa bomba linalotoka Ziwa Victoria tupime kuwa usanifu unafanyika na ukishafanyika utaonyesha kuwa bomba litapita katika njia ipi.

Mheshimiwa Spika, sasa kama litapita kwenye njia ambazo vijiji hivyo vipo ni dhahiri kabisa kuwa vitapewa maji.

**MHE.MCH LUCKSON.N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, tataizo la usambazaji maji vijijini ni tatizo kubwa kwa nchi nzima na kwangu kule pia kuna vijiji ambalo miradi ilitakiwa kutekelezwa lakini imeshindikana.

Je, Serikali imetenga fedha za kutosha mwaja huu kuhakikisha kuwa vijiji hivi vinapata maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa lipo tatizo la maji nchi nzima na hasa maji vijijini na Serikali kupitia Wizara ya Maji iliweka Sera na kuweka program ya utekelezaji wa miradi hii ambayo tulianza kwa vijiji kumikumi katika kila Halmashauri.

Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mbunge kuwa ili tupate fedha za kutosha yeye ni mmoja wa watakao pitisha bajeti yetu kuiwezesha iweze kutekeleza miradi hiyo ya maji katika vijiji vingi.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, mradi wa maji bomba kutoka Ziwa Victoria umeonyesha mafanikio makubwa sana Mikoa ya Kanda ya Ziwa, na kwasababu hiyo kwa vile sasa maeneo ya Wilaya za Mbozi, Mwomba na Ileje na hasa Miji ya Tunduma kuna shida kubwa ya maji.

Serikali haioni kuwa sasa kuiga mtindo wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria ikaenda sasa kuchukua maji kutoka Ziwa Rukwa kwa ajili ya kuondoa tatizo na kero kubwa katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, niseme tu kuwa wazo lake ni zuri wao vilevile wana nafasi ya kulifanyia wazo hili katika vikao vyao vya RCC ambavyo vikitoka pale vinakuja kwetu linakuwa ni wazi la pamoja na hii inaweza kufanyika baada ya kuona kwamba hakuna njia zingine mbadala za kiteknolojia mbadala katika yale maeneo kwamba hawataweza kupata maji kwa urahisi zaidi tutafikia hiyo ya kutumia Ziwa Rukwa.

**SPIKA**: Kwa dakika tano tumekuwa na maswali ya nyongeza manne kwa sababu ni mafupi na majibu ni mafupi ndivyo inavyotakiwa Swali linalofuata ni Mheshimiwa Silvetry Francis Koka.

Na. 27

**Tatizo la Maji Kibaha- Mjini**

**MHE. SILVESTRY F.KOKA** aliuliza:-

Halmashauri ya Mji wa Kibaha ina ardhi yenye miamba isiyofaa kwa upatikanaji wa maji ya visima na hata yakipatikana ni machache na yana chumvi nyingi hivyo kuifanya Halmsahuri kutofaidika na miradi ya visima:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuipatia bomba kubwa la peke yake Mamlaka ya Maji ya Halmashauri ya Kibaha kama njia mbadala ya kutatua tatizo la maji katika jimbo hili.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mji wa Kibaha una shida kubwa ya maji. Kwa kiasi kikubwa Mji wa Kibaha unategemea maji yanayotoka Mtambo wa Ruvu Juu unaoendeshwa na Shirika la Majisafi na Majitaka Dar es salaam (*DAWASCO).*

Chanzo hicho cha Ruvu juu kinahudumia pia Mji mdogo wa Mlandizi pamoja na vijiji vya Visiga, Misugusugu, Kongowe, Soga, Kwa mfipa, Simbani, Mwendapole, Kwa Mathias, Msangani na Picha ya Ndege, ambavyo viko kandokando ya mabomba makuu yanayotoka Ruvu juu kwenda kwenye matanki ya Kimara – Dar es salaam. Sababu kubwa ya kutotosheleza kwa huduma ya maji kwenye eneo lote linalohudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu ni uwezo mdogo wa uzalishaji pamoja na upotevu mkubwa wa maji. Mtambo huu ulijengwa mwaka 1956 na ulilenga kuhudumia watu laki nane (800,000) lakini kwa sasa unahudumia watu takribani milioni mbili.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inakamilisha taratibu za zabuni kwa ajili ya upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu ili kuongeza uwezo wake kutoka kuzalisha wa lita milioni 82 kwa siku za sasa hadi lita milioni 196 kwa siku. Upanuzi huo utahusisha ujenzi wa kitekeo cha maji kipya *(intake*) na ulazaji wa bomba jipya kutoka Mlandizi hadi Dar es salaam.

Mabomba mawili yaliyopo sasa yatafanyiwa ukarabati na yatatumika kusambaza maji kwenye vijiji vya kandokando ya bomba kuu na maeneo mengine ikiwemo

Mji wa Kibaha. Bada ya upanuzi huo kukamilika, Mji wa Kibaha utapata huduma za maji kwa masaa 24 kwa siku.

**MHE. SILVESTRY F.KOKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Mheshimiwa Spika, ningependa Serikali iweze kuwapa majibu wananchi wa Kibaha sasa ni lini huu mradi wa maji utakamilika na ni lini sasa Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea Jimbo la Kibaha na kujionea adha ya huduma ya maji wanayopata wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kibaha wamekuwa wakipata adha kubwa katika huduma hata ya haya machache yaliyopo na wakionekana kuwa ni omba omba na kwamba hii huduma kwao siyo stahili.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia Halmashauri ya Mji wa Kibaha ili iweze kupata Mamlaka yake ya Maji na kuweza kutoa huduma hii kwa ufasaha katika Mji wa Kibaha Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, swali kwamba ni lini sasa wananchi watapata maji na lini mradi huu utakamilika. La msingi ni kuwa mchakato ulishaanza hivi ninavyoongea tayari makampuni yameshapendekezwa, yale ambayo yanashindania katika ujenzi wa chanzo kule Ruvu Juu na Makampuni mengine yameshaorodheshwa yanayoshindania ulazaji wa bomba toka Ruvu Juu mpaka Mjini na kazi watakazofanya kwa sasa hivi ni kushindania kuandaa mapendekezo ya kifedha na kiufundi ili apatikane mmoja na ambaye anatakiwa kuanza kazi ya ujenzi wa mradi huu mwezi wa nane 2015 mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo wananchi watapata maji, kuhusu wananchi wa Jimbo la Kibaha Mjini kwamba sasa wapate uwakilishi kwamba wapate Mamlaka yao ya Maji nilishawahi kujibu swali kama hili hapa Bungeni, kwamba hatuwezi kuwa na Mamlaka mbili kwenye chanzo

kimoja tunachoweza kufanya ni kuhakikisha kuwa Kibaha na Bagamoyo wanakuwa na uwakilishi katika Bodi ya *DAWASCO.*

Bodi iliyoko sasa hivi inamaliza muda wake mwezi wa nane tutamshauri Waziri ili kuwe na uwakilishi wa Kibaha na Bagamoyo katika Bodi mpya itakayoundwa.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la maji limekuwa ni tatizo kubwa ndani ya nchi yetu, mwaka jana wakati ninahoji suala hili la maji nchini na nikatoa ushauri wa kutumia maji ya bahari kwa ajili ya kuyageuza na kuwa maji ya kawaida, Waziri aliniambia kuwa tayari kuna timu ambayo inafanyia utafiti suala hilo, sasa ninataka kujua.

Je, utafiti ule umefikia wapi ili kuondokana na matatizo haya ambayo sehemu kubwa ya nchi yetu inakabiliwa na tataizo kubwa la maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa iko njia mbadala ya kuwapatia wananchi maji kupitia maji ya bahari ambayo yanapitia *process desalination*, tunachosema ni kwamba sehemu hii kwa sasa hivi Serikali imeruhusu sekta binafsi kujihusisha katika eneo hili ili kuweza kuyatengeneza hayo maji kwa kupitia njia ya *desalination* ili iweze kuwasaidia wananchi.

Lakini sisi kama Serikali kwa sasa hivi tutajitahidi kutumia teknolojia zilizopo bila kutumia maji ya bahari kwa miundombinu iliyopo na maji yaliyopo aihitaji hiyo *process* lakini hatujazuia kwa makapuni binafsi kufanya *process* hiyo.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuwa teknolojia hiyo ni ghali sana na nchi za waarabu ambazo zinatumia teknolojia zinatumia umeme mwingi sana kwenye ku- *process* maji. Kwa hiyo, tusingependa twende huko tuanze kwanza kwa hizi ambazo tunazo tuone kama tunaweza kuwasaidia wananchi wetu kwa teknolojia iliyopo sasa hivi.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema.

Na. 28

**Ujenzi wa Barabara ya Lami Kutoka Marangu-Kilema**

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA** aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Lami kutoka Marangu- Kilema Sokoni umeanza rasmi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga upya madaraja matano ya zamani katika barabara hiyo?

(b) Je, Serikali itatoa lini kibali cha Mkandarasi kuchukua moram katika Mlima wa Ngangu ili kuharakisha mradi huo?

(c) Je, ni kweli Serikali ina mpango wa kubomoa jengo la Hotel ya Kibo iliyoko kwenye Hifadhi ya Barabara na fidia kiasi gani itatolewa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakati Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa barabara Kawawa Nduoni - Kilema hadi Marangu Mtoni, ilibainika kuwa madaraja manne ya Mbonjo, Ruwa, Makoa na Whona yanastahili kufanyiwa matengenezo. Ili kubaini matengenezo yanayohitajika kufanyika katika madaraja hayo, Mhandisi mshauri anafanya uchunguzi wa kitaalam. Uamuzi wa nini kifanyike kwenye madaraja hayo utatolewa baada ya tathmini ya Mhandisi Mshauri.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilishatoa kibali kwa Mkandarasi kuchukua changarawe kutoka chanzo kingine karibu na Kilacha baada ya Mmiliki wa eneo la awali lililopo karibu na mlima Ngangu kutoridhia eneo lake kutumika kwa ajili ya kuchimba changarawe. Kwa sasa upatikanaji wa changarawe siyo tatizo.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa nyaraka za usanifu wa michoro iliyoandaliwa na Mhandisi Mshauri, Barabara ya Marangu Mtoni - Kilema itajengwa bila kuathiri jengo la Hoteli ya Kibo.

Aidha, Serikali haiwalipi fidia wamiliki wa mali zilizomo ndani ya hifadhi ya eneo la barabara kwa kuwa hawastahili fidia kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bunge Na.13 ya mwaka 2007.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili nyongeza.

(a) Kwa kuwa Serikali imeshindwa kuvunja lile jengo la Kibo na wakakubali barabara ijengwe kama ilivyo, ni kwanini barabara kutoka Marangu Mtoni kwenda KINAPA nyumba zilizopo karibu na barabara ile ikizingatiwa kule hakuna ardhi, zimewekewa alama ya kuvunjwa. Kwanini hamkuzingatia sera hiyo kama mlivyofanya kuruhusu jengo la *Kibo Hotel* liendelee kuwepo na barabara iendelee kuwepo.

(b) Hii barabara ya Marangu Mtoni kwenda Kilema Sokoni ni barabara pacha ya barabara ya Kawawa kwenda Nduoni Kirua Vunjo Magharibi, sasa barabara ile imejengwa lakini sasa hivi mvua zimenyesha na wananchi wanalalamika labda wanaweza kuachiwa barabara iliyochakachuliwa. Unasemaje kuhusu hiyo barabara ya Marangu Mtoni kwenda Kilema pamoja na hiyo ya Kawawa kwenda Nduoni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba ujenzi unaoendelea kwa sasa hivi hautaathiri ubomoaji, lakini hoteli hiyo iko ndani ya barabara.

Sasa hivi tulikuwa tumeelekezwa kwamba tuangalie maeneo yale ambayo, maana barabara ile inayozungumzwa ipo mlimani. Sasa kuna maeneo mengine kupata ile hifadhi ya barabara iliyopo kwenye sheria kidogo imekuwa na ngumu tunataka tufanyie mapitio, yale maeneo ambayo ni vigumu kupata hiyo *road reserve* ndiyo maana hiyo imebaki. Lakini muda ukifika kwamba sasa tu-*clear road reserve* basi itahusika na sheria hiyo.

(b) Kwenye barabara ambayo unasema ilishatengenezwa lakini mvua zimeharibu tutazingatia kuweza kuirekebisha katika matengenezo kwa kutumia hela ya mfuko wa barabara. *(Makofi)*

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika ahsante, nina swali moja la nyongeza.

Kwa sababu imeonesha dalili ya ufa katika daraja ambalo linaunganisha Kenya na Tanzania lililopo katika Mto Mara pale Kirume.

Je, Serikali ina mpango gani kuimarisha au kujenga upya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Nasari naomba urudi ulipotoka. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze upya. Daraja ambalo lipo mto Mara, barabara ya lami ambayo inaunganisha Tanzania na Kenya ni hatari na kwa usalama wa abiria,

Je, Serikali ina mpango gani, kujenga upya daraja la mto Mara eneo la Marasomoche kwa ajili ya kuimarisha daraja hilo?

**SPIKA:** Ni swali jipya hilo, ila kwa sababu ni daraja kubwa naomba ujibu kama unaweza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** Mheshimiwa Spika, naomba swali lake la daraja la Kirume tulifanyie kazi ili tuweze kumpa majibu sahihi na wananchi wa Mara waweze kusikia.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Mara nyingi makandarasi wanaopewa kazi ya kujenga barabara huchimba mashimo ili kuchukua moram kwa ajili ya ujenzi, lakini huacha mashimo hayo makubwa mara wanapomaliza kazi zao na kuathiri mazingira ya maeneo hayo.

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba Makandarasi wanapomaliza kazi wanayafukia yale mashimo ili kutoathiri mazingira.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwenye mikataba ya ujenzi wa barabara tumeweka kifungu ambacho mkandarasi anapomaliza kazi, ni lazima yale ma-*blow pit* ambapo alikuwa anachukua changarawe ayatengeneze na ayaache katika mazingira ambayo ynakubalika kulingana na mkataba ule. Endapo kuna mkandarasi ambaye ameacha ovyo, huyu atakuwa amevunja sheria kwa kufanya hivyo.

Kwenye mikataba mingi huwa tunakuwa na kipindi cha maangalizo kwa hiyo kipindi hicho ndiyo tunaangalia kama kuna mkandarasi ambaye hajatekeleza hili basi tunatoa tozo na kumkata kwenye fedha zake za malipo ya mwisho.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa ujenzi wa barabara inayotoka Dodoma kwenda Iringa inapita katikati ya Mji wa Iringa.

Je Serikali imeweka mkakati gani kuchepusha ile barabara, mradi ule utakapokamilika kusiwepo msongamano wa magari katikati ya Mji?

**SPIKA:** Maswali mapya, mnatakiwa kuuliza maswali ya kiujumla. Kwa sababu mkiwa mkoa mmoja labda anaweza kujibu, Waziri jibu kama unataka.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya kutoka Dodoma-Iringa tunaanza kuijenga na barabara ile ni kwamba itapita katikati ya Mji wa Manispaa ya Iringa na ni kweli kwamba kutakuwa na msongamano. Suala hili tumeshaliona tunalifanyia kazi ili tupate barabara ya mchepuo, yale magari ambayo hayana sababu ya kupita katikati ya Mji yaweze kupita pembeni ili kupunguza msongamano wa magari katikati ya Mji. Kwa hiyo suala hilo tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa anapaswa kuuliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Joshua Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikuombe radhi nilikuwa nakwenda kwa sababu ya swali la Mheshimiwa Msigwa ndiyo sababu nilikuwa nakwenda kwenye dawati lake.

**SPIKA:** Endelea tu.

Na. 29

### Ahadi ya Kufunguliwa kwa Kiwanda cha Chai Njombe

**MHE. JOSHUA S. NASSARI (K.n.y. MHE. MCH. PETER S. MSIGWA** aliuliza:-

Zao la Chai limekuwa ndio tegemeo kubwa la uchumi wa wananchi Njombe Kaskazini, hususani Tarafa ya Lupembe, lakini uchumi wa Chai maeneo hayo umedorora kwa sasa kutokana na mgogoro kati ya Mwekezaji na wananchi ambapo Kiwanda cha Chai hakifanyi kazi kwa takribani miaka nane sasa:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 22 Septemba, 2010 ya kuhakikisha kwamba Kiwanda cha Chai kinafunguliwa na kuanza kazi haraka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Kiwanda cha Chai Lupembe ulianza mwezi Julai, 2008 kati ya wanahisa ambao ni Mwekezaji *M/S Dhow Merchantile EA Limited* na Muungano wa Vyama vya Ushirika Lupembe (MUVYULU) ambapo *M/S Dhow Merchantile* anamiliki asilimia 70 na MUVYULU anamiliki asilimia 30.

Kiwango hiki cha umiliki kilifikiwa baada ya Serikali kuuza hisa zake zote asilimia 25.76 na MUVYULU kuuza hisa zake asilimia 44.24 kati ya asilimia 74.24 ilizokuwa inamiliki na kubakiwa na asilimia 30. Mwezi Julai, 2008 MUVYULU walifikia hatua ya kufunga kiwanda hicho na kupeleka suala hilo Mahakamani baada ya kutokea kutokuelewana kati yao na Mwekezaji mwenza *M/S Dhow Merchantile (EA) Limited.*

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, alifikishiwa kadhia hii na wananchi wa Lupembe na kuahidi kushughulikia mgogoro wa Kiwanda cha Chai cha Lupembe. Pamoja na kuweka angalizo kwamba suala hili liko Mahakamani. Aidha, Serikali kupitia uongozi wa Wilaya na Mkoa wa Iringa pamoja na Wizara yangu imefanya jitihada mbalimbali kwa nyakati tofauti za kushawishi pande husika kumaliza mgogoro huo nje ya Mahakama bila mafanikio. Hata hivyo, kesi hii bado inaendelea Mahakamani na ni matarajio yetu kwamba kesi hii itamalizika.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa uchumi wa wakulima na wananchi wa Tarafa ya Lupembe hauathiriki na kufungwa kwa kiwanda hicho wakati wa kusubiri maamuzi ya Mahakama, Serikali imehamasisha wawekezaji kujenga kiwanda mbadala katika Tarafa ya Lupembe ili wakulima wauze majani ya chai kiwandani hapo.

Kutokana na uhamasishaji huo, Kampuni ya Chai na Kahawa ya Mufindi Mufindi *(Tea and Coffee Company (MTC)* Wamejenga Kiwanda katika Tarafa ya Lupembe kwa ubia na wakulima ambapo kampuni ya *MTC* inamiliki asilimia 75 na wakulima asilimia 25. Aidha, ili kuhakikisha kiwanda hicho kinafanya kazi kwa ufanisi, wabia hao wameunda Kampuni ya uendeshaji wa kiwanda hicho *(Ikanga Tea Company Ltd.)* ili kuendesha kiwanda hicho na kwa sasa kimeanza kusindika majani ya chai katika Tarafa ya Lupembe tangu tarehe 1 Novemba, 2012.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukienda maeneo mengi katika nchi yetu kila eneo lina zao lake kubwa la uchumi na kama swali la awali lililokuwa linaulizwa ni zao la chai. Ukienda maeneo mengine.

Kwa mfano, kule kwetu Arumeru ilikuwa ni kahawa ambayo ilikuwa chini ya Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini miaka ya nyuma zao la kahawa lilikuwa ndiyo zao kuu la uchumi, wananchi walikatwa pesa kwenye mfuko maalum kupitia zao la kahawa, lakini leo tunazungumza miaka 20 baadaye zaidi ya shilingi milioni mia sita mpaka leo ile fedha ya mfuko maalum wananchi hawajarudishiwa na vyama vya ushirika havifanyi tena kazi.

Ningependa kujua Wizara hii ya Kilimo, Chakula na ushirika ina mpango gani ili kuhakikisha kwamba wale wananchi ambao walikatwa fedha kwenye zao la kahawa kwenye mfuko maalum wanarudishiwa fedha zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini swali hilo ndiyo kabisa liko nje, unajua lile lingine ni kesi ya Mahakama kwamba kiwanda kimefungwa, hili lingine halihusiki. Naomba tuendelee na Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, zao la chai ni zao mojawapo linalochangia katika uchumi wa Taifa na Chai inalimwa Njombe – Mbeya, wakulima wana tatizo kubwa sana kupata mbolea ya ruzuku.

Je, Serikali ina mkakati gani kutoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima hawa ambao wanasaidia kuinua pato la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mufindi ndiyo mzalishaji mkuu wa chai nchini lakini zipo Wilaya kama Rungwe, Lushoto, lakini kwa kuhakikisha kwamba wakulima wadogo ambao kwa sasa hivi wanalima wastani kama wa kilo 1000 ya majani makavu ya chai, wanaweza kufikia wastani wa kilo elfu mbili kwa majani ya chai.

Kwa hiyo, ili tufikie hatua hiyo na kwa sababu chai hii ya wakulima wadogo inaonekana ikifika hata kwenye mnada wa soko Mombasa ni chai ambayo inapendwa sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga na kwenye mkutano wa wadau wa chai ambapo tulikutana nao Morogoro tulitoa ahadi kwamba tutakutana na umoja wa wakulima wadogo TASHTIDA wa chai, wakala wao, ili kupata ufumbuzi ya namna ambavyo wao watatoka kuongeza tija kutoka kilo 1000 za majani makavu kwenda kilo 2000.

Kwa hiyo, naomba niwaahidi wakulima wetu wa chai katika Wilaya hizi, Mheshimiwa Profesa Mwakyusa, Mheshimiwa Msolla na wengine kwamba suala hili linafanyiwa kazi kwa karibu na tutawashirikisha Wabunge wanaotoka kwenye sehemu zinazolima chai.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Moshi Kakoso atauliza swali hilo.

Na. 30

**Ruzuku kwa Zao la Tumbaku**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Tumbaku ni zao linaloliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na hivyo kuinua pato la Taifa:-

(a) Je, ni lini zao hilo litaingizwa kwenye ruzuku ya Serikali ili kuweza kupunguza gharama za pembejeo kwa wakulima wa zao hili?

(b) Serikali iliahidi asilimia mbili (2%) ya ushuru lakini haijatekelezwa. Je, Serikali itakamilisha lini ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kutoa ruzuku ya pembejeo kwa muda utakaoruhusu kulingana na mazingira ya kiuchumi na na kijamii kwa mazao yote ya chakula na biashara ili kujenga uzoefu wa matumizi ya pembejeo hususani mbolea na mbegu bora.

Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti kwa sasa ruzuku inatolewa kwa baadhi ya mazao kama vile chai, pamba, kahawa, korosho, alizeti, mtama mahindi na mpunga.

Mheshimiwa Spika, zao la tumbaku ni miongoni mwa mazao makuu ya kilimo nchini ambayo kwa sasa hayapati ruzuku ya pembejeo kutokana na ufinyu wa Bajeti pamoja na uwezo wa zao lenyewe kujihami kutokana na mazingira nafuu ya bei na soko la tumbaku ukilinganisha na mazao mengine kama pamba na korosho. Aidha, mkakati wa Serikali ni kutoa ruzuku kwenye mazao mengine kadiri ya upatikanaji wa rasilimali fedha utakavyoongezeka.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali Na. 112 na Mheshimwa Victor Mwambalaswa Mbunge wa Lupa na swali Na. 113 la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, katika Mkutano wa Tisa tarehe 9/11/2012 ni kuwa uamuzi wa kufanya mgawanyo wa ushuru wa mazao wa asilimia 5 kwa kuwapatia wakulima wa tumbaku asilimia mbili (2) ya ushuru huo ulifanyika wakati sheria ya Fedha ya mwaka 2011*(The Finance Act 2011)* ilishapitishwa na Bunge na hivyo kutokufanyika kwa marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa *(The Local Government Finance Act, 1982)* ambayo ingeruhusu mgawanyo huo kwa wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Spika, ahadi hiyo ya Serikali ilitokana na na kushuka kwa bei ya tumbaku ambayo kwa sasa imeanza kuimarika hadi kufikia Dola za Kimarekani 1.82 kwa kilo msimu wa 2012/13 kutoka dola za kimarekani 1.4 msimu wa 2010/2011.

Aidha, katika kukabiliana na kubadilika mara kwa mara bei za mazao, Serikali kwa kushirikiana na wadau ipo katika mchakato wa kuanzisha mfuko maalum wa kufidia bei za mazao kwa wakulima pale zao linaposhuka *(Price Stabilization Fund)* kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri na kuwaepusha na hasara kubwa inayotokana na kushuka bei za mazao katika masoko ya kimataifa hapo inapotokea.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini nina maswlai mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, zao hili limekuwa likizalishwa katika mikoa tisa na zaidi ya Wilaya ishirini zinazalisha zao hili, ni sababu zipi zinazofanya isione umuhimu wa zao hili kuwapa ruzuku ya Serikali ili waweze kuzalisha kwa wingi na kuwapa nafuu wakulima ambao wanazalisha katika nchi hii?

Swali la Pili, kwa kuwa, Serikali iliahidi ndani ya Bunge lako Tukufu na kupewa uzito na Waziri Mkuu kwamba wakulima wangepewa fedha zile za kuwasaidia kwa sababu ya mdororo wa kiuchumi. Ni kwanini Serikali mpaka sasa bado haijatekeleza na haioni umuhimu sasa wa kuwapa fidia wale wakulima ambao walipata mdororo wa kiuchumi katika msimu uliopita na kuwafanya waweze kupata kifutajasho?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso na kwa bahati yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo na haya masuala tumeyazungumza hata kwenye Kamati juzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona ni muhimu sana wa kushughulikia zao la tumbaku. Zao la tumbaku kimsingi ndilo zao linaloleta pesa nyingi sana za kigeni kuliko zao lingine lolote katika mazao yote ya biashara yanayouzwa hapa nchini.

Kwa hiyo, zao la Tumbaku ni zao kubwa sana Tanzania na Serikali tunalifuatilia kwa karibu na tunafanya kazi kwa karibu sana na Bodi ya tumbaku, na tunasema siyo katika masuala haya tu ya mbolea tu na ruzuku yapo masuala mengi sana ya usimamizi wa zao lote hili ambalo tunafanyakazi na bodi ya Tumbaku kwa karibu sana na lengo ni kuongeza tija katika zao la tumbaku na kuongeza upatikanaji wa masoko ili wakulima wa Tanzania watoke kwenye kupata dola milioni mia mbili na sitini kwenda mpaka milioni mia nne ambayo ndiyo lengo la *export earnings.*

Mheshimiwa Spika, swali la pili wakulima wangepewa fedha za mdororo, mdororo wa kiuchumi haukugonga zao

la tumbaku tu uligonga mazao mengi. Kusema kweli kwenye ile *Stabilization Capacity* ya Serikali inategemea na uwezo wa Serikali. Uwezo wa Serikali kama wote tunavyofahamu haukuwa mkubwa kiasi hicho.

Kwa hiyo, siyo zao la tumbaku tu lakini nadhani zao la kahawa pia lina mgogoro huo kwa Mzee Dkt. Augustine Lyatonga Mrema na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini tunajipanga ili huko mbele tunapokwenda haya mazao yawe na tija zaidi na manufaa zaidi na mapato zaidi kwa wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika Wilaya ya Kasulu, wapo wakulima ambao tangu mwaka jana tumbaku yao imerundikwa stoo, hawajaweza kupata soko la kuuza tumbaku hiyo. Wakulima hao wameendelea kuwa masikini kwa sababu, walitegemea kupata kipato kutokana na tumbaku yao.

Mheshimiwa Spika, wakulima hao ni wa vijiji vya Nyumbigwa, Rungwe Mpya na Ahsante Nyerere.

Je, Serikali, inawaambia nini wakulima hao ambao mpaka sasa hawajaweza kuuza tumbaku yao?

**SPIKA:** Ah, haya. Sijui, atakumbuka?

Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana. Ni swali jipya pia.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephine Ngenzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili suala la wakulima hawa wa Wilaya ya Kasulu, zao la tumbaku ni zao ambalo linakwenda

mpaka kwenye Wilaya nyingine mpya nyingi. Kwa hiyo, ninaomba nimsihi tusubiri kwani suala hili linaghughulikiwa na Bodi, tujue tatizo ni nini na twende tukaangalie, inawezekana tatizo ni wale *classifiers* au matatizo mengine. Inaweza ikawa matatizo yako katika sura mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nikutane na Bodi na wawakilishi wa Bodi, Viongozi wao, ili tujue suala hili lina sura gani na tulipatie ufumbuzi wa namna gani. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, tumbaku inaleta madhara sana katika nchi yetu, magonjwa ya kansa na inapigwa vita dunia nzima. Kwa hiyo, kwa nini, Serikali, isiwe na mpango wa kuwahamasisha wakulima wetu walime bangi, isindikwe, iuzwe nchi za nje, tupate hela ya kigeni? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Badala ya tumbaku, waweke bangi? Haya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, labda mmefanya utafiti. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme, hii hali ya kujaribu kupingana na uzalishaji wa zao la tumbaku kwa sasa hivi, haina tija kwa sababu, nchi nyingi sana duniani zinaendelea kuwa na mahitaji makubwa ya zao la tumbaku.

Kwa bahati nzuri tumbaku ya Tanzania, inakubalika sana kwenye masoko hayo makuu ya dunia. Hivi karibuni tumeingia kwenye soko la China, wametukubalia.

**SPIKA:** Muda, muda, muda. Msianze kujiremba hapa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, samahani, wanataka kujua.

**MBUNGE FULANI:** Bangi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, zao la bangi bado halijawa zao la biashara ya kilimo. Lakini kuna nchi nyingine Ulaya ambazo wameruhusu zao hilo la bangi. Sasa Mheshimiwa Esta, anatikisa kichwa pale. Mimi nadhani hapo itakapofikia bangi kuruhusiwa *au* likikubalika zao hili litumike na likapata uhalali wa matumizi kwenye maeneo mbalimbali duniani, basi ni jambo ambalo linaweza kufikiriwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani, sasa inabidi niendelee tu. Maana naona sasa tutaingia kwenye mabalaa bure. *(Kicheko)*

Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Leticia Nyerere, atauliza Swali linalofuata.

Na. 31

**VITENDO VYA KINYAMA KWA OMBAOMBA**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Kuna taarifa kuwa baadhi ya wanaume wanawapatia mimba wasichana walemavu wanao-ombaomba, kitendo ambacho ni cha kinyama:-

(a) Je, Serikali, ina mkakati gani kuhakikisha kuwa vitendo hivyo vya kinyama vinakoma?

(b) Je, ipo tayari kufanya marekebisho katika Sheria ya Kujamiiana, ili kuongeza adhabu kwa watuhumiwa?

**WAZIRI NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, kwamba ni kweli kwamba, wapo baadhi ya wanaume wanaowarubuni wasichana walemavu na wale wanao omba omba mitaani. Vitendo hivi ni kinyume na Sheria ya Makosa ya Kujamilana, yaani *The Sexual Offences (Special Provisions) Act, 1998.* Sheria hiyo ni moja ya Mikakati iliyochukuliwa kupambana na uhalifu huu wa kinyama.

Aidha, mkakati mwingine ni kuweka adhabu za kuogopesha *(Deterrence).* Adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha miaka 30, pamoja na viboko na faini. Sheria inatambua kwamba, wasichana wa aina hii hawana uwezo wa kiakili na utashi wa kutoa ridhaa ya kujamiiana. Hivyo, utetezi wa mhalifu kwamba, msichana alitoa ridhaa ya kujamiiana haukubaliki Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua na mkakati mwingine wa Kisheria ni ambapo msichana aliyedhalilishwa ana umri wa miaka 10 au chini yake, mhalifu atapewa adhabu ya kutumikia kifungo cha maisha Gerezani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia nafasi hii kuwahamasisha wanawake wote, wanaume wote, wenye mapenzi mema kwa haki za watoto, walemavu na watu wote, wanapoona vitendo hivyo vya kudhalilisha wataoe taarifa kwenye vyombo vya dola, ili hatua stahiki zichukuliwe na kuwafikisha Mahakamani.

(b) Mheshimiwa Spika, adhabu zilizoainishwa katika Sheria ya Kujamiina ni kubwa na zinatosheleza. Hata hivyo, kazi ya kutunga na kurekebisha Sheria kwa kuongeza adhabu ni kazi

ya Bunge hili. Serikali, inaridhia kwamba, adhabu hii inakidhi viwango vya adhabu vilivyopendekezwa katika Mikataba ya Haki za Binadamu na katika masharti ya Ibara ya 13 (b) (e), ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, wanaume wengi wanaovizia walemavu, ama wana matatizo ya ubongo, hawajiamini na vile vile hawana uwezo wa kushawishi wanawake.

Je, Serikali, haioni kwamba, kuna haja sasa ya kuanzisha Kituo cha kuwafundisha wanaume hawa jinsi gani wataweza kuachana na ngono ya dezo? *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa, Waheshimiwa Wabunge, walitoa sauti za vicheko)*

**SPIKA:** Naomba uendelee, muda wangu unaisha.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, kuna baadhi ya nchi duniani wanatumia adhabu ya kuhasi; yaani *permanent disfiguration of genital parts.*

Je, Serikali, haioni kwamba, kuna umuhimu wa kutazama kama adhabu hii iweze kutumika, hatimaye Taifa letu liwanusuru watoto wa kike na wanawake kwa ujumla?

**WAZIRI NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzisha Kituo Maalum cha kufundishia. Mimi hili ninaliona kwamba, zamani katika mila na desturi kwa baadhi ya makabila walikuwa wanafanya hivyo kwa watoto wa kiume wanapoenda jando, wanawafundisha baadhi ya vitu vya namna hiyo.

Lakini kwa Serikali, sasa kuanzisha Kituo Maalum, hiyo haiwezekani. Hilo ni jambo binafsi na sio kwamba, wale wanakuwa na matatizo, baadhi yao hawana matatizo kabisa, ni watu wazima, wana akili zao; ni kwamba, basi tu wana tamaa za kijinga.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, mimi kama mama, kwa kweli, nahuzunishwa na vitendo vya wanaume kuchukua walemavu, mlemavu wa ubongo, unaenda kufanyanaye mapenzi. Unamchukua kiwete unaenda kufanyanae mapenzi; kwa kweli, sio jambo la busara.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, adhabu ya kuhasi. Kwa kweli, katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*(Hapa, Waheshimiwa Wabunge, walipaza sauti ya kicheko)*

**SPIKA:** Naomba tusikilize majibu.

**WAZIRI NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba, katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kifungu cha 13 (e), ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha mtu. Sasa kuhasi ni adhabu ya kutweza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, tunaendelea. Leo maswali ya ajabu ajabu tu, tunaendelea. Kama mengine yatakuwa ya nguoni hapa.

Tuendelee Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo?

Na. 32

**Mgogoro wa Mpaka Kijiji cha Kikulyunguna Pori la Akiba la Selous**

**MHE. FAITH M. MITAMBO** aliuliza:-

Mgogoro wa mipaka kati ya Kijiji cha Kikulyungu na Pori la Akiba Selous, umekuwepo kwa muda wa zaidi ya miaka kumi (10) sasa:-

(a) Je, Serikali, itamaliza lini mgogoro huo?

(b) Je, Serikali, itahakiki lini huo mpaka kama ulivyo kwenye tangazo la Serikali, la mwaka 1974?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mgogoro kati ya Kijiji cha Kikulyungu na Pori la Akiba la *Selous,* ulishughulikiwa na Wizara yangu mwaka 2010 kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Liwale na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Magingo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010, Wizara yangu ilihakiki mpaka kati ya Pori la Akiba la *Selous* na Vijiji vinavyounda *WMA* ya Liwale, kwa kuzingatia maelezo ya Tangazo la Serikali, Namba 275 la mwaka 1974. Uhakiki huo ulibaini kuwepo maeneo yaliyokuwa yameingizwa kimakosa kwenye Pori la Akiba la *Selous* na maeneo mengine yaliyokuwa yameingizwa kimakosa kwenye ardhi ya Vijiji, ikiwemo sehemu ya Kijiji cha Kikulyungu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilirejesha kwa wananchi maeneo yaliyokuwa yameingizwa ndani ya Pori la Akiba la Selous, hivyo mpaka unaotenganisha Pori la Akiba la *Selous* na Kijiji cha Kikulyungu uliopo sasa, ni mpaka halali. Hali kadhalika unazingatia Tangazo la Serikali la mwaka 1974.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, uhakiki uliofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii mwaka 2010, ulikwepesha kusudi kwa makusudi kabisa mpaka halali ambao ulikuwa umetolewa kwenye Tangazo la Serikali la mwaka 1972 na kusogeza mpaka huo kutoka Mto Matandu mpaka kuingia eneo la Kijiji cha Kikulyungu.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa, wananchi hawakuridhika na uhakiki ambao ulifanywa mwaka 2010.

Je, Wizara ya Maliasili, iko tayari sasa turudi tena katika Kijiji cha Kikulyungu, tuweze kuuhakiki mpaka huu upya?

Mheshimiwa Spika kijiji cha Kikulyungu, kilitolewa katika umoja wa hifadhi ya Magingo, kwa sababu ya mgogoro huu wa mpaka. Wizara ya Maliasili, inaweza kusema sasa iko tayari kukirudisha Kijiji hiki katika Jumuiya ile ya Magingo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, inatambua jitihada hizi ambazo Mheshimiwa Faith, amekuwa akizifanya. Ninapenda niseme yafuatayo; moja ni Serikali na Wizara, iko tayari kwa kuzingatia umuhimu wa kuwepo amani, mshikamano na wananchi ambao kwa kweli, wao ndio wahifadhi. Wao ndio ambao wanahifadhi hili eneo la pori la akiba la *Selous,* miaka yote.

Serikali hatuna ugomvi wa mipaka kama upo, hata baada ya kurekebishwa mwaka 2010, Wizara, itakuwa tayari kurejea tena kwenye mazungumzo haya, ili tuweze kuhakikisha kwamba, mipaka iko wazi kati ya hifadhi na wananchi. Migogoro kama ipo, inatatuliwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo katika jibu langu la msingi; *WMA,* ambayo ilifanya hiki Kijiji cha Magingo kiondolewe kutokana na mgogoro wa ardhi. Wataweza kurejesha katika mfumo huu wa *WMA* mara baada ya kuhakikisha kwamba, tunaumaliza mgogoro huo. Ningependa kuahidi hapa kwamba, tutafanya kila iwezekanavyo haraka turejee yale makubaliano na tuhakikishe kwamba, amani inapatikana katika eneo letu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa sababu Swali la msingi na mazingira yake yanafanana na hali iliyopo katika Kata ya Kania na Kijiji cha Kania na Mpago, Jimbo la Biharamulo Magharibi. Ambapo wananchi wameishi zaidi ya miaka 50 na Profesa Kulikoyela Kahigi, ni mzaliwa wa pale, leo hii wanaambiwa wanaishi kwenye hifadhi.

Je, Wizara iko tayari kwenda kuangalia mipaka upya na kuwarejeshea amani wananchi wale?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali, imeunda Tume ya Kitaifa, ambayo inajumuisha wadau mbalimbali na pia sekta mbalimbali katika Wizara mbalimbali nchini, kwa ajili ya kupitia migogoro katika maeneo yetu ya hifadhi na mipaka ya wananchi nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu, kwamba, Tume ile tayari imemaliza kazi yake na imeleta taarifa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Taarifa hiyo, inaendelea kuchambuliwa. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba, hiki Kijiji cha Kaniha na Mihango, pale Biharamulo Magharibi, ambapo hivi karibuni Mheshimiwa Waziri, alinituma na nilifika kutembelea hilo Pori la Biharamulo, itakuwa ni sehemu ya maeneo ambayo tutayaangalia na tutayatolea majibu ya pamoja. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, tatizo la mipaka na suala zima la miundombinu hasa ya barabara inayopatikana katika maeneo ya *Selous,* ambapo mara nyingi sana wananchi wanapotumia huwa wanapata matatizo. Kwa mfano, watu wa Mloka, kule Rufiji, wanapopita katika maeneo haya, huwa wanabambikiwa kesi za ujangili.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa kadhia hii ya wananchi wetu katika maeneo yanayozunguka eneo la *Selous?*

**SPIKA:** Migogoro ya mipaka, tena mmeshaingia kwenye migogoro ya...

Mheshimiwa, kama unaweza kujibu? Lakini kwa kifupi sana, dakika moja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, nijibu tu kwa kifupi swali la nyongeza la Mheshimiwa Jafo, ambalo pia linazungumzia maeneo haya haya ya mipaka na maeneo haya haya yanayohusiana na mahusiano kati ya wananchi na wa hifadhi. Niseme katika mchakato ambao tunaupitia unaosimamiwa na Mheshimiwa Waziri, tunahakikisha kwamba, tunarekebisha migogoro iliyopo katika maeneo yetu ya hifadhi na wananchi, nchi nzima.

Lakini pili tunaangalia upya kuhakikisha kwamba, mahusiano mazuri kati ya hifadhi na wananchi wanaozunguka maeneo yetu yanaimarishwa na kunakuwa na ushirikiano kamili.

Na. 33

**Wawekezaji Katika Mbuga ya Serengeti**

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE** aliuliza:-

(a) Je, kuna wawekezaji wangapi kwa mchanganuo?

(b) Je, wawekezaji hao wanasaidiaje katika kuchangia maendeleo ya Wilaya ya Serengeti? Na kwa miaka mitatu iliyopita, wamesaidia kuchangia maendeleo kwa fedha jumla ya kiasi gani?

(c) Je, kuna watumishi wangapi kwa ujumla? Kati ya hao ni wangapi wanatoka Wilaya ya Serengeti?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, swali lenye sehemu *(a), (b)* na *(c),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizopo, hifadhi ya Taifa ya Serengeti ina wawekezaji 18 kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Kuna Loji tano ambazo ni *Serengeti Sopa Lodge, Serengeti Seronera Wildlife Lodge, Serengeti Serena Lodge, Four Season Safari (Bilila) Lodge* na *Lobo Wildlife Lodge.*

(ii) Makambi ya kudumu *(Permanent Tented Camps)* ya kulaza wageni 13, ambayo ni *Kusini Sanctuary Camp, Serengeti Soroi Camp, Grumet River Camp, Mbalangeti Tented Camp, Mbuzi Mawe Camp, Migration Camp, Lamai Camp, Sayari Camp, Singita Mara River Camp, Serengeti Bushtops Camp, Serengeti Pioneer Camp, Kirawira Luxury Camp* na *Serengeti Balloons Safaris Camp.*

Mheshimiwa Spika, wawekezaji hao wanasaidia kuchangia maendeleo ya Wilaya ya Serengeti kupitia tozo mbalimbali wanazotozwa na shirika. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti hukusanya tozo kwa wawekezaji waliopo ndani ya hifadhi ya Taifa ya Serengeti na sehemu ya fedha hizo hutolewa kwa wananchi wa Serengeti kupitia mpango wa ujirani mwema ili kuchangia maendeleo ya wananchi katika maeneo yaliyo jirani na hifadhi ikiwemo Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu Hifadhi ya Serengeti imechangia miradi mbalimbali ya maendeleo yenye thamani ya shilingi milioni 97, 431, 51kwa mchanganuo ufuatao;

Mheshimiwa Spika, 2010/2011 shilingi milioni 44.1, 2011/2012 shilingi milioni 40, 2012/2013 kwa maneno mengine hadi hapa tulipo shilingi miloni 13.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ni pamoja na ununuzi wa thamani katika shule ya Sekondari ya wasichana ya Mama Maria Nyerere, Ujenzi wa choo katika zahanati ya Bohu Sedeko, ujenzi wa mabweni ya wasichana kwenye eneo la kisangula, nata, machochweni na Isenya.

Mheshimiwa Spika, mwisho *lodge* na kambi za kulaza wageni zilizopo katika hifadhi ya Taifa ya Serengeti zina wafanya kazi 1056 na kati yao wafanyakazi 156 wanatoka katika Wilaya ya Serengeti.

**MHE. DR. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini ni ushauri wa bure wafanye utafiti upya kwa ajili ya *update* ya takwimu

walizonazo. Ni masikitiko makubwa hata *lodge* ambayo ni maarufu duniani na imeshinda zawadi mara mbili mfululizo mwaka juzi na mwaka jana sasa kwa *lodge* wengi wanaita *VIP lodge* haiko kwenye orodha hii.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji kwa takwimu wakati nimeleta swali hili kwa niaba ya wana Serengeti ziko *camp* na *lodge* hizi zipatazo 47. Kwa hiyo, naomba wa *update* takwimu hizo.

Mheshimiwa Spika, swali (a) Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya kazi na Serikali kwa ujumla wako tayari kushirikiana na Wilaya ya Serengeti na Mbunge? Ili kusudi hawa wawekezaji waweze kutoa mchango wao katika taifa na kwa Wilaya ya Serengeti?

Mheshimiwa Spika, (b) kwa kawaida inatakiwa 75% ya waajiriwa katika maeneo ya uwekezaji watoke kwenye eneo husika, lakini takwimu hizi ni asilimia 14.7 hali hii ni kuwaonea wana Serengeti. Serikali iko tayari kwa makusudi kabisa kufanya *operation* maalum kuweka usawia? Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba nijibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, moja niseme tu kwamba takwimu ambazo Wizara imezitoa hapa Bungeni zilikuwa zinahusu uwekezaji ulio ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, kwamba kuna *lodge,* kuna *tented Camps*, kuna *Mobile Camps* nyingi ambazo hazijahusishwa katika takwimu hizi ambazo tumezitoa na zipo katika maeneo mbalimbali yanayozunguka hifadhi ya taifa ya Serengeti na ikiwemo Wilaya ya Serengeti na niseme vilevile kwamba *VIP Lodge* ambayo katika miaka miwili mfululizo sasa imeshinda nafasi ya kwanza kuwa *lodge* yenye sifa na ubora ulitukuka duniani ipo katika Wilaya ya Serengeti lakini bado ipo nje ya hifadhi

ya Taifa ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, la pili la Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara tutafanya kila jitihada za makusudi kushirikiana na Wilaya ya Serengeti, moja ni suala zima la utambuzi wa uwekezaji ambao kwanza tunauhitaji uliopo katika maeneo yanayozunguka hifadhi ya Taifa kwa sababu wote wanaowekeza ni kwa sababu waweze kuingia katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pili uwekezaji huu uweze kuwa na tija moja kwenye ajira za watu wetu na pili katika maslahi mengine ikiwa ni mapato kwa Halmashauri asante.

**SPIKA:** Ahsante sana waheshimiwa tunaenda kwa muda matangazo ya kazi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa umoja wa Wabunge wanawake naomba nianze zile kazi za Bunge kwanza. Wajumbe wa kamati ya kilimo, mifugo na maji Profesa Peter Msolwa naomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Namba 231 hii Kamati ya kilimo, mifugo na maji.

Halafu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wanawake *TWPG* Mheshimiwa Anna Abdallah anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wanawake wote kuwa tarehe 13 na tarehe 14 Aprili, 2013 kutakuwa na vikao vya mafunzo Chuo kikuu Dodoma *(UDOM)* yaliyoandaliwa na Shirika la *Oxfarm* kikao kitaanza saa nne asubuhi yaani kule *UDOM* kuna mafunzo yanaendelea juu ya wanawake. Kwa hiyo, tarehe 13 na tarehe 14 Aprili, 2013 mnaruhusiwa takribani wanawake 300 kutoka mikoa yote Tanzania.

Masuala yatokayojadiliwa pamoja na unyanyasaji wa wanawake *violence against women* ya pili uwezeshaji wanawake kiuchumi *(Women Economic Empowerment),* halafu na nyingine umilikishwaji wa rasilimali *ownership of resources. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wanawake wote wanaombwa kuhudhuria mafunzo hayo muhimu kwani itakuwa fursa nzuri kwao kubadilishana uzoefu na wanawake wengine kutoka katika maeneo yao.

Tangazo la mwisho ni la Mwenyekiti wa *APNAC* Dkt. Mary Mwanjelwa anaomba niwatangazie wajumbe wa *APNAC* kuwa leo kutakuwa na kikao chumba Namba 227 katika jengo la utawala hawajataja chumba lakini mtajua wenyewe mpo wachache jengo la utawala kikao cha Kamati Kuu siyo wabunge wote.

Nani alisema Mwongozo dakika mbili maana yake tunaenda kwa utaratibu.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nasimama kwa Kanuni ya 68(7) hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika. Kwa ajili ya muda naomba nisimalizie yaliyopo hapa.

Lakini ninakwenda kwenye wakati wa swali Namba 31 linajibiwa kuanzia aliyeliuliza na aliyekuwa akilijibu picha iliyopo ni kwamba mwanaume anayefanya urafiki au mapenzi na kiwete ni udhalilishaji mimi ninavyofahamu.

**SPIKA:** Hoja ni nini sasa.

**MHE.ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, hoja ni kwamba wananchi huko nje wataelewa kwamba kuoa au kutembea na kiwete ni makosa. Mheshimiwa Spika nilitaka mwongozo wako.

Je, ndivyo wananchi waelewe hivyo?

**WAZIRI YA NCHI,OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kufafanua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi kama mama nimeguswa na wale wanaume ambao wanafanya mapenzi na walemavu kama vile viwete halafu wanawatelekeza baada ya kuwazalisha.

Mheshimiwa Spika, huo ni udhalilishaji wa hali ya juu sana. Unamzalisha mlemavu halafu unamtelekeza jamani, kweli, huo ni ubinadamu kweli! Wanaume. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya tumeelewa, nadhani ilitakiwa ieleweke kwamba unakwenda kumwona maskini huyu dada au mtoto huyu unamfanyia vitendo vibaya halafu unaenda zako. Unaenda zako wala hujulikani kufanya mapenzi ni hata na hao kama kweli wewe ukaonana na ndugu zake, ukafanya nini na kwamba utamtunza, kwa hali yake yote ile hakuna anayekataa.

Nadhani tulielewa hivyo. Naona wengine *speed* ya muda hawajapata tuna Makamu Mwenyekitiu wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria na Utawala anaomba niwatangazie wajumbe kwamba saa saba mchana watakutana kwenye ukumbi wa Msekwa C. Katibu tuendelee.

Waheshimiwa Wabunge kwa utaratibi tuliojipangia asubuhi hii tutakuwa na wazungumzaji 18, jioni tutakuwa na wazungumzaji 17 tunakwenda kwa mujibu wa saa. Kwa hiyo, tuendelee kama jana msipoteze muda mzungumze kwenye *point* na mjiandae vizuri. Kwa hiyo msemaji wangu wa kwanza leo atakuwa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kasembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister A. Bura.

**MHE. MWIGULU N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nilikuwa JKT Msangi kule alikuwepo Afande Mbweya na Shigongo na nilihitimu *AG 0593.*

*Sasa* nianzie kwenye suala la elimu jambo la elimu na hususani kwenye elimu ya Sekondari kufuatia matokeo yaliyojitokeza, napenda nitoe mchango na naomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania mnisikilize kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, katika elimu ya Sekondari nchi yetu inapita katika kipindi cha mpito. Ikumbukwe kwamba tangu uhuru, tangu Serikali ilipotaifisha shule za Sekondarji za Misheni kila mmoja aangalie kwenye mkoa wake Serikali haikuwahi kujenga shule nyingi za Sekondari kama ilivyojenga katika awamu hii kwenye shule za kata na kufuatia ujenzi wa shule nyingi kwa aina hiyo kwa ghafla na kufuatana na mahitaji kwamba wanafunzi wengi sana walihitajika kwenda ni lazima upungufu wa aina nyingi wa mahitaji yanayotakiwa shuleni ungejitokeza.

Mheshimiwa Spika, moja ya kitu ambacho kimejitokeza ni kwamba shule nyingi sana zimejengwa kwa mara ya kwanza tangu uhuru imekuja kutokea kwamba Walimu wakakosekana kabisa kabisa. Yaani Serikali haina mahali pa kutoa walimu wote wanaotoka mashuleni wanapelekwa moja kwa moja kwenda kufundisha na hili limejitokeza na Serikali ikachukua jitihada za kupandisha baadhi ya vyuo na kupanua vyuo vya walimu.

Sasa kufuatia rai ya Waziri Mkuu mimi ningeomba Wabunge tuielewe hiyo kwamba hili si la kunyoshea mtu kidole kwa sababu hamna yoyote yule ambaye anaweza akasema kwamba Serikali ingetoa wapi Walimu.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia hata kwenye hiki kitabu, niliona tu kuanzia nje walikimbilia tu kusema Waziri wa Elimu ajiuzulu hivi akishajiuzulu ndiyo anaenda kufundisha kwa sababu la kwanza tungesema hivi Walimu hawapo hata kutoka nje ya nchi. Sasa nilitegemea waje na mawazo mapya kwamba kufuatana na kwamba hakuna walimu kabisa kabisa sisi maoni yetu ni haya badala yake.

Kurasa 70 zinakuja zote zinalalamika. Wananchi wanalalamika na viongozi wanalalamika huku wanasema wanatamani nchi. Mnatamani mkafanye nini wakati hata mawazo mbadala hamna. Hivi hamjawahi kujua kwamba huwa hamchaguliwi kwa sababu hamna mawazo mbadala mnalalamika, mnalalamika *page* 70 hivi hii ni maoni ya kambi ya upinzani au malalamiko ya kambi ya upinzani *what is this?*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ili nisilalamike naomba nijikite kwenye ushauri wangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa Serikali imemaliza kabisa kabisa walimu kwamba inasubiria tu wale wakimaliza ndiyo iwapangie na shule tumejenga zinakuwa na walimu wawili wengine watatu, hakuna pa kuwatoa walimu.

Lakini hapa hapa nchini tuna wataalam wetu ambao wamemaliza vyuo, wapo wa vyuo vingine ma-*engineer,* wanasheria wapo kila mtaa hawana kazi. Mimi naomba Serikali pamoja na Bunge tufanye mambo mawili.

Kwanza tubadilishe sheria inayosema mwanafunzi wa Sekondari anatakiwa afundishwe na mwalimu tuseme mwanafunzi wa Sekondari atafundishwa na *lecturer*, *lecturer* wa Sekondari halafu tukishasema atafundishwa na *lecturer* tuwachukue wa-*engineer* popote pale walipo wajiandikishe wakafundishe. Mimi siamini kama *engineer wa* chuo kikuu cha Dar es Salaam atashindwa kufundisha mwanafunzi wa *Form two.*

Mheshimiwa Spika, siamini kama Mwanasheria atashindwa kufundisha *language* ya *form one* tuwachukue halafu tuwalipe kama *engineer* anayelipwa aliyeko Wizarani halafu wapande na cheo *senior one, senior two* kama aliyeko Wizarani.

Kwa nini tuna wataalam waliosoma kwa fedha za Serikali wapo hawana kazi halafu tuna *form one* hana mwalimu. Mbona wanafunzi anafudishwa na *form six*. Ukikuta shule ya kata imefaulisha kidogo ujue wale *form six* wamejitolea tolea kufundisha ndiyo wale wakafanya vile. lakini tuna wahandisi, tuna wachumi, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili tubadilishe utaratibu wa malipo kule jeshini kuna maafande, kuna maaskari na kuna maofisa tuwalipe kama wale wanavyolipa mawizarani, kwa hiyo, hilo litafanyika.

Lakini jambo la pili tatizo la mambo yote kwenye elimu ni suala la kibajeti, ni suala la kibajeti na Waziri Mkuu utagombana sana na walimu lakini kama hatutabadilisha uwekezaji kwenye elimu utagombana mpaka mwisho. Jambo la kufanya hapa tuongeze fedha zilizotengwa kwa ajili ya walimu, tuwalipe tumalizane nao, kwa sababu kama Bajeti inaendelea kama ile ile ya wakati shule ziko chache, walimu wameongezeka, shule zimeongezeka, fedha ya vitabu itatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa kengele ya kwanza imeshagongwa nihamie kwenye jambo lingine. Lakini jambo la pili ninalotaka kufafanua na hili nawaomba Watanzania msikilize kwa umakini sana. Kuna jambo la kigaidi limeandikwa hapa *page* karibu nne.

Kwa masikitiko makubwa mnapotosha mpaka mambo yanayohusu maisha ya watu, mnapotosha eti Usalama wa Taifa, eti Polisi wala msihangaike na kwenye jambo hili nasema wala msihangaike na Usalama wa taifa, wala polisi jambo la ugaidi ni jambo la mkanda, aliyerekodi ule mkanda yupo tayari kusema popote, aliyeniletea yupo tayari kusema popote na mimi niko tayari kusema mahali popote.

Mheshimiwa Spika, Chadema walipanga kuteka na kuua, walipanga yule kijana wa Igunga walipanga kumwua na huyu mwandishi waliyekuwa wanamwongelea walipanga kumwua halafu wanadhania eti picha imetengenezwa. Sasa kwa taarifa zenu hata pale walipokuwa wanaongea yule aliyekuwa anaongea alikuwa anaandika mpaka na ile karatasi aliyekuwa anaandika hii hapa *finger print* ya kwake, mwandiko wa kwake na hivi vyote vimeshafanyiwa kazi vimepatikana ni yeye na pale palipo fanyikia ni kwake aliyekuwa anarekodi amekubali amesema atatoa huo ushahidi, aliyeniletea atatoa na mimi nitatoa popote mahakamani, polisi, Bungeni na hata mbinguni nitasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapanga kuua na unapanga kwamba kiasi gani tutatengeneza isionekane Chadema ndiyo imefanya haya na lile mnalosema ipendekezwe tume pendekezeni kwa sababu si viongozi wote wa Chadema wanapenda yale mauaji kwa sababu hata lile lililofanyika majibu wanayo eti kiongozi anaandika kwamba anayewasiliana na gaidi naye aunganishwe na ugaidi.

Hivi eti anasema viongozi wa CCM lakini hebu fikirieni yule aliyekuwa anapanga yale mauaji ni Mkurugenzi wa Ulinzi na Usalama wa Chadema inamaana anawasiliana na viongozi gani kama siyo wale wakubwa zake na ndiyo wanaomwagiza apange yale.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kumtetea mtu kabla hata haijafika mahakamani inadhihirisha ule ulikuwa ni mpango wa chama na kwa kauli hii hapa ambayo ameandika kiongozi wa kambi ya upinzani ukurasa wa 31 kwamba viongozi hawa wanao wasiliana nao wawajibishwe kwa maana hiyo Jeshi la Polisi kuanzia leo hii nashukuru Mbowe hayupo hapa. Kwa hiyo, ndiyo inawezekana wameshamkamata kwa sababu yeye ndiyo anayewasiliana zaidi na Lwakatare, Katibu Mku wake naye ameshamtetea naye aunganishwe kwa sababu ameandika mwenyewe kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Ugaidi mtu yoyote anayefanya mawasiliano na gaidi au magaidi yeye pia anahamasisha ugaidi na yeye anastahili kuunganishwa na tuhuma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kiongozi ambaye ndiyo Mwenyekiti na Katibu wa Chama kile yule aliyekuwa anapanga ni *subordinate* wao na fedha walizokuwa wanatumia kuwalipa wale vijana zilikuwa za Chama chao. Kwa hiyo, waunganishwe, Polisi mnasubiri nini watu wameshaomba wenyewe waunganishwe?

Sasa mnakuja na mlolongo wa malalamiko oooh! *Zero* nyingi! *zero* nyingi! Tukiulizana hapa hivi *zero* zimeanza leo ungekuwepo Mbowe ningekuuliza wewe ulipata nini mnachochea vijana wa watu wakasirike huku mnapanga kuua halafu mkishapanga mnawahi kama mchawi anayeloga, halafu anawahi yeye kwenda kulia na kugaragara msibani.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hili la mauaji Chadema nawaomba mfanye vitu viwili kwanza kimbieni haraka sana kwenye kanisa lililo karibu au msikiti ulio karibu mkatubu dhambi ya kupanga kuwaua watu wasio na hatia mkishamaliza hilo mrudi mkaombe radhi kwa Watanzania *you look merciless, shameless* unatafuta uongozi huku unaua watu, *look at you*.

Mheshimiwa Spika baada ya hapo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mustapha Akunaay, *time, time please!*

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, mzungumzaji aliyepita, kwa kanuni ya 68(2), amezungumzia kitu ambacho ni *sub-judice,* kitendo ambacho kiko Mahakamani hakiwezi kuruhusiwa kuzungumziwa Bungeni.

Pili, Mbunge haruhusiwi kuzungumza mambo yanayomhusu Mbunge mwingine moja kwa moja. Naomba aondoe hiyo kwa kuzingatia kanuni hiyo.

**SPIKA:** Sawa nakubali na ni vizuri wote mkaheshimu kanuni hizo.

Tunaendelea! Mchangiaji wangu wa pili, ni Mheshimiwa Mariam Kasembe.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Tumemaliza hilo, kwa sababu unajua ninachosema, wote mnatakiwa ku-*observe rules*, siyo mkuki kwa nguruwe kwa mmoja na mwingine siyo mkuki, siyo sahihi! Tunaendelea! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Tunaendelea Mheshimiwa Kasembe!

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Katika hotuba hii nitajaribu kuchangia katika eneo la utawala, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na nikipata nafasi na masuala ya nishati.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la utawala ukurasa wa 70, Serikali imeelezea jinsi ambavyo imejitahidi kuanzisha Halmashauri 31 ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Lengo kubwa la Serikali kusogeza huduma hizi karibu na wananchi ni kuharakisha maendeleo. Nilivyokuwa napitia katika ukurasa huu, niliona Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea jinsi atakavyojitahidi kugawa rasilimali watu, vitendea kazi kwa uwiano ili kuharakisha maendeleo katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo binafsi limenipa wasiwasi, nilivyokuwa naangalia fedha zilizotengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Halmashauri ya Mji, ukilinganisha na matatizo yaliyojitokeza katika Wilaya ya Masasi, maafa yaliyojitokeza katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Halmashauri ya Mji, sasa hivi Halmashauri zote mbili, hazina vitendea kazi vya kutosha na hazina ofisi na zimepoteza mali nyingi, kwa mfano, magari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naangalia katika fedha zilizotengwa, nikawa najiuliza, je, fedha hizi zitaweza kutosheleza kutatua tatizo lile kubwa ambalo limejitokeza katika Halmashauri hizi mbili? Au je, Serikali ina mpango wowote au kuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kwenda kutatua matatizo haya yaliyojitokeza huko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anatoa majumuisho, atoe ufafanuzi kama wataweza kusaidia katika yale yaliyojitokeza kwenye Halmashauri zote mbili.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwenye suala la mafunzo ya kijeshi, imeelezwa kwamba, Serikali imeendeleza jitihada za kuchukua vijana kwa ajili ya mafunzo ya kijeshi, lakini vile vile wamewachukua vijana wetu hawa *form six* ambao wanaendelea kwa mujibu wa sheria. Naomba niwazungumzie wale vijana wanaokwenda kwa ajili ya kujitolea.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa ni wengi, wanafanya kazi nzuri, ni wakakamavu na wamepata mafunzo ya kutosha. Inasikitisha sana vijana hawa wanakaa kambini mwaka

mzima, wanafanya kazi za kujenga nchi, lakini baadaye wanakuja kukosa nafasi za kuajiriwa, inabidi warudi majumbani.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali, tumekuwa tukitoa nafasi za ajira huku nje, kwa mfano, nafasi za Polisi, Jeshi, Magereza na Uhamiaji. Naiomba Serikali, sasa hivi tungefuta kabisa utaratibu wa kutangaza nafasi hizi nje; lakini tukaenda moja kwa moja kwenye Jeshi la Kujenga Taifa na kuwachukua vijana ambao tayari wamekwishapata mafunzo. Vijana hao ndiyo wawe wanachukuliwa na kupelekwa kwenye Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Uhamiaji pamoja na Jeshi la Wananchi ili kuwasaidia vijana hawa, kwa sababu vijana hawa wana elimu ya kutosha, wapo vijana wa *form four*, *form six* na vyuo, lakini vile vile wapo vijana wa darasa la saba ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ichukue ushauri wangu huu. Haina maana yoyote tunatangaza nafasi hizi huku nje, tunachukua vijana walioko mitaani, wakati kwenye Jeshi la Kujenga Taifa wapo vijana ambao wako tayari na wangeweza kuwa askari wazuri katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niungane mkono na Mheshimiwa mwenzangu ambaye jana alizungumzia suala la kupeleka mafunzo ya ufundi katika Jeshi la Kujenga Taifa. Vijana wetu walioko katika Jeshi la Kujenga Taifa ni wengi, kama tungekuwa tumeanzisha Vyuo vya *VETA* katika makambi haya, nafikiri vijana wetu wangeweza kunufaika zaidi, ili wale ambao watakuwa wanakosa nafasi za ajira, Serikali iwaandalie vitendea kazi, wanapomaliza wakirudi majumbani waweze kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la nishati. Serikali imekuwa ikiendeleza jitihada za kusambaza umeme vijijini, nilipokuwa naangalia hotuba ya Waziri Mkuu, nimeona katika Mikoa ambayo itanufaika na mpango huu wa kusambaza umeme vijini kwa awamu hii ya kwanza, Mikoa ya Mtwara na Lindi ipo.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kuzungumzia hapa ni kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea katika Mikoa hii, alielezea vijiji ambavyo vinatakiwa kusambaziwa umeme kwa awamu ya kwanza na awamu ya pili. Nataka niambie Serikali kazi hii inakwenda taratibu mno na imeshaanza kuwakatisha tamaa wananchi, kwa sababu nguzo zimesambazwa na hakuna kazi yoyote inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nafuatilia niliambiwa kwamba, vitendea kazi hawana. Naiomba Serikali, kama kweli tumekusudia kusambaza umeme vijijini na kama kweli tuna nia ya kuwasaidia wananchi wapate umeme, naomba ijitahidi sana kupeleka vifaa vya kutosha ili kazi hii iweze kuendelea. Kwa sababu kama hii awamu ya kwanza, wale waliopangiwa kupata umeme hawataweza kupata kwa wakati, ina maana kazi ya kusambaza umeme vijijini itachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi walipata punguzo la bei ili kuwasaidia kunufaika na nishati hii ya gesi. Bei iliyokuwa imepangwa ilikuwa ni shilingi 99,000/, lakini naomba niambie Serikali kwamba bei hii haikuwa wazi. Kwa hiyo, wananchi wengine wamekuwa hawaitambui, tumefanya kazi ya ziada ya kuwaelimsha, lakini wanapokwenda *TANESCO* imekuwa ni kama *favour*, wengine wanaambiwa kwamba ni 99,000/= na wengine wanaambia bei nyingine. Naomba Serikali irejee tena kutamka hii bei iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile muda ulikuwa umepangwa kwa bei hii. Naiomba Serikali ule muda uliopangwa hautawanufaisha wananchi kwa sababu muda ule ni mfupi na ukizingatia kwa mfano, wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi, mwaka huu wameyumba sana katika kuuza korosho. Kwa hiyo, wananchi wengi wameshindwa kujiandaa katika kufanya *wiring* katika nyumba zao. Naiomba Serikali irejeshe tena suala hili la punguzo, tuweze

kuongezewa muda, ikiwezekana mngetuwekea muda wa miaka mitatu mpaka pale tutakapohakikisha kwamba, umeme vijijini umeweza kusambaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nisipoteze muda sana, naomba yale ambayo nimeyaomba kwa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha, hasa kwenye eneo la utawala yaweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile sisi watu wa Mkoa wa Mtwara, Ruvuma na Lindi, tuliomba mgawanyo wa Mkoa, lakini Mikoa ilipotangazwa tulipigwa na butwaa kuona kwamba sisi hatumo. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atuambie, hili ombi la Mikoa ya Kusini linakwama nini? Rais alipokuja kuomba kura, wananchi walimweleza kwamba, tunayo mahitaji ya kutaka Mkoa. Rais aliahidi kuwa, kabla hajamaliza kipindi chake, ataweza kulitekeleza hilo. Sasa miaka inakwenda, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anajumuisha atuambie, wapi tunakosea na nini tunatakiwa kufanya kwa sababu bado tunahitaji kupata Mkoa wa Kusini, unaojumuisha Wilaya ya Masasi, Nanyumbu, Tunduru pamoja na Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Aliko Kibona, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niende moja kwa moja katika kuchangia hoja iliyo mbele yetu, nikianza na elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pole kwa vijana wote waliofanya mtihani mwaka uliopita na wamefeli na pia nitoe pole kwa wazazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo…

**SPIKA:** Ndiyo umechangia hivyo!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Wazee wetu Tanzania nzima waliwekeza katika elimu kwa ajili ya watoto wao, kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne. Wengine waliuza mashamba, wengine waliuza mifugo. Matokeo yaliyokuja imekuwa ni masikitiko.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri, tusije na majibu mepesi katika jambo hili gumu, Mimi kule Mbeya ni mdau wa shule moja ya Sekondari inaitwa Lutengano. Shule ile ina Walimu wa kutosha, lakini watoto wamefeli. Shule ile tunawalipa Walimu wale vizuri lakini watoto wamefeli, shule ile watoto hawaendi na simu shuleni, lakini watoto wamefeli. Naomba tusubiri majibu ya Tume ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuone itatuletea nini.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ningependa kushauri hata kabla Tume haijaja, ili kuwaondolea kero na masikitiko makubwa wazazi wote waliopo katika nchi hii, watoto wetu, tuchukue sasa matokeo ya *Mock* na maendeleo ya mtoto kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne. Hayo yatumike katika maamuzi ya ama huyu mtoto amefaulu aweze kuendelea na kidato cha tano au aweze kupewa daraja sawasawa na alivyopata katika mitihani ya *Mock*.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa kama tu, Waziri atasema mitihani ya *Mock* ni geresha, basi tutakuwa na sababu ya kusema hawa watoto wameingia hasara kwa matokeo yaliyotoka. Kwenye eneo la elimu wazazi huko vijijini wanalalamika kwa kitu kinaitwa ada au malipo ya kulipia mtihani. Malipo kwa ajili ya mitihani ni kero, naomba Wizara iangalie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Tume ya Waziri Mkuu inaendelea na kazi, nisingependa kusema mengi juu ya upande wa elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kidogo kuhusu afya. Nawapongeza wenzetu wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri, lakini niende kwenye kipengele kimoja ambacho kanalalamikiwa na wananchi ambacho ni Vyuo. Hospitali

zetu nyingi vijijini hazina wataalam, vituo vya afya havina wataalam, zahanati hazina wataalam, Serikali imeendelea kufanya juhudi kuongeza idadi ya wataalam, lakini kilichotupata tulio wadau kwenye Vyuo mbalimbali vya Afya ni kiwango au *qualification* zinazotakiwa kwa mtoto kuingia kwenye Vyuo vya Afya. Eti tunaambiwa mtoto awe amepata *C* tatu na hizo *C* zitokane na masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, naomba wataalam waliangalie vizuri hili, limekuwa ni kero. Kuna manung'uniko huko nje, kwamba vyuo vingi ni vya *mission*, kama Mnero, kama Bumbuli, Nkasi kule na sehemu nyingine, *KCMC*. Uongo uliojitokeza sasa ni kwamba, kule Wizarani kuna mkakati wa kuhakikisha hivi vyuo havisajili, haviingizi watoto wengi kwa ajili ya kusoma masomo ya afya. Naomba wahusika waliangalie hili ili kukomesha uongo huu. Turudishe sifa zile za kwanza ili tuweze kupata wataalam wengi katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, Kasi ya ujenzi wa Zahanati ni ndogo mno. Tulipokuwa tunaomba kura kwa ajili ya uchaguzi uliopita, akinamama wengi vijijini na wananchi walitupa kura kwa sababu tulionesha kwamba Chama cha Mapinduzi kitajenga Zahanati katika kila kijiji. Kasi ni ndogo, naomba Waziri Mkuu, naomba wahusika tafadhali na wadau wote, hili jambo tuliangalie kwa sababu mwisho wa siku tutaonekana waongo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie kidogo kuhusu ulinzi. Hali ya usalama katika nchi yetu, naweza kusema ni tofauti na nilivyosoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tangu nimezaliwa ni muda mrefu sasa, nilikotoka ni mbali kuliko ninakokwenda, sijawahi kusikia *RPC* anauawa, sijawahi kusikia Kituo cha Polisi kinakwenda kuzingirwa na wananchi wanaoitwa kwa msamiati wa sasa hivi, wananchi wenye hasira kali. Sijawahi kusikia *Traffic* anapigwa makofi na dereva, sijawahi kusikia ni katika kipindi hiki ambacho tumeingiza dhana inaitwa ulinzi shirikishi, Polisi Jamii.

Mheshimiwa Spika, hiki kitu binafsi nakilaani, wenzetu kule Malawi walijaribu wakasema tuanzishe kitu kinaitwa

*Police Service* wakashindwa, wakarudi kwenye *Police Force*. Wataalam wastaafu ukiongea nao wale wazee wetu waliokuwa kwenye Jeshi la Polisi, hiki kitu kinaitwa Polisi Jamii wanasema, tuliposikia nchi inapokea kitu kinaitwa Polisi Jamii, tukajua mambo yameharibika na kweli mambo yameharibika. Ndiyo sasa tunaona hata *RPC* anauwawa. Nafikiri tufanye tathmini, jambo lolote ukiona hali ni mbaya, Polisi wanapigwa, Vituo vya Polisi vinavamiwa na kuchomwa moto.

Zamani tulikuwa tukisikia Polisi tulikuwa tunaheshimu kama dola, sidhani kama tunakokwenda Polisi tena inaoneka ni chombo cha dola, kitaonekana ni chombo cha mitaani. Wananchi hawajaelewa maana ya Ulinzi Shirikishi au Polisi Jamii, naomba wahusika walichukue hilo na tathimini iweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kuhusu viwanda. Nasikitika katika Mkutano uliopita niliwahi kuuliza swali kuhusu uwezekano wa kufufua Kiwanda cha Zana za Kilimo pale Mbeya. Majibu mepesi yalipatikana, tukaambiwa kwamba, aliyekuwa ameomba kuendeleza kiwanda kile hawezi kufanya kazi ile. Amefanya tathmini upya, ataingia hasara, kwa hiyo, anabadilisha, kitakuwa sehemu ya kutengenezea bia, kutunzia makreti ya bia, vitu kama hivyo. Wananchi wanalalamika, wanasema, kama yeye ameshindwa, ni vizuri tenda ingetangazwa upya. Lengo letu sisi tupate vifaa kwa ajili ya kilimo vikiwa jirani na nafuu.

Mheshimiwa Spika, naomba hilo lichukuliwe na liangaliwe upya, kama kwa kiwanda hiki haitawezekana, uwekezaji mwingine utakaokuja baada ya huu kushindakana, ni vizuri tukawa waangalifu kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie maji; nashukuru kwamba Serikali imeendelea kufanya juhudi kwa ajili ya kuwaletea maji wananchi wa vijijini. Lakini kule kwangu naendelea kulia, Mji wa Isongole naweza kusema unaongoza kwa shida ya maji katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitazame hilo aweze

kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Ileje, sehemu zile zinazoitwa Isongole na Itumba.

Mheshimiwa Spika, wapo wenzetu pale Tunduma...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa ajili ya nafasi hii, lakini Tunduma pia wapewe maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa atafuata Mheshimiwa Mwijage!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA** Tutumie muda mfupi jamani. Enhe!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 68(7). Naomba Mwongozo wako kuhusu Kanuni ya 64(c) na (f) iliyovunjwa na mzungumzaji, Mheshimiwa Mwigulu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Akunaay aliomba kuhusu utaratibu. Kwa kawaida, kikanuni ulitakiwa umkalishe Mheshimiwa Mwigulu akae chini, halafu afute kauli yake, lakini kiti kikamlinda.

Mheshimiwa Spika, umesema Wabunge wengine wasiendelee kuvunja hiyo Kanuni. Naomba Mwongozo wako, tutafuataje hii Kanuni wakati kiti kimemlinda Mheshimiwa Mwigulu mpaka amemaliza, anatukana na hakufuata kanuni? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge nasema hivi, wote tushikilie taratibu hizi. Jana tumeacha hotuba nzima imesomwa mpaka ikamalizika. Ndiyo maana nasema kuanzia

sasa, wote mu-*observe*, jana yalizungumzwa, hotuba nzima ilisomwa tukanyamaza, kwa hiyo sasa nasema tu- *observe* kanuni zetu.

Tuendelee na mchangiaji anayefuata, Mheshimiwa Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nisije nikapanda presha nikasahau, naunga mkono bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na takwimu, sina tatizo na maelezo, nimekuja hapa kuendelea kushauri. Nimekuja kushauri, sisi Wabunge tumefanya kazi, tulipokuwa Majimboni tumefanya kazi, kama unasema kazi haijafanyika ina maana miaka miwili na nusu imepotea bure. Tumefanya kazi kweli, tumejenga madarasa, madaraja na barabara. Nimekuja hapa kushauri, na zaidi nimekuja hapa kuomba ili waniongezee. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la chakula na njaa. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia alivyosambaza chakula takribani tani 69,000, hiki ni kiasi kikubwa sana cha chakula. Tungeelezwa gharama za kusafirisha, tungegundua ni fedha kiasi gani imetumika.

Naishauri Serikali yangu kwamba, pamoja na jitihada hizi Serikali isaidie hali ya hewa waweze kuwasaidia wananchi kutabiri ni msimu gani wa kulima. Wananchi wa mikoa ya kati ambao hali ya hewa imewachenga, mazao yao yameharibika. Laiti kama tungekuwa na hali ya hewa yenye mamlaka, yenye uwezo, watu hawa wangeambiwa wakati gani wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania nzima nashauri Ofisi ya Waziri Mkuu hatuna haja ya kuvumbua kitu kipya, turudi kwenye misaafu yetu ya zamani, tufanye kazi kwa operesheni. Operesheni kama Kilimo cha Kufa na Kupona, zimekwisha, hazisikiki. Kumbe basi wananchi wetu wanapaswa

kukumbushwa, ni wakati gani wa kulima na wakati gani wa kupanda na ukitilia maanani tatizo la chenga za hali ya hewa,naendelea kushauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejikita kulima maeneo ambayo yanaonesha tija kubwa kwenye mazao ya nafaka, *SAGCOT*, mambo ya Sumbawanga, Peramiho na sehemu kama hizo. Lakini ukitathmini tani 69,000 zilizosambazwa utakuja kugundua kwamba pamoja na uzuri wa mpango huo iko busara na maeneo ya Kanda ya Kaskazini, upande wa Kanda ya Ziwa kuna haja ya kuanzisha mashamba makubwa.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa unajadili bajeti unajiandaa kwa ajili ya bajeti ijayo. Bajeti ijayo naishauri Serikali yangu, mjiandae kusudi muweze kutumia bonde la Mto Ngono, kwetu kuna bonde kubwa linaitwa Mto Ngono. Lazima tuzalishe kwa wingi katika bonge lile, tuzalishe nafaka, tuzalishe mpunga, kusudi tuweze kutumia pale, lakini zaidi tuokoe gharama za Serikali kusafirisha chakula kutoka Peramiho mpaka Bukoba. *(Makofi)*

Mtu anayejua *economics,* hawezi kusafirisha chakula kutoka Peramiho kupeleka Bukoba wakati Bukoba kuna milimita za mvua 1100. Lakini tija nyingine ni kwamba watu wa Mahalia watapata fursa ya kushughulika katika shughuli zile. Lakini faida nyingine ya ziada, Kagera au Bukoba kama anavyosema Mzee Mulokozi, Mkuu wa Mkoa wa Kagera anaitwa Mzee Mulokozi, anasema Kagera ndiyo *hurb of Central Africa, The great central Africa,* kwa hiyo, kama mkizalisha pale chakula kitatoka Bukoba kwenye bonde la Mto Ngono na kwenda kuuzwa Sudani na Kongo – DRC.

Mheshimiwa Spika, naisaidia Serikali yangu na hasa bwana Mipango afikirie, chukueni takwimu za chakula kilichopita bandari ya Dar es Salaam kikienda DRC – Congo na Burundi, *massive*. Tunaweza kuwekeza katika kuzalisha chakula kwa kuzilenga nchi jirani, tukapata fedha nyingi na kama alivyosema rafiki yangu Mheshimiwa Keissy tukaepukana na bajeti tegemezi. Mchango wangu kuhusu chakula ni huo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie maisha ya visiwani na shughuli za uvuvi. Najua kuna watu wengine hawaelewi, mtu wa Kerebe na wa Bumbile, yeye uvuvi ndiyo shughuli yake aliyozaliwa nayo. Kwa hiyo, naishauri Serikali yangu pamoja na jitihada za kupambana na uvuvi haramu, nashauri wale watu wa mahali asilia, wazaliwa wa sehemu zile, wawezeshwe kwa nguvu waweze kukabili haya maingilio mapya, hawa watu wenye mitaji mikubwa na teknolojia, kinyume cha hapo tutaendelea kushuhudia uvuvi haramu na samaki wa Ziwa Viktoria ambao watu wote mnawapenda watatoweka. Ndiyo njia rahisi, wale watu wa mahali asilia ndiyo watakaokuwa walinzi na hakuna mtu atakayeharibu Ziwa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye elimu. Wamezungumza mengi na wameandika mengi kuhusu elimu. Niwaambie kitu kimoja, mimi nimesoma *decision making*. Katika *decision making* kuna kitu kinaitwa *inquiry* au *probe team* ambayo Watanzania wengi nimeshuhudia hata kwenye magazeti na hata kwenye taarifa za watu wengine hawaelewi kwa nini tunaanzisha Tume.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya sababu za kuanzisha Tume ni kuthibitisha kwamba kile tunachokijua kweli ndivyo kilivyo, yaani unaanzisha Tume kuthibitisha kwamba mtoto amefeli kwa sababu amekwenda shuleni bila kula chakula, unajua amekwenda bila kula chakula na unaunda Tume. Sasa inakusaidia nini? Baadaye kwa pamoja baada ya Tume, mnakubaliana kwamba hili ndiyo hili.

Mtulie taarifa itoke, Tume ya Waziri Mkuu ije itueleze tujue. Wengine wanaolalamika tangu wamalize shule kwenye shule aliyosomea hajawahi kupeleka hata penseli, unasema nini wewe? Unawajua Walimu wako waliokufundisha? Unasema nini? Naogopa majibu ya Ofisi ya Waziri Mkuu yanaweza kutufanya sisi ni watuhumiwa na tukafungwa, Mungu apishie mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumze jambo lingine. Mimi nimetembelea Jimbo langu, kuna tatizo nimeliona sijui kama

Tume italiona. Mafanikio ya Chama changu katika kuzuia vifo vya watoto wadogo wa umri wa miaka sifuri mpaka mitano (0- 5) kumepelekea changamoto ya watoto wengi kuingia shuleni. Ni changamoto, tumefanikiwa kuzuia vifo, watoto wako wengi shuleni. Shule moja yenye vyumba saba ina watoto 700. Ndugu zangu, viongozi wenzangu, Waheshimiwa Wabunge tusife moyo. Kwa hiyo, changamoto tunaitatua kwa kujenga madara zaidi.

Tulichaguliwa kuwa viongozi, kiongozi ni kama kijiko cha jikoni, hakiogopi moto. Tujenge madarasa mengine, tujenge vyoo vingine, lakini Serikali mhahakishe, mtu yeyote mwenye *certificate* ya ualimu, mtangaze tunapomaliza Bunge hili aende aajiriwe. (*Makofi*)

Kuna Walimu wengine hawajapata ajira, kuna wengine wameamua sasa kwenda kwenye ualimu waambie hata waliomaliza mwaka 2003 kama wana sifa za kwenda chuoni, waende kwa sababu kipaumbele cha kwanza ni elimu, kipaumbele cha pili ni elimu na atakayeikomboa nchi hii anaitwa elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumze tatizo la Walimu. Walimu pamoja na matatizo yao kuna mtu anakula fedha zao. Kuna makundi ya Taasisi za *Microfinance*, zinakula fedha za Walimu. Naiomba Serikali yangu isaidie Chama cha Walimu kuanzisha *microfinance* kusudi Walimu wakopeshane wao kwa wao kwa riba ndogo. Tatizo la Walimu ni mishahara midogo. Tatizo la Walimu ni riba kubwa wanazopigwa na haya makampuni ambayo hayastahili hata kusemwa mdomoni mwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye miundombinu. Nimesema nimekuja kuomba na Mheshimiwa Waziri Mkuu unajua. Naomba unitengenezee daraja la Kishara liishe. Daraja la Kishara wakulima wa kwangu ndiko wanakopita kwenda visiwani, ndiko wanakoboresha uchumi wao, wananchi wataweza kusembura na kulima sehemu zinazowezekana, lakini kwenye sehemu za matingatinga tunahitaji mkono wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo langu wamefanya kazi kweli, wamechimba barabara, Rwangani wanachimba barabara, Buyanja wanachimba barabara, sehemu za Rugenge wanachimba barabara, lakini sehemu za madaraja na nimeomba daraja moja tu la Kishara, litengenezwe, roho yangu iridhike.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mara tano. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura na baadaye atafuata Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A.M LISSU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba mara moja niseme kwamba, nataka nichangie jambo la kwanza masuala ya elimu ya sekondari. Jambo la pili, nitachangia sehemu inayohusu ulinzi na usalama hapa nchini na jambo la tatu, kama kutakuwa na muda, nitazungumzia masuala ya mchakato wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulileteawa kitabu cha takwimu muhimu za elimu kwa Tanzania. Kinaitwa *basic education statistics in Tanzania (BEST)* kuanzia mwaka 2007 – 2011. Takwimu hizi ziliandaliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mujibu wa takwimu hizi mambo yanayoonekana ya kimsingi kabisa ni kwamba, elimu ya sekondari katika nchi yetu imekuwa ikiporomoka kwa kiasi kikubwa kuanzia mwaka 2006, Serikali ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani. Takwimu hizi zinaonesha kwamba, katika miaka mitano ya mwisho ya Serikali ya Awamu ya Tatu ya Rais Mkapa, ufaulu wa wanafunzi ulikuwa unapanda. Ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne umeanza kushuka kuanzia mwaka 2006 mpaka hapa tulipofikia leo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu hizi waliopata daraja la kwanza kwa wastani kati

ya mwaka 2000 mpaka 2005 walikuwa asilimia 5.4 ya wanafunzi wote; waliopata daraja la pili katika kipindi hicho hicho walikuwa asilimi 7.0, waliopata daraja la tatu katika kipindi hicho walikuwa asilimia 21 na waliopata daraja la nne walikuwa ni asilimia 52.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo kusema kwamba kwa wastani wa kufaulu katika miaka mitano ya utawala wa Rais Mkapa wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha asilimia 84.5. Waliofeli katika kipindi hicho kwa wastani walikuwa ni asilimia 14.8, waliopata daraja la sifuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya Rais Kikwete kuingia madarakani daraja la kwanza mwaka 2006 walishuka kutoka asilimia 5.4 ya wakati wa Mkapa mpaka mpaka asilimia 3.3, waliopata daraja la pili walishuka kutoka asilimi 7.0 mpaka asilimia 5.8, waliopata daraja la tatu walishuka kutoka asilimia 21 mpaka asilimia 16.3, waliopata daraja la nne katika kipindi hicho walishuka kutoka asilimia 52 mpaka asilimia 51.7 na waliopata daraja la sifuri waliongezeka kutoka asilimia 14.8 mpaka kufikia asilimia 22.8, hii ni kwa takwimu za mpaka mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, wastani wa kufaulu katika miaka mitano ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne ulikuwa ni asilimia 77.2 kutoka asilimia 85.4 za wakati wa Rais Mkapa.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia kwa kila mwaka, takwimu hizi zinaonesha vitu vya ajabu. Wanafunzi waliopata daraja la kwanza mwaka 2006 ambao ni mwaka wa kwanza wa utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne walikuwa ni asilimia 4.9 kama sikosei, *by* mwaka 2010 walikuwa wamefikia asilimia 2.8, kutoka asilimia 4.9 mpaka asilimia 2.8! Miaka yote ya utawala wa Rais Mkapa wanafunzi waliokuwa wanapata daraja la kwanza, la pili, la tatu na la nne walikuwa wanaongezeka. Katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne idadi ya waliofaulu imekuwa inakwenda chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni sahihi kusema kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne ni janga la elimu la Taifa la Tanzania. Ni

sahihi kusema kwa, takwimu hizi, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni janga la elimu kwa Tanzania na hizi takwimu ni za Serikali yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Waziri Mkuu ameunda Tume baada ya matokeo ya mwaka jana kuchunguza kwa nini wanafunzi wamefeli. Mwaka 2010, baada ya wanafunzi kufeli kufikia asilimia 50 Serikali iliunda Tume kuchunguza kwa nini watoto wa kidato cha nne walikuwa wanafeli.

Mheshimiwa Spika, ripoti yenyewe hii hapa, inaitwa taarifa ya utafiti kuhusu kushuka kwa kiwango cha kufaulu mtihani wa Taifa wa kidato cha nne mwaka 2010. Taarifa imeandaliwa na Wizara ya Elimu, taarifa hii imeandaliwa na Maafisa Waandamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Waziri wa Elimu anafahamu na Waziri Mkuu anafahamu. Taarifa hii haijawahi kutolewa hadharani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa jana kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba, huu si wakati wa kulaumiana na kutafuta mchawi. Nakubaliana naye, huu si wakati wa kulaumiana na kutafuta mchawi, huu ni wakati wa kuwajibishana. Huu ni wakati wa walioshindwa kazi kuwajibishwa. Waziri wa Elimu ameshindwa kazi, amekataa kujiuzulu anatakiwa afukuzwe kazi. Ni janga la elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu ameshindwa kazi anatakiwa ajizulu, kama hajiuzulu apigiwe kura na Bunge hili ya kutokuwa na imani. Wakati huu kinachotakiwa ni watu kuwajibika kwa kushindwa kazi, si wakati wa kulea uovu na uchafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie masuala ya ulinzi na usalama. Ripoti iliyoandikwa kwenye gazeti la *The African* la siku ya Jumatatu ya wiki hii inasema, Jeshi la Polisi la nchi hii linaongoza kwa uonevu, kwa kutunga kesi za uongo, kwa kushtaki watu kwa makosa makubwa ya uongo ambayo kisheria hayana dhamana; makosa ya

mauaji, makosa ya wizi wa kutumia nguvu, makosa ya ugaidi. Ripoti inasema Jeshi la Polisi linahitaji kusafishwa, limekuwa ni jeshi la kihalifu. Ni ripoti ya *The African*.

Mheshimiwa Spika, hii ripoti inakwenda sambamba na ripoti nyingi ambazo zimeandikwa juu ya *criminality* ndani ya Jeshi la Polisi. Umekuwa ni utamaduni wa kihalifu. Jeshi hili linatungia watu vitu vya ajabu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna watu kwa kushirikiana na Polisi, wanapigiana simu, wanalipana fedha, halafu wanakuja wanafungua kesi za ugaidi. Kuna mtu amewasiliana na hawa wanaoitwa magaidi kwa miezi miwili, amepigiana simu kuliko alivyompigia mke wake. Halafu leo anasema huyo aliyekuwa anapigiana naye simu ni gaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mtu amemlipa huyo anayeitwa gaidi fedha baada ya huyu mtu kufanya ugaidi, leo anasimama na kusema sisi ni magaidi. Sheria ya ugaidi inasema, anayelipa fedha kwa magaidi ni gaidi anatakiwa akamatwe na afungwe. Anayeshirikiana na magaidi, anayewasiliana nao...

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu ndiyo nilivyosema kwamba tumalize.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa!

**SPIKA:** Jamani tuelewane kwa utaratibu. Nimesema jana kulisemwa, leo kumesemwa, tukasema tuishie hapo, lakini kama mnataka semeni na ila mjue na wengine watasema. Endelea Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Natumai muda wangu umelindwa wakati nimekaa.

**SPIKA:** Umelindwa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, siku ambayo mkutano wa kigaidi unafanyika, Mheshimiwa humu

ndani amezungumza na mmoja wa hao magaidi, wiki mbili baadaye akamlipa fedha, huyu ni gaidi anatakiwa akamatwe. Habari ya ugaidi ni mambo ya kutunga ya Jeshi la Polisi na baadhi ya watu walioko humu ndani. Kama wanafikiri hakuna ushahidi watashangaa. (*Makofi*)

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ninatumia Kanuni ya 64: "Kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli". Sasa namwomba hayo anayoyasema kwamba kuna watu wamelipwa humu ndani, baada ya muda wamepigiana simu. Kwa sababu fedha amezitamka na amesema kwa uhakika hebu atoe huo uthibitisho humu ndani ya Bunge. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza Kamati ya Kanuni itabidi tukutane, kwa sababu tumekubaliana wenyewe kwamba tufike mahali tuwe tunashauriana. Hizo kesi zote mnazozungumza zipo Mahakamani. Sasa ninachokisema, naomba msikilize, tatizo lenu ni kulalamika, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani akiwa kiongozi mkubwa sana, sikutaka kuingilia hotuba yake na wengine wote walinyamaza. Katika dunia *everybody has got the right to reply*.

Sasa tunachokisema, hii ndiyo anayosema mama Anna Abdalla, mengine yapo Mahakamani kwa nini hatupendi kuheshimu mambo ya Mahakamani. Nimesema tuishie hapo, tuzungumze yetu. Sasa mkitimua hapa kuna ripoti nzima hapa, mta-*defend* nini na mimi nilimpa heshima Mheshimiwa, nilimpa heshima kwa sababu ni kiongozi wenu. Kwa hiyo, naomba tuheshimiana, tuanze kuzungumza vitu ambavyo vipo katika mazungumzo yetu. Mheshimiwa Tundu Lissu naomba uendelee.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba muda wangu ulindwe. Hotuba ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatakiwa ijibiwe na Waziri Mkuu na siyo mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niendelee.

**SPIKA:** Endelea lakini tutunze heshima ya Mahakama.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, sijataja chochote kinachohusu Mahakama, nimesema mambo yanayofanywa na Polisi na marafiki zao na watu wengine waliomo humu ndani, hayo mambo hayako Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushahidi upo kama Mheshimiwa Anna Abdalla anautaka wa malipo yaliyofanywa tarehe 14 Januari, mwaka huu kwa mmoja wa magaidi. Mawasiliano yaliyofanyika tarehe 28 Desemba na mmoja wa magaidi na marafiki zake walioko humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze masuala ya Katiba. Mchakato wa kutengeneza Katiba mpya umetekwa nyara na unachafuliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba na Serikali. Mwenyekiti wetu na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alizungumza jana. Msimamo wetu ni kwamba, kwa vile Tume inachakachua utaratibu wa kupata Katiba Mpya, CHADEMA hatupo, siyo tu kwamba tutanyamaza, hatutanyamaza, tutatembea nchi nzima kuwaambia wananchi kwamba huu mchakato siyo wa Katiba Mpya, huu ni mchakato wa Katiba ya CCM.

Mheshimiwa Spika, tutawambia wananchi wetu kwamba, kwa sababu huu ni mchakato wa Katiba ya CCM ya mambo yale yale, ya watu wale wale na ya chama kile kile, kura ya maoni itakapofika hiyo Katiba ikataliwe na Watanzania. Hatuwezi tukakubali Tume ikatumia fedha za umma, ikaharibu utaratibu wa kupata Katiba, ukaingiza nchi hii kwenye machafuko.

Mheshimiwa Spika, uchakachuaji wa mfumo wakati wa utaratibu wa kupata Katiba mpya kwa umeiingiza Kenya kwenye maafa mwaka 2008, uchakachuaji wa utaratibu wa kupata Katiba Mpya umeiingiza Zimbabwe kwenye machafuko makubwa kwa miaka 15, mpaka juzi walipofanya

maridhiano kila mtu akakubali, wakatengeneza Katiba mpya ambayo kila mtu anaikubali. Utaratibu unaofanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba wa kuchakachua Katiba utaingiza nchi hii kwenye machafuko. Nilishasema kwenye Kamati nasema mbele ya Bunge Mungu atusaidie, lakini hatuwezi tukakubali Tume ikaharibu mchakato wa Katiba. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kengele ya pili, Mheshimiwa Tundu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Eeh!

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Kengele ya pili?

**SPIKA:** Tunaendelea Mheshimiwa Felister Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Salum Barwany ajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nimeshangaa msemaji aliyepita alivyotumia muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa aliyemaliza kuongea kwamba, ametambua kazi kubwa iliyofanywa na Chama cha Mapinduzi katika suala la elimu na watoto wake na yeye mwenyewe amesoma katika shule hizo ambazo zimejengwa na Chama cha Mapinduzi. Amesahau kwamba kipindi kilichopita, shule hazikuwa nyingi kama sasa hivi. Kwa hiyo, takwimu zake alizotoa naomba azirekebishe kwa sababu katika kipindi cha nyuma shule hazikuwa nyingi kama sasa hivi, kama kipindi cha mwaka 2005 na kipindi hiki. Naomba arekebishe takwimu zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mambo makubwa ambayo imefanya katika kipindi cha utawala wake. Tumejenga barabara nyingi na tumefanya mambo mengi, lakini kuna jambo moja tu limeshindikana katika Serikali hii, jambo hilo ni kuhamisha Serikali kuja katika Makao Makuu ya Chama cha

Mapinduzi au Makao Makuu ya nchi ambayo ni Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, tumekwishasubiri kwa muda mrefu na kila mwaka tunaliongelea hili kwamba, Serikali inatakiwa kuhamia Dodoma na kama hawataki basi hili suala la kusema kwamba ndiyo Makao Makuu lifike mwisho sasa.

Mheshimiwa Spika, *CDA* kwa mwaka huu wametengewa shilingi milioni 500, milioni 500 hawezi kufanya kazi yoyote. Wamepima viwanja hawana fedha za kulipa fidia kwa wananchi, viwanja vipo, wananchi hawawezi kugawiwa viwanja, Wabunge wanataka viwanja, wananchi wanataka viwanja kwa ajili ya kuendeleza Mji wa Dodoma, lakini *CDA* hawana fedha za kulipa fidia. Mwaka huu wamepewa shilingi milioni 500. Bajeti iliyopita mwaka jana waliambiwa kwamba watapima Mji Mkuu wa Serikali katikati ya Manispaa Dodoma na Wilaya ya Chamwino, hizo fedha hazijatoka mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, *CDA* hawawezi kupima Mji Mkuu wa Serikali kwa sababu hawana pesa. Naiomba Serikali izingatie hilo kwamba, ifikapo mwaka 2015 tuone juhudi ambazo zimefanywa na Serikali katika kuhamia Mkoa Dodoma au Mji wa Dodoma. Bado tunashuhudia majengo makubwa ya Serikali yakijengwa Dar es Salaam, bado tunashuhudia miundombinu mingi ikifanyika Dar es Salaam lakini Dodoma bado.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru tumejengewa barabara, barabara zimetengenezwa. Kwa hiyo, miundombinu ya barabara ipo safi kabisa, lakini bado Serikali haijafanya juhudi kubwa kwa ajili ya kuhamia Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulikwenda na Mheshimiwa Waziri katika maporomoko ya Ntomoko kule Kondoa na Waziri Mkuu akaahidi kutafuta fedha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya maporomoko ya Ntomoko.

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka leo ninavyoongea, hakuna kila kitu kinachoendelea katika maporomoko yale na tulimweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mporomoko yale yanahudumia maji vijiji 17. Lakini mpaka leo ninavyoongea hata kwenye bajeti ya Serikali hakuna fedha zilizotengewa kwa ajili ya miundombinu ya Ntomoko. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hii ilikuwa ahadi yake tangu mwaka jana hebu alifikirie na litimie sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumze suala la fedha za Miradi ya Maendeleo. Fedha za miradi ya maendeleo zinachelewa sana. Mwaka huu katika Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Bahi mpaka mwezi Machi, walipata asilimia 12 tu, Wilaya ya Kongwa walipata asilimia 15.3, Wilaya ya Kondoa walipata asilimia 11. Kwa hali hiyo, hatuwezi kufika mbali katika miradi yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tuna Hospitali ya Mkoa hapa ambayo inajenga wodi ya watoto na wodi ya wazazi, lakini miaka tano sasa wodi ile haijakamilika. Mwaka 2008 tulikuwa tunahitaji bilioni 1.5, mpaka sasa nadhani tunahitaji fedha nyingi kutokana na ule mradi kusimama. Serikali hebu iangalie hilo. Miradi ambayo imeshaanza ni bora ikakamilishwa kuliko kuanza miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, tuna jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, mpaka leo Mkuu wa Mkoa anakaa ofisi ya ajabu sana hapa Dodoma. Nadhani Wabunge hamjawahi kumtembelea, anakaa ofisi ya ajabu sana na hapa ndiyo Makao Makuu ya Serikali na Bunge linakutana hapa na kuna ugeni mwingi tu hapa, lakini Mkuu wa Mkoa wa Dodoma hana ofisi. Majengo ambayo hayajakamilika ya Serikali, Serikali ingeweka utaratibu wa kuyakamilisha ili *value for money* ionekane.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la ajira kwa kada za chini katika Halmashauri zetu, Watendaji wa Vijiji, Wahudumu, Madereva kwamba kada hizo zote lazima waajiriwe na Tume ya Utumishi. Siyo jambo la haki kabisa. Halmashauri nyingine hazina Wahudumu, hazina Watendaji wa Vijiji kwa sababu

lazima ajira itoke Dar es Salaam. Naomba suala hili litazamwe upya ili watendaji hawa wa kada za chini waajiriwe moja kwa moja na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka jana tulipanga fedha kwa ajili ya bwawa eneo la Farukwa na bwawa hili lingewahudumia wananchi Wilaya ya Chemba na wananchi wa Wilaya ya Bahi, mpaka leo hakuna kinachoendelea katika eneo lile. Wakulima wa Chemba na wakulima wa Bahi wanasubiri bwawa hili kwa hamu zaidi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji cha mpunga, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 tuliapa hapa Wabunge wote tukiwa sana na tukiwa na wadhifa sana, lakini kitu ambacho tunaona kama tumetengewa na Serikali yetu, ni kuhusu fedha za kuchochea maendeleo katika maeneo yetu, Wabunge wa Viti Maalum. Hatujaona mkakati wa dhati ambao Serikali inafanya kutusaidia Wabunge wa Viti Maalum katika hili. Naomba hili pia lifikiriwe na Serikali kuwakumbuka Wabunge wa Viti Maalum kwa nini katika hilo tunatengwa?

Mheshimiwa Spika, nizungumze sasa kuhusu *NIDA* Shirika la Vitambulisho la Taifa. Nawapongeza sana wafanyakazi wa *NIDA* kwa sababu ni miaka 50 sasa Watanzania hatuna vitambulisho. Lakini kwa mwaka huu *NIDA* wameweza kutoa vitambulisho kwa ajili ya Watanzania. Lakini tatizo walilonalo watu wa *NIDA* hawana fedha za kutosha. Bajeti iliyopita waliomba shilingi bilioni 150, lakini walipata bilioni 10 tu. Hawawezi kufanya jambo lolote mpaka 2015 kutoa vitambulisho kama tunavyodhani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kama kweli wanataka Watanzania wapate vitambulisho, kwa mwaka 2015 kila Mtanzania awe na kitambulisho cha Taifa wapewe fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya kazi ya kutoa vitambulisho kwa Watanzania, bila hivyo hawataweza kufikia malengo kama tunavyotarajia.

Mheshimiwa Spika, kuna asilimia 20 ya ruzuku ya fidia ya vyanzo vya mapato ambavyo vilifutwa na hii asilimia 20 inatoka Serikali kuu.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuamini mwaka wa fedha unakwisha Halmashauri hazijapokea hizo fedha na kama wamepokea, wamepokea asilimia ndogo sana, kwa hiyo, shughuli za maendeleo katika vijiji vyetu haziendi, zinasimama kwa sababu fedha hazileti kwa wakati muafaka na Wizara ya Fedha. Naiomba Serikali yetu kwamba, ifike wakati sasa fedha zifike kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tusichezee amani ya Tanzania. Wale viongozi wa dini, nawaomba sana Watanzania wenzangu...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitawaita Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Salum Barwany, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe, Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Vicent Nyerere.

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo!

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahh! Nimemwita Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**SPIKA:** Aaa, hayupo, haya endelea Mheshimiwa Barwany!

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ili niweze kujadili hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge langu la tatu la bajeti tangu tuingie kwenye Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya kwanza mara baada ya kuchaguliwa kwangu, nilizungumzia suala zima la mgawanyo wa rasilimali katika nchi. Nilitahadharisha nchi na nikatahadharisha Wabunge wenzangu kwamba, iwapo tutafanya mchezo, tukafanya masihara juu ya mgawanyo wa rasilimali katika Taifa letu, nchi yetu tutaiingiza katika janga kubwa na maafa makubwa ya mgogoro wa vita ya wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hii imetokea katika nchi nyingi duniani hata katika Bara letu la Afrika. Leo Sudan kuna mgogoro mkubwa na nchi nyingine katika Afrika kwa sababu ya mgawanyo mbovu wa rasilimali katika nchi na hili linanyemelea sasa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo mbaya wa rasilimali unapelekea wananchi katika maeneo mengi kulalamikia mgawanyo huu. Matokeo mabaya ya Mikoa ya Lindi na Mtwara juu ya suala nzima la gesi, ni matokeo ya mgogoro wa kutokugawana vizuri rasilimali. Kwa nini leo watu wa Kusini wanalalamika kwamba, ni katika maeneo ambayo yapo nyuma kimaendeleo, wananchi wa Kusini ni wazalishaji wakubwa wa korosho, lakini wakati huo huo wananchi wa Kusini tayari wamepata eneo ambalo gesi inatoka. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inajisifu sasa, umaskini wa Taifa letu unaondoka, lakini ilikuwa muhimu watu wa Kusini sasa, kujua maslahi yao ambayo yanatokana na gesi ambayo ipo katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukitaka kumuua paka wako, basi unamtafutia jina mbaya. Huu ni utaratibu wa watu wote ambao hawawatakii mema wenzao, mgogoro wa watu wa

Kusini ulikuwa ni Serikali kukaa na watu wa Kusini kutaka kujua nini wanachokihitaji katika maendeleo yao. Kwa muda mrefu kabisa, imefikia mahali leo, wanapotoshwa watu wa Kusini, wanapotoshwa Watanzania wakiambiwa kwamba watu wa Kusini hawataki gesi yao itoke kusini, si kweli. Wananchi wa Mikoa ya Kusini wanataka Serikali ilete sera kuonesha ni namna gani Watanzania watanufaika juu ya rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, gesi ni utajiri mkubwa na Mataifa mengi duniani yametajirika kupitia mafuta na gesi. Lakini katika Taifa letu tumedai mara nyingi katika Bunge hili, hebu tuleteni mikataba, leo mikataba inasainiwa na Makampuni mbalimbali ya Kimataifa juu ya uchimbaji wa gesi katika Mikoa Kusini, lakini wanasaini mikataba hiyo kwa sera gani, kwa mwongozo upi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni watu wachache wanakaa na kufanya maamuzi juu ya rasilimali za Watanzania, gesi ni utajiri mkubwa. Tunataka Serikali ilete sera Bungeni, sisi kama wawakilishi wa wananchi tuweze kueleza wananchi wetu kwamba, mpango wa Serikali ni huu. Leo sisi Wabunge wa Kusini ni mabubu, tunashindwa kuwaeleza wananchi wetu kwamba, mpango wa Serikali juu ya gesi ukoje, hakuna Mbunge ambaye anaweza kutwambia hapa mkakati wa Serikali juu ya utajiri huu uko wapi?

Mheshimiwa Spika, hili limeleta mkanganyiko na isifikiriwe kwamba, watu wa Kusini wamenyamaza leo hapana, bado watu wa Kusini msimamo wao upo pale pale, wanaitaka Serikali ieleze, Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika Awamu ya Nne ilisema, itaweka kinu cha kuchambua gesi Mtwara kwa megawati 300, umeme utapatikana Mtwara utapelekwa Dar es Salaam, siyo gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam. Leo tunaambiwa kwamba gesi inatoka Mtwara kupitia bomba kwenda Dar es Salaam, wananchi wa Lindi na Mtwara wanataka waelezwe.

Mheshimiwa Spika, miaka 20 iliyopita wananchi wa Kusini waliambiwa kwamba gesi ya Kilwa Songo Songo itapelekwa Dar es Salaam na gesi ya Mtwara Mnazi Bay

itanufaisha watu wa Kusini na kutakuwa na gridi ya Taifa, mpaka leo gesi ya Kusini inatoka, lakini gridi ya Taifa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara haipo. Huo ndiyo mgawanyo mbaya wa rasilimali katika nchi na ndiyo unaweza kuleta migogoro na watu wakaingia katika machafuko makubwa katika Taifa lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la stakabadhi ghalani. Huu ni mwezi wa sita tangu wakulima wa korosho wavune, lakini mpaka leo mkulima bado hajauza korosho zake, anataka awapeleke shuleni watoto wake, anataka kuandaa mashamba yake kwa kilimo kipya, lakini mpaka leo wananchi wetu wamekatishwa tamaa.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa hapa na viongozi wa Serikali tu, kwamba stakabadhi ghalani imewanufaisha wakulima, lakini wakulima wenyewe bado hawajasema kwamba, wamenufaishwa vipi na stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumzia soko la dunia la korosho limeanguka, lakini ni korosho gani, ni korosho ghafi. Lakini leo tuna Viwanda 12 vya Korosho katika Mikoa ya Kusini ambao ni mkopo katika mabenki ya dunia. Viwanda vile vyote wamechukua viongozi wa Chama cha Mapinduzi na ndio wanavimiliki viwanda vile leo. Ni mali yao, wanatumia kufanya maghala, baada ya kufanyia *process* korosho, tukauza korosho ambazo tayari zimetengenezwa, tukapata soko zuri katika soko la dunia, lakini mpaka leo tunauza korosho ghafi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunapozungumzia suala la korosho, wananchi wa kusini bado hawajaielewa Serikali za CCM wanavyoing'ang'ania stakabadhi ghalani hata kama bado haijawanufaisha wananchi wao katika zao hilo.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa katika miaka ya nyuma kwamba, msimu wa korosho unapofika, wananchi wote wananafsika na zao lile. Lakini leo msimu wa korosho unafika, huwezi kujua kwamba huu ni msimu wa korosho

katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kuna umaskini uliokithiri katika mikoa ile kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani. Tunaitaka Serikali itazame upya mfumo wa stakabadhi ghalani, unawanufaisha vipi wakulima wa Mikoa ya Kusini, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie habari ya Halmashauri yangu. Mwaka 2010 Manispaa ya Lindi imetangazwa kama ni Manispaa kutoka katika Halmashauri ya Mji wa Lindi. Lakini bado wananchi wa Lindi hawajaona umuhimu wa kuwa na Manispaa hiyo. Ruzuku inayotolewa na Serikali ni ile ile ya Halmashauri ya Mji na hii nimeizungumza mara nyingi hapa, ni shilingi bilioni nane, lakini tumeongezewa tena mzigo wa Kata tano kutoka Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kwamba maslahi ya Manispaa ni zaidi ya Mji. Lakini bado Serikali haijaonesha umuhimu wa Manispaa ya Lindi kwa kuongeza ruzuku ya maendeleo. Hili nimelizungumza sana, nimelipigia kelele, lakini Serikali imekuwa kiziwi na pofu juu ya hoja hii ya wananchi wa Lindi. Tumeongezewa shule, dispensari, barabara lakini bado ruzuku inayopatikana katika Manispaa ya Lindi ni ile ile iliyokuwa ikitolewa kwa Halmashauri ya Mji wa Lindi katika miaka 10 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Bandari ya Lindi na ndio kilio cha wananchi wa Lindi na ni ahadi ya Rais hiyo. Ahadi ya Rais ni kitu chenye kuheshimiwa. Mheshimiwa Rais ameahidi katika mambo ambayo atayashughulikia, ni kuhakikisha kwamba kutakuwa na Bandari ya Lindi, leo katika bajeti tunaambiwa kwamba kuna Bandari ya Bagamoyo. Hivi kuna haja gani katika nchi yetu kujenga Bandari nyingine. Tuna Bandari Mtwara haijakidhi vigezo vya matumizi ya Bandari na pia bandari ya Tanga ambayo nayo bado haijakidhi mahitaji ya bandari.

Mheshimiwa Spika, tuna bandari nyingi katika nchi yetu, kwa nini leo tutumie mabilioni ya fedha, tutumie mikopo ya Kimataifa, kujenga bandari wakati bandari zetu ambazo tunazo, bado hazijafikia kiwango cha mahitaji ya bandari

zile. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Hivyo tunaomba kwamba, ahadi za Mheshimiwa Rais ambazo huwa zinatolewa kwa wananchi, wananchi wanatoa kura zao kwa mujibu wa sera na Ilani unapochaguliwa kuwa kiongozi na hutekelezi ahadi yako, unatapeli kura za wananchi wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka wananchi wahakikishe kwamba kura zao zinakidhi haja ya Ilani ya Uchaguzi ya Vyama vya Siasa. Hivyo, mwaka 2010 Chama cha Mapinduzi kilipata ridhaa Lindi kuliko wagombea wote wa Urais, kwa mujibu wa mahitaji ya watu wa Lindi, waliahidiwa kwamba bandari yenu itajengwa na itafanya kazi, leo tumeshafika miaka saba, Bandari ya Lindi bado haijafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina zaidi ya hapa, lakini mgawanyo wa rasilimali ni muhimu katika Taifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Barwany. Sasa namwita Mheshimiwa Malocha na Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe atafuatia.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia juu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika hotuba yangu, naomba nianze na migogoro ya ardhi iliyopo nchini.

Mheshimiwa Spika, utakubaliana nami kwamba nchi hii sasa hivi kila kona ina migogoro ya ardhi na ni ukweli usiopingika, ukienda Kilosa migogoro ipo, Babati na maeneo mengine. Migogoro hii inatokana na Serikali kutochukua hatua za haraka za utatuzi, Serikali inachukua hatua wakati tayari uvunjifu wa amani umeshatokea kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Spika, nimeona nizungumzie hili kwa sababu hata kwenye eneo langu, Wilaya ya Sumbawanga kuna mgogoro mkubwa ambao sasa hivi unahatarisha amani kubwa sana. Umekosesha amani wananchi na hata mwekezaji mwenyewe amekosa amani. Mgogoro huo ni wa

muda mrefu, lakini Serikali haijatoa utatuzi na matokeo yake hivi sasa ni uvunjifu wa amani, watu kuuawa, mali ya mwekezaji kuharibiwa, wananchi kunyanyaswa, kukatwa masikio, kuchomwa moto na vyuma vyenye ncha kali, wananchi kuwa maskini, wananchi kutangatanga na kukosa mahali pa kulima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali ya Mkoa kufanya jitihada za kuunda Tume, kuangalia chanzo cha mgogoro huo na kubaini chanzo ni kwamba, vijiji vinavyozunguka shamba la Malonje vyenye mgogoro huo, vilipimiwa ardhi hiyo toka mwaka 1974 na mwekezaji amekuja kupewa nyuma. Kwa hiyo, mchonganishi mkubwa wa mgogoro huu ni Serikali yenyewe. Serikali inagonganisha kati ya wananchi na mwekezaji, matokeo yake wananchi na mwekezaji wanaumizana.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali ya Mkoa imeliona hilo na imeijulisha Serikali Kuu. Nashangaa kwa nini Serikali inachelea kuchukua maamuzi. Bunge lililopita nilimwona Waziri wa Ardhi nikamweleza, akasema mgogoro huu ameshamwandikia Waziri Mkuu, anasubiri utetezi. Sasa nashindwa kuelewa, kwa nini Serikali inachelewa wakati wananchi wanaumia, kuna muujiza gani juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kama kuna viongozi ambao walitumia nafasi zao kukiuka utaratibu, kumpa mwekezaji kinyume na utaratibu, kwa nini hatua zisichukuliwe na kwa nini Serikali isichukue hatua za makusudi kunusuru mgogoro huu. Matokeo yake kunatokea uvunjivu wa amani. Kwa hiyo, naishauri Serikali, katika mgogoro huu ichukue hatua za haraka ili kurejesha amani katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mgogoro huu na kwa sababu ya nchi yetu imeshaingiliana na mambo ya kisiasa, unakuta mtu mwingine anazusha, Mbunge umekwenda kusalimia, kuona wananchi, mtu mwingine anazusha kwamba, Mbunge amechochea, wakati wananchi wametoa malalamiko na wewe umewaambia utayafikisha Serikalini, wanasema Mbunge anachochea.

Naomba kabisa kukanusha utaratibu huu na Serikali ichukue hatua juu ya jambo hili na ikitaka kupata ukweli itume Tume iende ikaangalie, itaona mateso ambayo wananchi wanayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nimeona nizungumzie ni suala la kilimo. Kumekuwa na tatizo kubwa la ukosefu wa soko la zao la mpunga, soko lisiloeleweka. Nashangaa kwa nini Serikali inafikia hatua ya kuingiza mchele kutoka nje, wakati ndani ya nchi bado tunao mchele mwingi ambao hauna soko. Mchele unaoingizwa nchini, ni mchele ambao hauna hata ladha na wala hatujui umezalishwa kutumia kemikali za aina gani. Matokeo yake tunaacha mchele ambao umezalishwa na wakulima wetu, wenye ladha nzuri, tunaingiza mchele mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi wakati nakuja Bungeni nimepitia maeneo ya Sumbawanga, mchele umejaa, ukija pale Tunduma, mchele umejaa, ukija Mbeya, mchele umejaa, ukija Morogoro, mchele umejaa, hawana kwa kuuza na cha ajabu sasa hivi wameshaanza mavuno ya msimu huu, wananchi hawajui mpunga ule watauza wapi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itafute utaratibu wa kununua mpunga kama inavyofanya kwenye mahindi na kukusanya kutunza kwenye maghala, kama inatokea kuna maeneo yanakosa mchele, basi Serikali iweze kuwashawishi wafanyabiashara waweze kutawanya katika maeneo yale, kuliko kuingiza mchele nchini, wakati upo mchele mwingine mwingi ambao unazalishwa na wakulima na Serikali yenyewe inahimiza kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie, ni juu ya Serikali kuangalia namna ya kutoa posho angalau kwa kiwango kidogo kwa Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji. Lazima tukubaliane kuwa, dunia ya leo hakuna mtu anayefanya kazi ya kujitolea. Unakuta hata vifaa vyenyewe vya ujenzi vinashushwa mtu anadai hela, sembuse huyu kiongozi

ambaye amechaguliwa na wananchi, muda wote anatumikia umma kuanzia asubuhi hadi usiku na anakosa muda kabisa wa kufanya shughuli zake za kusaidia familia.

Mheshimiwa Spika, anahamasisha wananchi katika shughuli za maendeleo, anapokea viongozi, anasuluhisha migogoro, anashiriki katika misiba mbalimbali kama kiongozi ndani ya kijiji, lakini mtu huyu Serikali haijamwangalia. Naishauri Serikali, kama kweli tuna dhamira njema kwamba, binadamu wote ni sawa na tunataka Serikali yetu ifanye kazi kwa pamoja, naomba Serikali hata kwa kiasi kidogo iweze kuwaangalia viongozi hawa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la kushuka kwa kiwango cha elimu nchini. Katika kipengele hiki, naomba nizungumzie kwa suala la Wakaguzi wa shule za msingi na sekondari. Nimejionea mwenyewe kutoka kwenye Mkoa wangu wa Rukwa. Ukiangalia Wakaguzi waliopo pale mkoani wana upungufu mkubwa wa vyombo vya kufanyia kazi, hata ofisi wanayokaa ni kama wanafanya mkutano kila siku, hawana ofisi maalum. Wanakaa kwenye ofisi ambayo ukienda, utadhani ofisi ile inaendesha mikutano kila siku maana wanarundikana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Serikali ijaribu kutazama kada hii na iwasaidie maana hawana nyenzo za kufanyia kazi na maeneo mengine ambayo wamepewa magari, hawajapewa fedha za kuendesha vile vyombo. Kwa hiyo, unakuta magari yale yanatumiwa na Halmashauri, yeye hana mamlaka na madereva hawana.

Mheshimiwa Spika, ukiacha hilo, mtu anayemkagua mwenzake anapaswa athaminiwe na Serikali imwangalie katika suala zima la uwezeshi ili aweze kujiamini na anapokwenda kukagua awe anajiamini. Lakini usipomwezesha mtu huyu na anakwenda kumkagua mtu ambaye wakati mwingine anamzidi hata mshahara, unyonge ni mkubwa sana na hawezi kufanya kazi kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutowajali watu hawa wamekata tamaa, wengine wanatamani hata warudi madarasani wakafundishe, kwa sababu wanaona kuwa Mkaguzi tu kwa jina tu, cheo kikubwa, lakini maslahi hakuna, ni kama nafasi ya mateso. Kwa hiyo, naomba Serikali hii ijaribu kuwaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu vile vile chombo ambacho kingekuwa karibu na wao ni *TSD*. *TSD* iko Dar es Salaam sijui Temeke au Ilala. Ningeomba Serikali irudishe mfumo wa kuwa na *TSD* kwenye Wilaya mbalimbali ili chombo hiki kiweze kuwa karibu na Wakaguzi hawa na kiwe ni chombo vile vile cha kuwasaidia katika kutatua matatizo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni Bodi katika shule zetu za Sekondari. Naiomba sheria ibadilishwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia. Nasema hivi, msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Taarifa hii ya kiuchochezi, utafute utaratibu wa kutozikubali. Taarifa ya KUB (Kiongozi wa Upinzani Bungeni) ambaye mimi namwita ni Kiongozi wa Uchochezi Bungeni. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilishangaa Mheshimiwa Waziri Mkuu anapewa mambo mazito kwa kweli ya kumdhalilisha, lakini ukweli ni kwamba, mbona baada ya kutoka Bungeni hapo nje, anakwenda anasema Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba barabara pale kwangu Hai. Kwa ushahidi ambao Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ametembelea

Wilaya ya Hai, KUB alitamka wazi kwamba, mnyonge, mnyongeni haki yake mpeni, mbona hayo hajasema Bungeni hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2010, wenzetu walisema jamani tupeni Serikali na Watanzania nao wanajua, tupeni Serikali sisi, baada ya hapo, siku 100 Katiba iko mezani, sasa mchakato wa Katiba unaendelea, wanasema hawataki Katiba. Naiomba Serikali shupavu ya Chama cha Mapinduzi sasa ifanye kazi kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kwamba, wenzetu wanavyosema wanakwenda mitaani kuchochea Watanzania waandamane kwa sababu ya Katiba, hili suala si dogo, suala hili ni la kuchukulia hatua. Serikali ijipange kwa sababu kazi ya Serikali sio kuongoza, kazi ya Serikali ni kutawala, kwa hiyo, Serikali itawale.

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushe yaliyotajwa katika hotuba ya Waziri Mkuu katika hii sehemu ya *CDA*. *CDA* wamepangiwa shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya mishahara. Lakini kama hiyo mishahara mikubwa kiasi hicho hata matumizi mengineyo ingekuwepo lakini sifuri. Lakini hiyo imechukua karibu asilimia 50 ya mishahara ambayo iko katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kama ni kosa la uchapishaji ijulikane, lakini kama ni hela zimechomekwa pale Serikali ilifanyie kazi suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la Makao Makuu kuhamia Dodoma. Hivi kweli kuna utashi wa kuhamia Dodoma? Sisi enzi yetu tukiwa wadogo, magazeti yalikuwa machache sana nchini, kulikuwa na gazeti moja linaitwa Taifa. Mzee wetu marehemu Mwenyezi Mungu amrehemu, Mzee Kawawa alionesha ishara ya Serikali kuhamia Dodoma akipanda treni. Sasa kama ishara hiyo ya kuhamia Dodoma mpaka leo hii mwaka wa 36, Serikali haihamii Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli kuna utashi wa Serikali? Mbona tunaona majengo mengi mapya ya Wizara

mbalimbali yanajengwa Dar es Salaam ndani ya kipindi hiki, ikiwemo Wizara kwa mfano, ya Maliasili, Utumishi, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara zingine, majengo mapya, maghorofa makubwa, hayo kwa nini hayakujengwa Dodoma? Suala hili si la kufanyia utani, kuwe na utashi kabisa dhahiri kama ilivyokuwa Chuo Kikuu cha Dodoma. Utashi ulivyokuja mbona kimejengwa chuo kikubwa kuliko vyuo vingine vyote katika Afrika Mashariki na Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Malawi na Nigeria walikuja kusoma mfumo wa *CDA*. Lagos kuhamia Abuja imewachukua miaka 10 mpaka 15 na leo wako pale. Sasa inakuwaje wale wamekuja, ni wanafunzi wetu, halafu wamepiga hatua kuliko sisi. Kwa hiyo, suala hili naomba bajeti inayokuja mwakani panapo majaliwa, tusiunge mkono kama hakuna maelezo dhahiri ya Serikali kuhusu kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Waziri wa TAMISEMI, ukurasa wa 30, kuna suala limezungumziwa la ulinzi shirikishi wa misitu na maeneo oevu. Ukiangalia Mto Mara unazidi kwisha kwa sababu ya hali halisi ya ulinzi na ushirikishi wa jamii ni mdogo. Ukijaribu kuangalia Sheria namba 5 ya Vijiji ya mwaka 1999 haiwezi kusaidia vijiji hivi ilinde hifadhi ya ule msitu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, Serikali ichukue msitu ule uwe chini ya Serikali, chini ya Maliasili. Kwa sababu katika msitu ule kuna miti mizuri, kuna miti haipatikani sehemu zingine, wako viboko, kuna mamba katika mto ule. Sasa kwa nini maliasili isichukue eneo lile kwa ajili ya kuimarisha suala la ulinzi. Suala ambalo bajeti imetengwa shilingi bilioni 4.3 katika bajeti ya mwaka huu, inashangaza kwamba hadi sasa ni shilingi 671,000,000 zimekwenda. Je, katika mazingira haya je tutaweza kulinda mito hii na maeneo oevu?

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala zima la maslahi ya Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji. Mwenyekiti wewe huwezi kwenda kufanya kazi ya kijamii wakati unaacha utapiamlo unaota nyumbani kwako. Haiwezekani Diwani, mshahara

kidogo kwa maana ya posho na Wenyeviti wa Vijiji ambao hawana chochote, wasimamie shughuli za maendeleo ukitilia maanani kwamba Diwani kwa mfano, ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata, hawezi akasimamia haya maendeleo wakati yeye mwenyewe anaishi kwa kuombaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu suala la Jeshi la Kujenga Taifa. Nashauri kwanza muda ambao umepangwa, kwa hawa wenzetu Waheshimiwa Wabunge waliokwenda, wengine watu wazima kama mimi, ndugu yetu Mheshimiwa Yahya akiwa ni mfano. Hili nililichangia katika bajeti ya Ulinzi mwaka jana, tubadilike tusifanye mambo kwa mazoea, Serikali ilitazame upya suala hili, tunapata watu wengi kutoka nchi za nje, wanakuja kujitolea Tanzania. Kipindi hiki cha mwaka mmoja, hatutarajii kuna vita ambayo tunahitaji kupeleka Watanzania wote kupigana vita.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri mwaka mmoja ule wa kujitolea wengi wanataaluma mbalimbali, hatuna sababu ya kulia kilio cha Walimu wakati tunaweza kuwapeleka JKT kwa njia ya kujitolea, waende katika mashule mbalimbali nchini, wako wataalam wa afya, wa kilimo, waende vijijini wakafanye kazi kwa njia ya kujitolea ikiwa ni sehemu ya JKT. Kwa sababu hata tukiangalia matrekta ambayo tuliambiwa yamepelekwa katika kambi tano katika nchi hii hatujapewa utaratibu kwamba yamewezaje kuzalisha katika maeneo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, suala zima la makusanyo, ni kilio kikubwa kwa nchi nzima katika Halmashauri zetu, Tawala za Mikoa na maeneo mengine ya Serikali Kuu. Suala hili litazamwe upya ili tuache na kuombaomba katika bajeti hasa ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia taarifa iliyotolewa na Waziri Mkuu, ni asilimia 32 ya makadirio ambayo yameshapelekwa katika maeneo yote nchi nzima. Pia kuna

Sheria Ndogo ambapo inaonekana kuna ucheleweshaji wa Serikali kujibu Halmashauri, ndio majibu ambayo tumekutana nayo katika Kamati ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala linguine, ni ule uwezo wa kutambua vyanzo na kusimamia, yako maeneo mengine kuna udhaifu mkubwa kabisa wa usimamizi wa masuala ya makusanyo. Mara nyingine unakuta mtumishi ni wa ngazi ya chini ni mkusanya ushuru lakini ana hekalu, jumba, ana magari kwa sababu hela zile zinakwenda mfukoni na ushahidi upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kulipa vyanzo vya maeneo yale ambayo ilionekana ni kodi za kero. Serikali ikaanzisha utaratibu wanaouita *General Purpose Grant* (GPG). Haiwezekani imekuwa ni kiwango hicho tangu utaratibu huu umeanza mpaka leo hii. Haiendani na hali halisi ya mahitaji na ukiangalia eneo lile lilikuwa limekadiriwa tu, hapakuwa na *scientific data* ambazo zilikuwa zimechambuliwa. Mahitaji yanatofautiana katika Wilaya mbalimbali na hata kama ni Wilaya moja hiyo, haiwezekani mahitaji ya wakati huo ndiyo mpaka leo hii uwe unapewa kiwango hicho hicho cha fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu inasikitisha na kwa kweli ni fedheha kubwa sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa wanaofuata ni Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Vincent Nyerere.

Ngoja nifafanue; uongozi wa CHADEMA wamekubaliana na Wabunge wao kwamba, watagawana dakika katika kuchangia katika Wizara mbalimbali. Kwa hiyo,

hapa nitampa Mheshimiwa Paulina Gekul dakika tano na Mheshimiwa Vicent Nyerere nitampa dakika tano. Kwa hiyo, kengele ya kwanza itagonga baada ya dakika tatu na nyingine baada ya dakika mbili.

Baadaye atafuata Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nitajitahidi ili nitumie dakika hizi tano. Kuna usemi wa Kiswahili unasema kwamba, ukiona unaoga bafuni halafu kichaa akapita akachukua nguo zako usikimbizane nae. Naomba niende moja kwa moja kwenye masuala ya msingi ya wananchi nisikimbizane na wale wanaotukana, wananchi watapima wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, bajeti nzima ya matumizi ni shilingi trilioni 4.2/-, lakini Bajeti ya Maendeleo ni shilingi bilioni 639/-. Ukiangalia fedha za ndani tulizotenga ni shilingi bilioni 270/- tu kati ya shilingi trilioni 4.2/- tunazokwenda kuzitumia, *this is shame*. Ninasema hivi kwa sababu huko chini, wazazi wetu, ndugu zetu akinamama wanaolala hospitalini, wanakwenda kujifungua wanalala chini lakini Wabunge tunapitisha hela za kula, za mafuta, za *per diem* shilingi trilioni 4.2/-, bilioni 270/- fedha za maendeleo. Lakini za nje bilioni 369/- na jumla ya fedha ni bilioni 639/- hizi za wafadhili hazitolewi. Naomba Serikali ibadilishe mtazamo wa kibajeti. Hii haikubaliki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mzuri ku-*justify* haya; ukarabati wa jengo hili tumejitengea shilingi bilioni sita, ukarabati tu wa hapa panapovuja. Bilioni sita tumejitengea kukarabati jengo la Bunge, lakini ukiangalia Hospitali za Rufaa na za Mikoa zilizojengwa sasa hivi tulitembelea Hospitali ya Singida, hata ya Mkoa wangu wa Manyara wanaomba bilioni mbili hawazipati. Sisi kukarabati tu jengo la Bunge panapovuja bilioni sita inawezekana wapi? Nafikiri hizi fedha za ukarabati zibakishwe milioni 500/- zingine tupeleke huko Mikoani kwenye elimu na afya ziende zikafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nina dakika tano, sasa nizungumzie Mabaraza ya Katiba. Kwa kweli huu utaratibu kwa kweli ni utaratibu mbovu sana uliofanyika katika *Ward C*. *Imagine* watu hawajajieleza, Wenyeviti wamekaa na Madiwani wao, wanajuaje wajumbe wanne wa Mtaa wa Oysterbay kama yeye ni wa Mtaa wa Ngarenaro. Wanakwenda pale hawajielezi, mwongozo unasema kwamba watachaguliwa kwa wao kujieleza, lakini kwenye *Ward C* kilichofanyika hawakujieleza.

Mheshimiwa Spika, watu wanasema hapa watashangaa kama wananchi wataandamana, sio wanachama wa CHADEMA watakaokwenda kuandamana. Kinachosikitisha hata kwenye mitaa inayoongozwa na Wenyeviti wa CHADEMA, viongozi wa CCM wale wanaokaa kwenye mitaa ile inayoongozwa na CHADEMA walikatwa majina yao kwa kisingizio kwamba wanatoka kwenye mitaa ya CHADEMA.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano katika Mkoa wangu wa Manyara. Babati pale Mtaa wa Sawe, viongozi wa CCM, wao ambao walikuwa wanafikiri kuwa wanakipigania hicho chama wamekiona hiki chama hakifai, kwa sababu hata wao viongozi wanaokaa kwenye mitaa inayoongozwa na CHADEMA, majina yao yanakatwa.

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu umevurugwa vya kutosha. Hebu sikilizeni kilio cha Watanzania na kweli kama hamtabadilisha watakaoandamana si wanachama wa CHADEMA. Wataandamana Watanzania ambao wanaona utaratibu huu wa kikatiba umekwenda kuchukuliwa na Chama cha Mapinduzi na wanataka kuufanya uwe wa kwao.

Mheshimiwa Spika, muda hauniruhusu, naomba nizungumzie suala zima linalowakabili wananchi wangu wa Mkoa wa Manyara. Mheshimiwa Waziri kipindi hiki alitoa mahindi kwa ajili ya kupunguza makali ya njaa. Katika Wilaya yangu ya Babati, katika Jimbo la Babati Mjini, mahindi hayakwenda.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha, Mkuu wa Wilaya anakataza akinamama wanaotegemea uvuvi wa samaki kuendesha maisha yao na kusomesha watoto wao, kuvua Maziwa yote ya Mkoa wa Manyara; Ziwa Burunge, Ziwa Babati mpaka kule Basutu, Maziwa yamefungwa, mahindi ya njaa hayajapelekwa. Kama sio kukomoa Watanzania wa Mkoa wa Manyara ni nini? Nafikiri kama hamkupeleka mahindi mkafungue yale Maziwa, wale wananchi wakavue wavue samaki wasomeshe watoto wao, wale akinamama tuwanusuru waweze kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. VINCENT J. NYERERE**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimekuwa na tatizo ukurasa wa 26 na 27 aya ya 37. Tumetenga shilingi bilioni 440/- kwa ajili ya kunusuru kaya maskini zilizo katika mazingira hatarishi. Mpango huu unalenga kuwezesha kaya maskini kupata chakula, kuziongezea kipato kwa kuzipatia fedha ili kumudu mahitaji ya msingi kama vile lishe bora, huduma za afya na elimu. Mpango huu unatekelezwa kwa awamu katika Halmashauri zote Tanzania bara na Zanzibar na umeanza na utambuzi wa kaya maskini katika vijiji 20 vya Halmashauri ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizopo, Wilaya maskini kabisa nchini, ni Wilaya ya Bunda. Lakini inanipa wasiwasi kuona katika utekelezaji tunataka kuanza na Wilaya ya Bagamoyo. Huu ni mgawanyiko ambao siukubali. Hapa tunaanza kutengeneza ukabila. Nadhani hizi bilioni 440/-, tungeziacha kwanza tukafanya tathmini ya Wilaya zote, tukaenda kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kufanya Wilaya nyingine ziwe mwanzo, halafu na nyingine ziwe mwisho, matatizo hayawezi kusubiri. Wilaya ambazo zitasubiri kupewa fedha hizi sidhani kama wataridhika. Nadhani, yawezekana nia ni nzuri, lakini utaratibu ni mbaya. Ninyi wenyewe ni mashahidi, mmeangalia kilichotokea kule Mtwara baada ya propaganda ya kwamba gesi inakwenda Bagamoyo, nini kilitokea.

Mheshimiwa Spika, nadhani yawezekana nia ni nzuri sana, lakini mpango huu sidhani kama ni mzuri sana, tuangalie ni namna gani ya kupeleka fedha hizi kwenye Wilaya zote kwa pamoja kuliko kuanza na Wilaya ya Bagamoyo. Tafsiri yake itakuwa kwamba ni kwa sababu Rais anatoka Bagamoyo, ndiyo maana fedha hizi wamepeleka mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuko katika kipindi cha Bajeti, kipindi ambacho Wabunge wapo hapa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wao. Yawezekana lugha ikawa mbaya au ngumu, lakini ijulikane Serikali ni chombo cha mabavu, ndiyo kawaida na Mbunge alivyokuja hapa wananchi wake walimwambia katutetee, kuwatetea ina maana kuwanusuru na chombo cha mabavu. Nadhani Wabunge wenzangu, tungejitahidi sana kujikita kuangalia namna gani Serikali itapunguza mabavu kuwasaidia wanachi kuliko kutupiana maneno yasiyofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani Wabunge waliopo hapa, ni muda wao wa kutathmini maisha ya watu wao huko waliko na wananchi wanasubiri kuangalia aidha, katika kipindi hiki cha bajeti, maisha yanakuwa magumu, yanakuwa rahisi au yanakuwa vile vile yalivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda sana niwaase Wabunge wenzangu, tuangalie ni namna gani ya kuwasaidia wananchi wetu kwa sababu wana tabu. Hii tabia ya kusema, kuna wananchi wanaishi katika mazingira hatarishi wengine; ni uongo. Watanzania wote wanaishi kwenye mazingira hatarishi. Kama kuna utekelezaji, naomba sana uanze kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Serukamba na Mheshimiwa Vita Kawawa ajiandae. Halafu Mheshimiwa Dkt. Mrema pia ajiandae.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA**: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, lakini nina maeneo machache ambayo ningependa kuchangia. Kwanza ni hili la mfumko wa bei. Mfumko wa bei umekwenda chini, ni jambo jema, lakini nilikuwa najiuliza, hivi mfumko wa bei wa Kalinzi na wa Dar es Salaam ni sawa? Mfumko wa bei wa Morogoro na Nkasi ni sawa? Mfuko wa bei wa Sikonge na Dodoma ni sawa? Mfumko wa bei wa Mkigo na Mwanza ni sawa? Mfumko wa bei wa Mlele Katavi ni sawa na wa Kinondoni? Mfumko wa bei wa Masasi na Arusha ni sawa, Ilala na Ngara ni sawa?

Mheshimiwa Spika, haya ni maswali ambayo wachumi lazima watujibu. Kwa hapa ninachokiona, tunaendesha chumi mbili kama nchi. Ili tuweze kuzi-*merge* chumi hizi, lazima suala la miundombinu liwe la kipaumbele ya hali ya juu na hasa miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Spika, njia pekee ya kuweza kusafirisha mizigo kwa bei rahisi ni kupitia reli wala sio kitu kingine na nchi zote wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la reli na bandari ndiyo kitu pekee ambacho kitatusaidia kwanza katika biashara ya *transit trade*, kupunguza mfumko wa bei, kupunguza ugumu wa maisha na usafiri kuwa wa bei nafuu. Lakini kwenye reli tunafanya nini? Ukienda kwenye bajeti yetu pamoja na kwamba ni tumesema uchukuzi kwa maana ya reli ni kipaumbele, lakini si kwenye fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini tulifanya *feasibility study* ya kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka – Isaka mpaka Keza kwenda mpaka Rwanda na kwenda Msongati. *Feasibility study* hii imekwisha mwezi Desemba, 2009. Leo ni Aprili, 2013, bado hatuna *project* yoyote kubwa ya reli. Tunachofanya ni yaleyale ya kawaida. Nadhani wakati umefika, reli hii tuliyonayo ilijengwa miaka mia moja iliyopita. umefika wakati sasa niiombe Serikali, tufumbe macho, tuhakikishe tunajenga na sisi reli itakayoishi miaka mingine mia moja.?

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo, ukijenga reli ya *standard gauge,* kitakachotokea ni nini? Hata gharama ya kusafirisha kwa tani inapungua kuliko reli ya leo. Reli ya leo ni karibu dola nane lakini ukiweka *standard gauge* itakuwa *1.5 dollar.* Hizi ni *economics* tu. Kwa hiyo, ningeomba wenzetu, miaka minne tumemaliza *feasibility study,* bado hatujajenga reli. Tukipata fedha leo maana yake ni nini, itabidi tu-*update feasibility* maana yake ni 2015 imefika. Kwa hiyo, niwaombe watu wa Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili tulifanye haraka.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Wakenya, leo tunavyoongea wameanza kujenga *standard gauge* kutoka bandari ya Mombasa wanakuja Nairobi wanakwenda Uganda, wakifika Uganda watakwenda Rwanda. Tunachohangaikia hatuwezi kukipata, mwisho wa siku hapa tunakimbizana tupate mizigo. 2015 wale watu wa Burundi watakuwa na tani karibu milioni tatu za *nickel*, tunazifikishaje bandarini?

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala la bandari toka mwaka 2008 tumesema tutajenga gati ya 13 na 14 mpaka leo tunaongea. Wakati tulivyokwenda China kutafuta mkopo tulikwenda na Wakenya, wenzetu wamemaliza kujenga. Sasa kama hatufanyi maamuzi huu urasimu hauwezi kutupeleka popote. Mipango yetu ni mizuri sana, lakini anatekeleza nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuongelea suala lingine la *vision 2025.* Nataka Waziri Mkuu aniambie *vision 2025* na *five years plan* tumefika wapi? Kama ingekuwa ni safari ya Dar es Salaam kuja Dodoma sasa tumefika Morogoro, Chalinze au wapi? Akisema tulipofika na wote tukubali kweli tumefika hapo na vigezo vipo. Tuulizane *GDP gross per USD* ni ngapi? *GDP per capita income as per USD,* tumefika wapi? *Exports* zetu tumefika? *Still consumption* kwa ajili ya viwanda, tumefika wapi? Power *consumption,* tumefika wapi? *Human development industries,* tumefika wapi? Maana haiwezekani kila siku tunaimba, tuna *five years plan,* tuna *vision* 2025 miaka inakwenda, lakini basi tupeane na *evaluation* tumefika wapi

ili tuweze kujua hapa tumerudi nyuma twende kwa kasi zaidi. Tusipofanya hivyo, tutafika miaka hiyo bado hatujafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la udini. Nimesikia rafiki zangu wa upinzani wanasema udini umeletwa na CCM, hapana. Suala la udini, viongozi tusiogope kuchukua *responsibility*. Hili ni suala la sisi viongozi wote *regardless of our parties*, lazima tulisimamie, tulinde nchi yetu. Nchi hii tumeirithi ikiwa na amani, haiwezekani leo tumeanza kufika tunachaguana kwa kuangalia dini zetu, hili ni la hatari. Hii nchi tunaihitaji wote, tukianza kutupiana lawama, hatuwezi kuisaidia nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe, sisi viongozi tuchunge ndimi zetu, sisi viongozi tuwe wa kwanza kwenda kutafuta *solution* ya matatizo yetu. Leo tunataka kuuana kwa ajili ya kuchinja. Wakati Wakenya wanaongea mwaka kesho kumpa kila mtoto *laptop,* sisi tunahangaika na kuchinja. Kweli jamani hii ndiyo Tanzania tunayoitaka? Jamani tuseme hapana, tushirikiane viongozi wote kusema hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye *speech* yake anasema wameanza *Presidential Delivery Bureau*. Ni jambo jema sana. Lakini naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ukisikiliza na hizo *labs, very fascinating,* lakini je, tuko tayari kubadili *culture* yetu? Je, *culture* yetu ya urasimu tuko tayari ku-*deal* nayo? Je, tuko tayari kuanza kuaminiana? Nchi hii hatuaminiani. Viongozi wakifanya maamuzi tunawaita mafisadi, viongozi magazeti yakiandika tunaacha kufanya maamuzi. Tutatekelezaje haya? Hakuna mtu mwenye fedha zake anataka kuja kuwekeza Tanzania aingie kwenye urasimu, wakati akienda Rwanda leo anapokelewa, akienda Kenya anapokelewa, sisi hata kujibu barua ni miezi mitano, mwaka mmoja, hatuwezi kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema naomba niwe *devil advocate* kwamba jamani, kama kweli tunaleta jambo hili jema, lakini na *culture* yetu tuwe tayari kuibadilisha, tuwe tayari kufanya kazi kwa bidii, lakini pia tuwe tayari kuchukua maamuzi. Maamuzi nchi hii yanachelewa sana. Unaweza ukaandika barua leo Wizarani, ukajibiwa baada ya mwaka mmoja, ama usijibiwe kabisa. *What kind of a culture?*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana, Tunaanzisha vitu vizuri vingi, lakini tuwe tayari kubadilisha culture yetu ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kama muda utaniruhusu ni suala mabadiliko ya Katiba. Nimemsikiliza sana jana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, anasema Mabaraza ya Katiba yote yanakuwa ya watu wa CCM. Hivi nataka niulize wenye hati milki ya Katiba hii ni ambao sio wana-CCM? Hivi wana-CCM sisi hatuna nafasi ya kujadili mambo haya? Kwamba kwa sababu mimi ni CCM, nimeingia kwenye Baraza la Katiba na-*loose monopoly* ya Katiba? Lakini hawawezi kuepuka sisi ni wengi, tumewashinda. Sisi ni wengi kwa maana ya Madiwani, ya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, kwa Wabunge na sisi ndiyo wenye Serikali. Kwa hiyo kama mnaamua kwenye jambo hili, haya lazima myakubali, haya hayakwepeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kama tunasema kuna Mabaraza ya Katiba, lazima tutarajie...

**TAARIFA**

**SPIKA:** Jamani nimesema, muda utakwisha. Haya taarifa ya nini Mheshimiwa Tundu Lissu?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU**: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kama ilivyofanyiwa marekebisho, hakuna mahali popote ambapo Sheria hiyo imesema kwamba, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya

watakwenda kuchujwa na *Ward C*, hakuna mahali popote ambako imesema hivyo. Huo ni utaratibu wa Tume, utaratibu ambao tumesema haufai kwa sababu hauko kwenye Sheria.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Serukamba na muda wake mpeni.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naikataa hiyo taarifa. Narudia tenda, nimesema kama Taifa lazima tuanze kuaminiana. Tumeipa Tume *mandate,* inafanya kazi yake, hatuwezi kuja hapa Bungeni kuanza kui-*criticize* na nasema Serikali kama hawa watu wanasema wao wanajitoa kwenye mchakato, *let them go* na hii biashara tuiache. Tunayo Katiba ambayo ni nzuri, tuendelee kuongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali tusiingie kwenye huu mtego wa hawa watu watatutishia kwamba, tutakwenda kuwaambia wananchi wasiipigie kura Katiba *let them go*. Halafu tunaacha mchakato, Katiba ipo, Serikali inaendelea, tunaendelea kuongoza nchi. *What is a problem? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekaa hapa wakati tunapitisha Katiba tumekubaliana, wenzetu wakatoka nje, wakaenda kuomba Ikulu, tumewasikiliza, tumebadilisha, tumeya-*incorporate* yote haya mliyajua, leo mnataka nini? Tusiwavuruge Watanzania, hii nchi ni yetu wote, naomba sana viongozi tuwe makini, hii nchi ni yetu wote, *at the end of the day, we have nowhere to go as a country* hatuna pa kwenda. *This is the best country for us*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuiache Tume ifanye majukumu yake na kwa kweli ni aibu kwa Serikali na kwa Wabunge leo tunaanza ku-*question credibility* ya Tume ambayo ina Vyama vyote, hiki ni kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Wananchi wanasema tumefyatua matofali na kujenga mpaka ngazi ya *renter* lakini Halmashauri hazijafanya *finishing*. Hii ni kwa sababu fedha zinakuwa hazitoshi, makusanyo yanapotea hayasimamiwi vizuri. Kwa hiyo, natoa ushauri tu kwamba, makusanyo yanapofanyika, Viongozi wa ngazi ya Mkoa na Wilaya, wasimamie vizuri makusanyo ili yapatikane kwa uhalali; fedha nyingi sana zinapotea.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuliongelea ni la ulinzi na usalama. Kule katika Wilaya ya Kalambo kuna vituo vya mpakani. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa nane amezungumzia usalama mipakani. Katika Kata ya Katete, Wilaya ya Kalambo, kuna Kituo cha Kasesha, Mwimbi kuna Kituo cha Mosi na Kasanga pia kuna kituo; utakuta askari walioko kule hawana hata silaha na *immigration officers* hawana hata usafiri. Sasa unashangaa mahali kama pale Kasesha, ukiingia ng'ambo ya Zambia askari wana silaha, ukija upande wa Tanzania askari hawana hata rungu! Kwa hiyo, ina maana hata ujambazi ukifanyika upande wa pili wakikurupushwa wakifika Tanzania watapumzika tu maana wanajua hakuna lolote. Naiomba Serikali iwape wale vijana silaha, *otherwise,* maisha yao yapo hatarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata wageni haramu kwenye Mwambao wa Ziwa Tanganyika wanaingia kiholela, tena kule kumekuwa ndiyo njia ya kuingilia na kwenda Malawi mpaka Afrika Kusini, sasa hivi wanapitia Ziwa Tanganyika. Naomba usalama na ulinzi uimarishwe kwenye hivyo vituo vya mpakani, lakini pia uimarishwe kwenye Ziwa la Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, nikiongelea kuhusu afya, ni kwamba, zahanati na vituo vya afya vinajengwa, lakini watumishi waliopo kule ni wahudumu, hakuna watumishi ambao ni wataalam na tunajua kabisa shughuli za afya siyo za kubahatisha. Watumishi wa afya hawafanyi kazi na mafaili, wanafanya kazi na binadamu na kwa binadamu ukifanya kosa kidogo tu hata kama ni *aspirin* au *panadol,* ukikosea kidogo tu basi umeshaua. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iangalie tena hivi vituo, kwa Mpango wa MMAM vituo

vifurikishwe watumishi walio na utaalamu, lakini pia na dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, kwa leo sina mengi, muda huu nilioutumia unatosha na niliyochangia yanatosha. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema Mheshimiwa Eng. Mnyaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuanza utangulizi, jana Mheshimiwa Kayombo, alinukuu Dira ya Taifa 2020. Kwa umuhimu wa nukuu ile, napenda niirejee tena kwa haya ninayotaka kuyaongea leo.

Mheshimiwa Spika, amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao ni mazingira ya lazima kabisa ya msingi kwa maendeleo. Hiyo aliisema jana na ni vizuri iingie kwenye masikio ya Serikali, kwenye masikio yetu Wabunge na iingie kwenye masikio ya Wananchi. Dira hiyo hiyo ya Taifa iliendelea ikasema, kimsingi maendeleo ya Taifa hayana budi yamlenge binadamu, yatokane na ukuaji endelevu wa uchumi, yahusishwe na watu wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya nukuu hiyo niseme kwamba, kuna matatizo Loliondo, kuna matatizo Mtwara, kuna matatizo Kondoa katika Kata ya Kinyasi, kuna migogoro ya kidini, maendeleo yatakuwa ni shida, ikiwa hali iko hivi nchini na kwenye maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la ajabu ni kwamba, tunajifunza kitu cha ajabu sasa hivi kwamba, mgogoro wa Loliondo, Madiwani wa CCM wanakwenda Dar es Salaam kwenye vyombo vya habari tunawaangalia kwenye runinga, Waziri wa CCM anakwenda kwenye vyombo vya habari tunaangalia runinga. Hii njia ya kutatua migogoro kwa kwenda kwenye vyombo vya habari, sawa, Wananchi tumeshajua ndiyo njia sahihi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni kwamba, Katibu Mkuu wa CCM akaunda Kamati yake iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, nayo kutafuta suluhu ya mgogoro huu, *fine,* lakini tuelewe kwamba, hizi suluhu za migogoro ya Wananchi, kuna Wananchi wa kila chama, lakini uzoefu unaonesha kwamba, kuna Kamati ya SMT na SMZ ambayo kwa muda wa miaka 48 inatatua migogoro ya Muungano haijamalizika. (*Makofi*)

Ukurasa wa 14 wa Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza wamekutana tena hivi karibuni, akaeleza mambo mengi lakini hatukujua mpaka leo yaliyotatuliwa ni yapi na yapi. Je, Kamati za Vyama zinaweza zikatatua migogoro hii? Ikiwa Serikali iliyoko madarakani ni ya CCM, je, CCM nao hawaiamini tena Serikali yao? Pana *question mark* hapa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije suala la Mtwara; mimi mwenyewe nilileta ombi la watu wa Mtwara, lakini tikitaka iliyofanyika, na wala siwezi kupingana na kiti, naistahimilia. Niliistahimilia hasa pale nilipoona Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwenda Mtwara na aliporudi alitupa *briefing* Wabunge, tulipata matumaini kwamba, mgogoro umekwisha, bahati mbaya kumbe kunafukuta zaidi. Ndipo nikaona ile haja ya kuwasilisha ombi la watu wa Mtwara, nikaliwasilisha, bahati mbaya yakatokea yaliyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme Bunge lako lina haki ya kuingilia kati migogoro hii kwamba, sisi kama wawakilishi wa Wananchi, tunayo haki ya Kikatiba na ndiyo maana ikawemo kwenye Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwamba Serikali inaweza ikafanya kosa na Serikali inaweza ikaharibu, Mungu wangu! *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niseme kwamba, kilio cha watu wa Mtwara kina misingi mine; leo niitaje ili chanzo hasa kijulikane kwamba wanachotaka ni nini: *Megawatt* 300 za umeme zizalishwe Mtwara. Wanachotaka Lindi na Mtwara iunganishwe na Gridi ya Taifa. Ikiwa haya mambo mawili yatafanyika, Bandari ya Mtwara itafunguka, ajira zitafunguka,

viwanda vitafunguka. La nne ni kwamba, hayo yakitendeka ile dhana ambayo naamini Mkuu wa Mkoa wa Mtwara yupo ananisikia ya *Mtwara Corridor*, aliyoishughulikia kwa jitihada zake zote nayo itafunguka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yote haya ni mambo ambayo watu wa Mtwara wameahidiwa zaidi ya miaka 16. Mambo haya yapo kwenye *Project* iliyoitwa *Power Six* ya miaka ya tisini. Mambo haya yapo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 na 2010, Ibara ya 63, kifungu (j) na (k). (*Makofi*)

Mambo haya yapo katika Hotuba ya Rais aliyoitoa tarehe 10 Juni, 2009 hapa Dodoma. Mambo haya yapo katika Hotuba ya Rais ya tarehe 25 Julai, katika kilele cha Siku ya Mashujaa aliyoitoa Mtwara. Mambo haya yamo katika taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Ikulu tarehe 12 Oktoba, 2011. Yote haya yamo, kilichobadilisha nini? Hapa ndipo kwenye kitendawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuangalie gharama za Mradi; watu wa Mtwara hawapingani na hoja ya gesi kutumika Dar es Salaam, wanapingana na hoja ya kwamba, mambo haya ya kubadilisha yameanza muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, leo niruhusu na nawaomba Wabunge, waende wakatafute *Hansard* ya tarehe 31 Januari, 1997, sitaisoma yote, lakini naomba ninukuu vipengele hivi: Mbunge wa wakati huo, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, aliuliza swali la nyongeza, la msingi mtalitafuta; akauliza akasema, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, Benki ya Dunia imekubali tena kuufadhili Mradi huu; je, anaweza kuwahakikishia watu wa Mtwara kwamba, hatachukua tena fedha hizo kwa manufaa ya mkoa mwingine kama alivyofanya hizi? Makofi yakapigwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri anajibu kwamba, ni kweli kabisa kwamba, sasa hivi fedha ambazo tutazipata kutoka Benki ya Dunia, kiasi cha dola milioni 300, sehemu ya fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kupeleka na kutoa umeme kwa Miji ya Mtwara na Lindi na pia kuwezesha Kanda hiyo ya Kusini

kuunganishwa na Gridi ya Taifa. Sasa haya masuala ni kwamba, wanachofanya ni ahadi za miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, naomba na ninatangaza nia yangu, kipindi hiki cha miezi minne; Aprili, Mei, Juni na Julai, Serikali au Bunge lako litafute hatua mahususi kumaliza suala hili. Vinginevyo, kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili nitaleta tena ile hoja au *petition,* ombi la watu wa Mtwara ikiwa suala hili halijapatiwa ufumbuzi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, katika suala la migogoro, lalala, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Njwayo na Mheshimiwa Kafulila ajiandae.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na suala la maji. Maji ni uhai, lakini kwa masikitiko makubwa, ni takriban miaka 51 kuna baadhi ya vijiji katika Jimbo la Mufindi Kaskazini havina maji. Kuna Kata ya Ihano yenye vijiji sita, hakuna kisima hata kimoja, Mnabulo yenye vijiji vitano hakuna kisima hata kimoja, Ikoya yenye vijiji vinne hamna kisima hata kimoja, Sadani yenye vijiji sita hamna kisima hata kimoja.

Mheshimiwa Spika, juzi tulipata Mradi wa Maji katika Kata ya Mdabulo katika vijiji vyote vitano, wametokea wafadhili ambao wamekubali kutusaidia katika huo Mradi wa Maji, lakini kwa masikitiko makubwa tulipokuwa tunaenda kutafuta vifaa likajitokeza suala la *VAT.* Tumewaomba wenzetu wa Serikali kwa maana ya Wizara ya Fedha, *VAT* ilikuwa ina *amount* ya milioni 90, wale wafadhili wamesema

hatuko tayari kutoa milioni 90 kwa ajili ya kuchangia Mradi huu, fedha tulizozitoa zaidi ya bilioni moja na nusu zinatosha. Cha kusikitisha, mpaka leo hii Wizara ya Fedha hawataki kutusaidia kutoa *exemption* ya milioni 90 ambayo ingesaidia zaidi ya vijiji vitano kupata maji. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliingilie suala hili kati kusudi tuweze kupata *exemption* hiyo ya milioni 90.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo napenda kulizungumzia ni suala la maslahi ya Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Serikali za Mitaa. Katika utaratibu wa utawala, Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Serikali za Mitaa ndiyo wenye watu, Madiwani hawana watu, Wabunge hawana watu, wala Rais hana watu. Kazi za msingi zinafanyika katika maeneo yale, lakini Serikali haiangalii maslahi ya wale watu kule chini. Wanachangia kwa kiasi kikubwa katika utendaji katika nchi hii lakini hatuwaangalii. Wengine wanafikia hatua wanakufa hata Serikali inashindwa kuwasaidia kwa njia moja au nyingine katika mazishi yao. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliangalie jambo hili kusudi watu wetu hawa waangaliwe kwa macho mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la Watendaji wa Vijiji pamoja na wa Kata. Wengi wanakaimu na wanakaimu kwa muda mrefu, kwa hiyo, utendaji wao wa kazi umekuwa wa mashaka. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aziruhusu Halmashauri ziajiri kwenye maeneo haya kwa sababu ukiulizia wanasema tutatoa ajira kesho na kesho kutwa, kwa hiyo, ufanisi wa kutosha katika maeneo haya haupatikani. Kwa hiyo, naomba tuliangalie kwa macho mawili jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la ajira. Kuna tatizo kubwa la ajira katika nchi hii. Kama Serikali inataka kutatua tatizo hili kwa dhati kabisa, ningeomba tujielekeze sana katika eneo la *SIDO*, tuwasaidie wapate mtaji wa kutosha ambao wanaweza kuwafikia Wananchi walio wengi na vilevile tuisaidie Serikali

ifufue viwanda vingi vya nguo ambavyo huwa vinatoa ajira nyingi.

Mheshimiwa Spika, ukienda Cambodia ni nchi ndogo, lakini viwanda vya *textile* vinaajiri zaidi ya watu milioni tatu. Sisi kama tukijika katika eneo hili hata tatizo la uuzaji wa pamba katika nchi yetu lisingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ameamua kwa dhati kuusaidia Mradi wa Nyuki. Mradi wa Nyuki hauna gharama, kama kweli ataamua kujikita na kujielekeza kwa nguvu zake zote katika eneo hili, nina hakika kabisa vijana wengi watapata ajira ya kutosha katika maeneo haya. Nawaomba Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(NEC)* waende kwenye maeneo yote, wasichague baadhi ya maeneo. Kule Mufundi nina taasisi yangu inaitwa *ASHITEK*, ambayo inashughulikia suala la ufugaji wa nyuki. Taasisi hii tumeshasogea hadi Mikoa ya Njombe na Mbeya, tunaendelea kutoa huduma hii. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aongeze nguvu zake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la kilimo hasa cha Chai. Sisi watu wa Mufindi tunalima Chai, watu wa Njombe na Rungwe wanalima Chai, lakini cha kusikitisha, soko na mnada mkuu wa Chai uko Mombasa. Kwa hiyo, Chai yote inayolimwa katika maeneo haya inaonekana inatoka Kenya haitoki Tanzania. Sasa Serikali inatakiwa ifanye juhudi za kutosha ianzishe soko na mnada wa Chai ndani ya nchi yetu kusudi Chai inayotoka Tanzania ionekane kweli inatoka Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule Mufindi tuna *Mufindi Paper Mills (MPM),* wanazalisha karatasi, lakini cha kushangaza hawana kiwanda cha kutengeneza mifuko, mifuko inatengenezwa na kiwanda ambacho kiko Kenya. Ile mifuko ndiyo inafanya *packaging* ya Chai, ikija Tanzania inauzwa kwa dola 100. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa Wizara ya Ubinafsishaji na Uwekezaji, walianglie jambo hili;

hata mifuko Tanzania tunashindwa kutengeneza, hii ni aibu na inasikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalopenda kuchangia ni suala la nguzo za umeme. Wilaya ya Mufindi tunazalisha nguzo za umeme za kutosha, lakini cha kusikitisha ni kwamba, bei ya nguzo katika Wilaya ya Mufindi haitofautiani na bei ya nguzo zinazouzwa Dar es Salaam na Mwanza. Naomba waiangalie Mufindi kwa macho tofauti, pale zinapotoka nguzo, *especially* Mufindi, bei ya nguzo iwe rahisi ukilinganisha na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, suala langu la mwisho ninalotaka kulizungumzia hapa ni hospitali. Katika hospitali nataka nizungumzie maeneo mawili; kwanza ni tiba kwa wazee. Serikali haijajipanga kuhakikisha inawahudumia wazee kupata tiba zao za uhakika. Wazee hawapati dawa, kwa hiyo, wamekuwa wanataabika. Serikali inatakiwa iliangalie suala hili kusudi wazee waweze kupata tiba ya uhakika. *(Makofi)*

Wananchi wametumia nguvu kubwa sana kutengeneza zahanati. Katika Wilaya ya Mufindi, Jimbo la Mufindi Kaskazini tumejenga Zahanati za Ikwea, Itona, Ifupila, Lulanda, Igeleke, Maduma, Kikombo na Vikula, lakini mpaka leo hii zahanati hizi hazijafunguliwa, hazijapelekewa dawa wala hazijapelekewa waganga.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa mwisho ni kuhusu Hati Chafu. Kuna *statement* inasemekana hapa kwamba, wilaya inayopata Hati Chafu haitakiwi kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, Wananchi hawatakiwi kuhukumiwa kwa sababu ya uzembe wa wafanyakazi. Kama kuna mfanyakazi amefanya vibaya, ahukumiwe kwa nafasi ya ufanyakazi wake. Hawa ndiyo wanatuletea matatizo katika nchi hii, unakuta mfanyakazi amefanya jambo baya anaondolewa kutoka kwenye wilaya moja anapelekwa kwenye wilaya nyingine, hapo hatuwasaidii, matokeo yake tunahukumu wananchi ambao hawana hatia yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa sababu nataka nipate fedha kwenye maeneo yetu ili zifanye mambo ya maendeleo. Kwa hiyo, sioni sababu ya kukataa kuunga mkono hoja maana nikikataa nitazipataje hizo fedha kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi wetu. *(Makofi)*

Pamoja na kuunga mkono hoja, nina mambo mbalimbali ya kuishauri Serikali. La kwanza, naomba Serikali iisimamie *TCRA*, Mamlaka inayodhibiti Mawasiliano Tanzania, kwa sababu kama inavyokumbukwa ni karibu miaka miwili nyuma sasa ilianzisha mchakato wa usajili wa simu hapa nchini na tulielezwa kwamba, baada ya usajili ule kupita sasa mtu asingeweza kupiga simu bila kusajiliwa. Kilichopo sasa ni tofauti na mambo tuliyoelezwa; watu wamekuwa wakipiga simu zisizosajiliwa na zimekuwa zinatumika simu hizo kutukana, kufanya mambo ya ovyo na mfumo mzima wa mawasiliano umekuwa na matatizo, hata Wananchi wanaibiwa pesa zao kwenye *ATM* kutokana na usimamizi mbovu ulioko kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Ofisi ya Waziri iwasimamie *TCRA* na Wizara husika, Wizara Mama ya Mawasiliano iwasimamie *TCRA* ili jambo hili lisiendelee tena kuleta kero kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutoa ushauri kwa Serikali, kwa muda mrefu sana tumekuwa tukisikia taarifa kwamba, Serikali imekuwa ikipata mapato makubwa sana yanayokusanywa na *TRA*, lakini katika matumizi tumekuwa tunawasikia Mawaziri wakilalamika kutokuwepo na fedha za kutosha wakati tumeshaambiwa *TRA* imekuwa ikikusanya.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba tuwe tunaelezwa ukweli kwa nini maeneo ya kukusanya fedha ni mengi lakini

matumizi yanakuwa na hitilafu. Kwa maana hiyo basi, naomba kuishauri Serikali labda iongeze vyanzo vyake vya kukusanya mapato ya Watanzania, tuanzishe Bandari Kavu nyingi na za kutosha ili zisaidie kuongeza pesa.

Vilevile Taasisi ambazo ni chanzo kizuri cha kupata pesa, zitengenezewe utaratibu mzuri wa kuboreshwa ili ziweze kusimamia upatikanaji wa fedha. Kwa mfano, tunayo Mamlaka inayosimamia Madini nchini *(TMAA);* ina matatizo makubwa kweli kwenye vifaa na hata mapato yao kama mamlaka. Watu hawa miezi mitano iliyopita, *Airport* zetu zilizopo nchini zimeweza kukusanya bilioni 13 katika muda wa miezi mitano. Maana yake nini? Watu hawa tukiwatengenezea mazingira mazuri, wanaweza wakapata pesa nyingi za kutosha zikapunguza ukwasi uliopo kwenye bajeti yetu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nirudi nyumbani Mtwara kidogo; Mkoa wa Mtwara au Kanda ya Kusini ndiyo maeneo ambayo hayana Hospitali ya Rufaa. Hivi leo mtu wa Tandahimba au Nanyamba akipatwa ndwele, akipata ugonjwa analazimika kwenda Dar es Salaam ambako ni mbali na mnajua tena wakati mwingine unapata ugonjwa ukiwa haukukaa vizuri kiuchumi. Sasa hii shughuli ya kupata rufaa ya kwenda Dar es Salaam tumechoka Wanamtwara. Ningeiomba Serikali, iamue kwa makusudi sasa katika hii miaka miwili tuijenge hospitali yetu ya rufaa pale Mtwara. Natambua kuna ujenzi wa *fence* pale ambao unapendeza lakini haina maana kuwepo *fence* tu kuwepo kwa maeneo, tunachotaka hapa kutengwe fedha za kutosha ili tuwaokoe Watanzania walioko kule.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 70 ndiyo gharama za Mradi uliopo. Ningependa tunapomaliza *general budget* ile, tupate angalau bilioni 35 za kuanza pale na awamu nyingine tumalizie bilioni 35 tuepukane na hii adha ya kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchangia Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi. Mkoa wetu

wa Mtwara unaunganishwa na barabara hii, lakini barabara hii ndiyo ya uchumi, ndiyo inayoleta mapato mengi ya Mkoa wa Mtwara na nchi. Inachangia kwa kiasi kikubwa kwa sababu asilimia 60 ya korosho zote za Tanzania zinatoka Mtwara na hasa Wilaya za Tandahimba, Newala, Masasi na Mtwara Vijijini. Tukiiboresha barabara hii itakuwa chanzo kizuri cha uchumi. Natambua kwamba, tarehe 28 Machi, 2013 kumetangazwa *tender* ya kuifanyia upembuzi yakinifu barabara hii. Ningeomba tuongeze kasi au *speed* ya jambo hili ili katika muda mfupi ujao tusiendelee kupata adha tena huku tukitilia maanani kwamba, barabara hiyo ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina matatizo makubwa sana ya soko la mazao ya kilimo; ukisikia pamba ni tatizo, korosho ni tatizo, chai ni tatizo, tumbaku ni tatizo na hii kwa kweli inatokana na kwamba, hatuna mpango mkakati wa kutafuta masoko ya uhakika ya mazao yetu. Leo hapa kwa muda mrefu Serikali imekuwa haina mpango wa kuyaongezea thamani mazao yetu, badala yake inapeleka mazao yetu kwenye *raw form,* jambo ambalo watu inakuwa vigumu sana kuchangamkia manunuzi ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa rai kwa Serikali, tuamue kwa dhati kabisa sasa kuwekeza kwenye uongezaji wa thamani ya mazao yetu na hii itatusaidia sana kupata soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeona ukurasa wa 31 mpaka wa 37, amejaribu ku-*introduce price stabilization fund,* jambo ambalo litasaidia kwa namna moja au nyingine, bei itakapokuwa inashuka basi kutakuwa na *compensation* kwa wakulima. Ninachosema, kwa uzoefu nilionao, jambo hili litakuwa bure kwa sababu tuna changamoto nyingi. Moja ya changamoto ni wafanyabiashara wanao-*curtail* kuhakikisha kwamba wanawadhulumu wakulima, kwa hiyo, Serikali lazima ianze

kwanza kuwabana hao maana hata tukileta huu mfumo wa *stabilization fund ...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njwayo, ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa David Kafulila, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi na Mheshimiwa Kakoso ajiandae.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda kuwa mfupi, nianze moja kwa moja na dhana nzima ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, hili Taifa ni miongoni mwa Mataifa tajiri sana Duniani, lakini kwa miaka mingi kwa sababu ya kukosa uongozi sahihi na thabiti, tumeendelea kuwafanya Watanzania kuwa maskini pasipo sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu Taifa la Tanzania limetajwa kuwa ni la pili kwa vyanzo asilia vya utalii Duniani baada ya Brazili. Ukitaka kujua ni kiasi gani tunapata kwenye utalii, ni chini ya asilimia kumi ya kile ambacho tunastahili kukipata kwa sababu hatujajiandaa katika utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya 11 kwa mito mingi Duniani, lakini zaidi inao utajiri wa Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika ni Ziwa ambalo linachangia asilimia 17 ya *fresh water* Duniani. Maji yote duniani ni kama bilioni 1.4 kilomita za ujazo, lakini maji ambayo yanafaa kunywewa Duniani ni kama kilomita za ujazo milioni 35, Ziwa Tanganyika kati ya milioni 35 kilomita za ujazo, ina-*contribute* asilimia 17.

Mheshimiwa Spika, lakini ni huzuni kwamba, watu wa Kigoma, wanaokaa mita 100 kutoka usawa wa Ziwa, hakuna maji ya uhakika. Mlitaka Mwenyezi Mungu aisaidie Kigoma kiasi gani ili isiwe na kero ya maji? Utafiti umefanywa na *SENOBET*, Kampuni ambayo ni miongoni mwa Makampuni

makubwa kwa ku-*collect opinions* Duniani. Kero ya maji Tanzania ndiyo kero namba moja; yaani kama kunahitajika kuweka *stimulus package* tungeweka kwenye maji. Akina mama wanaumia, maji ni kero na Serikali hii nikiiangalia sioni matumaini. Sioni matumaini ya kwamba, kuna Serikali ambayo ipo *serious* na tatizo la maji. Watu wanaumia na tatizo la maji. Serikali kila siku inapanga bajeti kidogo kwa sababu uwezo wake wa kukusanya ni mdogo. Nchi ina vyanzo vingi, lakini uwezo mdogo wa watawala, matokeo yake akina mama wanaumia kwa kufuata maji kilomita nzima; haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii Tanzania ina kila aina ya utajiri, tuna hii *Coastal Zone,* tuna karibu kilomita 1,424 za *Coastal Zone* Bandari ya Hindi. Namibia wana kama kilomita 1,500 za *Coastal Zone*. Namibia *export* peke yake ni milioni 340 kwa mwaka. Tanzania ni vitu vya aibu, kila kitu cha utajiri tunacho, tunashindwa nini kuwatajirisha Wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, leo tunalia na tatizo la ajira, lakini moja ya maeneo ambayo yanatengeneza ajira nyingi Duniani ni *processing* na *manufacturing industries*. Mkijenga viwanda vya ku-*process* bidhaa, mkijenga viwanda vya kuzalisha mnaweza mkatatua tatizo la ajira. Hamuwezi kuwadanganya Wananchi hapa kwamba, kuna Serikali itakayoajiri Wananchi wote wanaohitaji ajira; haipo, lakini ni wajibu wa Serikali kutengeneza misingi ambayo itasababisha watu wapate ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunasafirisha pamba zaidi ya magunia 400,000 kwenda nje; ni mambo ya aibu; tunapeleka ajira Ulaya, India na Marekani wakati Tanzania kuna tatizo la ajira. Tungeweza kutengeneza *base* ya viwanda vya *manufacturing* tungetatua tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, kabla muda haujakwisha, nisingependa kumaliza kuzungumza kabla sijagusia tatizo la ardhi. Moja ya mambo ambayo leo hii Duniani na Mheshimiwa Spika wewe ni shahidi maana unakwenda kwenye vikao vikubwa Duniani, ni tatizo kubwa la *land*

*grabbing*. Kule Kigoma Uvinza amekuja mwekezaji, ambaye kuna kila dalili kwamba, huyu ni tapeli, anapewa ardhi ya Makao Makuu ya Wilaya hekta 10,000. Muda siyo mrefu, taarifa zimetangazwa Duniani, mshirika wake ambayo ni *Law University,* amejitoa kwa sababu hamwamini yule mwekezaji. Lakini Serikali yetu haishtuki kwamba huyu ni tapeli, hatukatai uwekezaji, lakini lazima tuwe na *genuine investors,* tuwe na wawekezaji ambao ni sahihi. Humu ndani wapo watu ambao wakiwezeshwa mitaji ya kutosha wanaweza wakawekeza wakatengeneza ajira. Kenya wanafanya nini na sisi tunashindwa nini?

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo tunahitaji Serikali ibadilike kufikiri na hii fikra ya Serikali inaanzia kwetu sisi Wabunge. Ningependa kabla sijamaliza, nisasahau tatizo ambalo tulilipitisha kwenye Bunge lililopita, tulipitisha Sheria hapa ya kwamba, *CAG* atakapoleta taarifa Bungeni hapo hapo na Serikali itenge taarifa yake. Leo Mawaziri hawa hapa tangu jana mmewaagiza; taarifa ipo wapi hapa? Tunapitisha sheria za ndiyo matokeo yake tunasababisha *crisis* hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuhitaji Bunge limalizike hapa bila taarifa ya Serikali kuletwa. Watuambie taarifa hiyo imekaguliwa lini na *CAG*. Kwa utaratibu wa kawaida, *CAG* akishafanya uchunguzi wake anaipa Serikali, Serikali inajibu, ikishajibu hiyo ndiyo inakuwa taarifa sahihi ya Serikali. Kwa sababu *CAG* ameonekana kwamba ni msaada kwa Watanzania, anatoa vitu ambavyo vinasababisha kui-*shape* Serikali iende Wananchi wanavyohitaji, akaonekana ni tatizo mnaanza kutunga sheria za kufinya kushoto, mnafinya kulia; kwa maslahi ya nani? Halafu mnawalazimisha Watanzania waseme hakuna haja ya kuzozana, ni nchi yetu sote; yetu sote mnakula wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema hapa kwamba, sungura ni mdogo, lakini siyo kweli kwamba sungura ni mdogo. Katika maeneo ambayo ni tatizo katika Serikali hii ni manunuzi na tunajua zaidi ya asilimia 60 ya fedha za Serikali inakwenda kwenye manunuzi. *CAG* jana alizungumza hapa kwamba,

michakato mizima ya manunuzi, bei huwa ni mara mbili ya bei ya kawaida. Hii ni kwa sababu Watendaji wa Serikali siyo waaminifu. Kuna gharama za safari, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kimsingi, namheshimu sana na amekuwa akisema kwamba atajitahidi, lakini mpaka sasa bado kuna tatizo la matumizi ya safari za Viongozi na hasa Viongozi Wakuu. Kiongozi anasafiri misafara mikubwa na watu wengine hawana hata kazi, lakini *traveller agents* wale ambao Serikali inawatumia wana-*charge fee* kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kufanya uchunguzi kuhusu masuala ya safari. Kuna gharama kubwa sana ambazo tunazipoteza, kuna gharama kubwa sana ambazo Serikali inazipoteza kutokana na mfumo mbovu wa manunuzi.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza hapa kwamba, huwezi ukajenga uchumi kama hujajenga reli imara, kama hujawa na usafiri wa meli wa uhakika. Mwaka wa 1990, Reli ya Kati ilikuwa na uwezo wa kusafirisha tani 1,400 kwa mwaka, leo inasafirisha chini ya tani 400 kwa mwaka. Serikali ikianza kujitahidi kidogo wanasema kwa nini hamuisifu CCM; tuisifu imebomoa yenyewe halafu irudishe kidogo ipate sifa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, reli aliyoiacha Mkoloni ilikuwa bora kuliko ya leo, mkirekebisha kidogo mnaomba sifa; sifa ipi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Natse.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ili na mimi kwa niaba ya Wananchi wa Bukene, niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanza na suala la maji. Maji bado ni tatizo katika maeneo mengi ikiwemo na ndani ya Jimboni langu la Bukene.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi ambayo ni ya faraja sana kwetu sisi Wanamkoa wa Tabora kwa ujumla, ya kufikisha maji ya Ziwa Victoria kutoka Kahama yafike Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hofu yangu katika hili ni kasi ya utekelezaji wa ahadi hii ya Rais. Ahadi hii ya Rais ina *timeframe;* Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba, kabla ya mwaka 2015, kabla hajamaliza muda wake wa Uongozi wa Awamu ya Nne, maji ya Ziwa Victoria yatafika Tabora kutokea Kahama.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tupo mwaka 2013, bado kama miaka mawili na Mradi mkubwa kama huu wa kutoa maji Kahama kuyafikisha Tabora hauwezi kutekelezwa kwa miezi mitatu, miezi sita, ni mradi ambao angalau unahitaji miaka miwili na kitu kuutekeleza. Sasa hivi tumebakiza miaka miwili kufika mwaka 2015, kwa hiyo, kwa kasi tunayoenda nayo, nina hofu kwamba kama hatutaongeza *speed* basi inawezekana ahadi ya Rais isitekelezeke, jambo ambalo Wanatabora hatutaki litokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahadi hii ikitekelezeka, Wananchi wengi sana watafaidika na maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria. Katika Jimbo langu la Bukene, Wananchi wa Igusule, Nawa, Wamara, Lubumbu, Itobo na Busasi, watafaidika na kupata maji haya. Wananchi wa Nzega Mjini vilevile na wa Igunga na maeneo yote ambayo yapo barabarani katika njia ya Nzega – Tabora, watafaidika na maji haya ya kutoka Ziwa Victoria. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho, atoe maelezo ili tujue *status* ya utekelezaji wa Mradi huu iko vipi, Serikali imejipanga vipi, upembuzi yakinifu utaisha lini, fedha zitapatikana vipi, ni za ndani au ni za nje; kwa sababu hatutaki ifike mwaka 2015 ahadi ya Rais iwe haijatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa 30 wa Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu, umezungumzia masuala ya umwagiliaji. Nimeona kwamba, Serikali imejipanga kujenga mabwawa mapya ya umwagiliaji. Sipingi dhana ya kujenga mabwawa mapya, lakini naishauri Serikali kwamba ni jambo jema pia kuhakikisha mabwawa na skimu za umwagiliaji ambazo zimeanza kujengwa zinakamilika zinafika mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu kwangu katika Jimbo la Bukene, nina bwawa kubwa la Kahama Yaharanga, ambalo lina uwezo wa kumwagilizia hekta 500. Serikali karibu imetumia milioni 900 miaka minne, mitano, nyuma kulijenga kwa maana ya tuta. Bwawa hili halijaweza kuanza kufanya kazi iliyokusudiwa kwa sababu miundombinu ya mifereji ambayo itatoa maji kwenye bwawa kupeleka kwenye hizo hekta 500 haijajengwa hadi leo.

Mwaka jana nilimwuliza Waziri mhusika, alinijibu kwamba, wamefanikiwa kupata shilingi 200,000,000 kutoka Mfuko wa Umwagiliaji wa Wilaya ambazo zingetumika kujenga hiyo mifereji, lakini mpaka leo hakuna chochote ambacho kimefanyika. Kwa hiyo, hofu yangu ni kwamba, Serikali tumetumia shilingi 900,000,000, fedha nyingi kujenga tuta kwa maana ya bwawa na mvua zimenyesha, bwawa limejaa lakini maji hayatumiki kwa sababu mifereji ya kupeleka maji kwenye hizo hekta 500 haipo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati anatoa maelezo, tuelezwe kwamba, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha miundombinu ya mifereji ili sasa shilingi 900,000,000 zilizotumika kujenga bwawa ziwe na faida, ziwe na tija, kwa sababu *otherwise* tutakuwa tumetumia shilingi 900,000,000 bila ya faida, ambapo ni hasara na ni jambo ambalo halina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lipo katika ukurasa wa 70 kuhusu ugawaji wa maeneo mapya ya utawala. Wilaya ya Nzega ni moja kati ya Wilaya kubwa sana hapa nchini. Kwa mujibu wa sensa iliyopita, Wilaya ya Nzega sasa hivi inakaribia kuwa na watu 600,000 na ina Kata 37 ambayo nadhani ni ya pili kwa wingi wa Kata baada ya Wilaya ya

Kahama. Sasa sisi ndani ya Wilaya ya Nzega, kwa kutumia taratibu zilizopo tumeshaanza michakato ya kuwashirikisha Wananchi, kushirikisha vikao halali, ili kupendekeza sasa tusogeze huduma za kiutawala, huduma za kiuchumi na za kijamii karibu na Wananchi kwa kupendekeza kuimega Wilaya ya Nzega na kuunda Wilaya mpya ya Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Bukene ni kubwa, lina Kata 16, zaidi ya kilomita za mraba 3000 na tuna uwezo wa kukusanya mapato ya ndani karibu nusu bilioni kutokana na pamba, tumbaku na mazao mengine ambayo tunalima. Kwa hiyo, imefika wakati kwamba, sasa tusogeze huduma za kiutawala, huduma za kiuchumi na za kijamii karibu na Wananchi kwa kuwa sasa na Halmashauri na Wilaya mpya ya Bukene. Tunaomba mapendekezo yetu yatakapofika ngazi za TAMISEMI, ngazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, yazingatiwe ili katika Wilaya na Halmashauri mpya zijazo, pengine mwaka ujao, basi Halmashauri na Wilaya mpya ya Bukene, iwe ni mojawapo kati ya Halmashauri ambazo zitazingatiwa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 71 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imezungumzia maafa. Maafa ni jambo ambalo mtu halitegemei, linakuja bila ya mtu kutarajia. Ni rai yangu kwamba, Mfuko huu uimarishwe kwa maana ya kuongezewa fedha, kwa maana ya kuongezewa ustadi na vifaa ambavyo vinahitajika, lakini uwezo huu ushuke katika ngazi za Wilaya na ngazi za Halmashauri. Katika ngazi za Wilaya huko kuna Kamati za Maafa zinazoongozwa na Wakuu wa Wilaya, lakini changamoto kubwa unakuta hawako vizuri kiuwezo, kiuwezeshaji, kwa hiyo, unakuta maafa yanatokea watu wanakimbia na kuhangaika tu lakini waliokumbwa na maafa hawasaidiwi. Juzi na jana kwangu kule Jimbo la Bukene, mvua kubwa zimenyesha, mafuriko yametokea na zaidi ya nyumba karibu 200 zimeanguka. Namshukuru Mkuu wa Wilaya na Kamati yake ya Maafa ya Wilaya ya Nzega, wanahangaika wanajitahidi, lakini wawezeshwe. Nawapa pole Wananchi wa Bukene, ambao nyumba zao zimeathirika.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Nianze na suala la miundombinu. Mkoa wa Katavi ni mpya na mkoa ambao uko pembezoni unahitaji zaidi kupata huduma ya miundombinu. Serikali ilipokuwa imetoa mpango mkakati wa kuiwezesha mikoa iliyo pembezoni kupewa huduma za barabara, Wananchi tulifurahi sana, lakini bahati mbaya mpaka sasa barabara ya Mpanda - Sumbawanga bado ujenzi wake unaenda kwa kusuasua. Nilikuwa naiomba sana Serikali iharakishe kumalizia barabara inayotoka Sumbawanga kuja Mpanda kupitia Kibaoni ikamilike mapema. Kuna barabara ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma, ni muhimu sana na ni kiunganishi kati ya Wananchi wa Mpanda na Mkoa wa Kigoma. Barabara hii iliahidiwa na Serikali ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, bahati mbaya mpaka sasa bado wala dalili zile za kuanza kwa ujenzi hazijafanyika. Naiomba Serikali iharakishe mchakato wa barabara hii ili ujenzi uanze, uweze kuleta maendeleo mazuri kwa Wananchi wa Mikoa hii miwili; Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo barabara muhimu sana; barabara ya Mpanda kupitia Inyonga Wilaya mpya ya Mlele kwenda Tabora. Barabara hii ni kiunganishi kwa Wananchi walio wengi, hasa wa Kanda ya Ziwa. Barabara hii inatumiwa na watu wengi kuanzia Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na Mkoa wa Kagera. Ni kiunganishi kinachowasaidia Wananchi walio wengi kupata huduma ya barabara, ambayo ndiyo inayowaunganisha kupata chakula kutoka katika Mikoa ya Rukwa na Katavi. Naiomba Serikali iharakishe upembuzi yakinifu uliokuwa umelengwa ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Itawasaidia sana Wananchi na kukuza uchumi katika maeneo ya mikoa hii kwa maana ya Mkoa wa Katavi, Tabora na kurahisisha huduma nzuri katika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na mingineyo.

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna barabara ndogo zinazounganisha Wilaya. Tunayo barabara ya Karema – Mpanda, inahitaji iboreshwe na kujengwa kwa kiwango cha lami, kwa sababu eneo hili ni eneo linalounganisha mpaka kati ya nchi ya DRC Congo na nchi yetu ya Tanzania. Ni vizuri katika maeneo haya hasa ya kiusalama yakaboreshwa na ukiangalia ni sambamba na ujenzi unaoendelea wa Bandari kule Ziwa Tanganyika ili tuweze kuwaunganisha Wananchi wa maeneo haya waweze kukuza uchumi wao. Haitakuwa vizuri na wala haitapendeza kama tutajenga bandari wakati barabara inayounganisha hapa ni ya udongo. Nilikuwa naiomba Serikali ijielekeze huko.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ninalopenda kulichangia ni la huduma ya maji. Maji ni tatizo katika mikoa ya pembezoni. Wananchi walio wengi katika vijiji vingi hawana huduma ya maji. Tuna Vijiji vya Igagala, Vikonge, Katuma na Kasekese ambavyo havina huduma ya maji ambayo toka kuanza kwa nchi hii au kupata kwa uhuru, hawajawahi kupata huduma ya maji. Naiomba Serikali iongeze bajeti ya maji kwani maji ni tatizo na maji ni uhai na maji ndiyo yanayotegemea Wananchi walio wengi waweze kupata huduma huko vijijini. Nitawashangaa sana pale tunapoelekeza nguvu kubwa sana kupeleka maji maeneo ya mijini wakati kwenye matatizo mengi zaidi ni vijijini kwani Wananchi wanapoteza muda mwingi sana kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni suala la kilimo; naiomba Serikali iongeze nguvu kuhakikisha wanaiwezesha *NFRA* kupewa fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa mazao. Wananchi walio wengi wanajitokeza wanalima lakini mazao yao hayapati soko; naiomba Serikali iliwezeshe Shirika hili lipewe fedha za kutosha ili waweze kununua mazao kwa wakati mwafaka na kuweka vya kutosha na hii itawasaidia sana wakulima kuwa na jitihada za kuzalisha kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la elimu. Katika maeneo ya Jimbo langu tuna tatizo kubwa sana la walimu hasa wa shule za sekondari. Tunaiomba

Serikali iongeze walimu. Tuna Shule ya Ikola ina walimu wawili tu na Shule ya Katuma nayo ina walimu wawili, lakini karibu Jimbo zima shule hizo zina walimu wachache sana. Tunapotaka kuboresha elimu lazima tuwape walimu wa kutosha sambamba na kuboresha mazingira ya walimu. Walimu walio wengi wanaishi katika mazingira mabaya, wana nyumba ambazo siyo stahili, kwa hiyo, tunaomba tuwawezeshe waweze kupata nyumba nzuri na kuwafanya wapate motisha na kuboresha mishahara yao; hii itasaidia kukuza elimu katika maeneo yote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na suala la migogoro ya ardhi. Tuna migogoro mingi sana ya ardhi katika maeneo ya Wilaya ya Mpanda hasa kuongezwa kwa mipaka katika maeneo ambayo wanapakana na Hifadhi za Mapori na Hifadhi za Taifa. Naishauri Serikali, tutumie busara tunapokuwa tunapanua maeneo haya, tuwashirikishe Wananchi ili waweze kuelewa maeneo halisi na kuwapa mipaka ambayo itawasaidia kuondoa migogoro. Kinachofanyika ni tofauti kabisa, Serikali inaweza ikaja tu ikafika ikapanga na kuonesha mipaka ambayo haijawashirikisha Wananchi. Naiomba Serikali ikae vizuri na iwashirikishe Wananchi kwani tunapokuwa na mipango shirikishi haiwezi ikaleta migogoro. Migogoro ya ardhi ni mikubwa sana katika nchi hii, itakayochangia uvunjifu wa amani. Naomba eneo hili tulipe uzito na tuhakikishe tunawasaidia Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbilinyi dakika tano na Mheshimiwa Natse dakika tano.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Leo naomba nianze kwa kunukuu maneno machache ya kwenye Biblia. Biblia inasema: “Mwanamke mpumbavu huibomoa nyumba yake kwa mikono yake mwenyewe.” Vivyo hivyo, Serikali pumbavu hulibomoa Taifa lake kwa mikono yake yenyewe ambalo ni Baraza la Mawaziri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, sasa sipendi tufike huko.

**SPIKA:** Serikali pumbavu ni pamoja na wewe. Naomba ujadili hoja yako vizuri tu. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, mimi siyo Serikali.

Bunge hili ni sehemu ya kujadili maslahi ya Taifa, lakini hawa watu wamekuwa wanatumia wingi wao katika kukwamisha masuala muhimu ya Wananchi. Juzi, Bunge lililopita hapa tulikuwa na hoja ya mitaala ya Mheshimiwa Mbatia, mkatumia wingi wenu mkaizuia mkamnyanyapaa Mheshimiwa Mbatia kwa Ubunge wake wa Kuteuliwa mkidhani kwamba mnamdhalilisha yeye bila ya kujua kwamba, mnamdhalilisha mtu aliyemteua. Mkamnyanyapaa Mheshimiwa Mbatia, mkajaribu kuficha ugonjwa maradhi yamewaumbua, matokeo ya Kidato cha Nne mmeona kilichotokea. *(Makofi)*

Mimi nasema hivi: "Mlificha maradhi msiba humwumbua." Mnakuja mnasema kwamba tunafanya kazi, sijui ooh Wanamapinduzi wale wengine akina Mheshimiwa Mwigulu kule wanakaa humu ndani wanaongea vitu gani, wanaongea vitu, wanataja watu majina, wanataja eeh; hii yote ni nini? Hatuwezi kuwa na elimu wakati Waziri anayehusika na elimu, elimu yake ni ya kuungaunga na hili nitoe lawama moja kwa moja kwa Usalama wa Taifa, kwa sababu Usalama wa Taifa wakati Mheshimiwa Rais anateua Mawaziri; kwa nini wasimwambie bwana tunalo faili la mtu fulani huyu ni chenga, huyu ni boya usimuweke atakuumbua! Angalia sasa Mheshimiwa Rais hana la kufanya, amemteua mtu, magazeti yanaandika na hakuna mtu yeyote anayejibu. Usalama wa Taifa umekalia kufuatilia masuala ya CHADEMA tu na kung'oa watu kucha, kung'oa watu meno, hizo ndiyo kazi wanazofanya badala ya kulisaidia Taifa na kumsaidia Mheshimiwa Rais kufanya vitu vilivyo sahihi.

Sasa nasema hivi, nakataa kuwa sehemu ya hii na niseme wazi, mimi Joseph Mbilinyi, kwa unyenyekevu mkubwa ninayo heshima kwa Wanambeya walionichagua kuwawakilisha katika masuala yao, lakini nikikaa nikiangalia sijisikii fahari sana kuwa sehemu hii. Kuwa sehemu na watu kama akina Mheshimiwa Mwigulu. Wanakuja hapa, ni mpumbavu kwa sababu wewe utafanyaje dili halafu unatuma hela kwa M-Pesa!

**SPIKA:** Naomba ukae chini, naomba ukae chini. Lugha zingine zinaudhi na hazina sababu. Ukitaka kujenga hoja yako unaweza, neno mpumbavu huwezi kulitumia katika Bunge hili. Nakwambia sasa nitawataja majina, Kanuni inaniruhusu mimi kuwataja watu majina na nikiwataja mnachukuliwa na Polisi. Endelea Mheshimiwa Mbilinyi, dakika zako zilizobaki.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, naomba Taifa linielewe kwamba, mpumbavu siyo tusi na ndiyo maana Biblia imetumia. Upumbavu ni *stupidity* na *stupidity is lack of knowledge and understanding,* ambapo Mawaziri wengi humu ndani wana-*lack of knowledge and understanding* na ndiyo wanasababisha Taifa hili liwe hivi na hatutaendelea ku-*take* hiyo kitu kabisa. *(Makofi*)

**SPIKA:** Tunaomba tumalize, Mheshimiwa Mchungaji Natse.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Hakuna taarifa tunaendelea, nimesema Mheshimiwa Natse, hakuna mtu anayetoa taarifa.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kuchangia kuhusu suala la udini. Suala la udini ni *very sensitive*. Migogoro imekuwepo na watu wameendelea kuifumbia macho. Kipekee niseme, Serikali iliyoko madarakani imeshindwa kuchukua hatua kufanya maamuzi, ina *power* na *authority* imenyamaza. Nakumbuka Awamu ya Pili ya Mzee Mwinyi,

matatizo yalipoanza ya mabucha ya Kitimoto alitamka tu na mambo yakaisha.

Mheshimiwa Spika, ninauliza; *if you have clean heart why worry* ya kutokufanya maamuzi? *We have very poor decision making* katika Serikali yetu. Niombe hilo lifanyike, hatuwezi kuvumilia kuona nchi hii inaingia katika majanga, maasi na mauaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwa takriban miaka miwili sasa kuhusu ugatuaji wa madaraka, Kijiji cha Chemchemi katika Halmashauri ya Karatu hakina uongozi, baada ya Wananchi kuiondoa Serikali yao. Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, aki-*wind up* aniambie ni lini Wananchi wa Kijiji cha Chemchemi watapata Serikali yao?

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mheshimiwa Mbunge wa Longido, alisema hivi kuhusu Longido na Ngorongoro, niwaambie Wananchi wa Ngorongoro na Loliondo, semeni, teteeni haki yenu. Alisema, akina mama wamenituma, Wananchi wa Dubai wanaendelea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kukaribia kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante. *Okay,* endelea ya kwanza.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, dakika zangu zilichukuliwa kidogo tu. Akina mama wamemtuma wanasema kwamba, watoto wa Dubai wananeemeka, wa Loliondo na Ngorongoro wanateseka. Hii inadhihirisha wazi kwamba, Serikali haiwajali ninyi wa Loliondo na Ngorongoro; teteeni haki yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Ukienda kwenye Taifa la watu makini, Taifa la watu wenye akili, huwezi kukuta wanapuuzia mambo muhimu kama mchakato wa Katiba

katika nchi yao. Ukienda katika Taifa la watu makini huwezi kukuta watu wakipuuzia mambo ambayo ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa kama vile amani, umoja, upendo na mshikamano wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanakata *cross party lines,* yanakwenda mbele zaidi ya misimamo na mitazamo ya kiitikadi za vyama vya kisiasa; ni mambo ya Kitaifa, ni mambo ambayo ni roho ya ustawi wa nchi yoyote katika Dunia hii. Katika Taifa letu, kwa sababu ya upuuzi tunajikuta tunadharau mambo kama haya na matokeo yake tunaacha watu wanayachezeachezea, tunaacha watu wanatuvuruga ilihali tukijua kabisa wanachezea Ikulu. Nafikiri ninaeleweka nikisema Ikulu? Hata siku moja huwezi kukuta mzee akamruhusu mjukuu wake achezee Ikulu hata kama anampenda namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sisi tunaruhusu watu wanapiga Ikulu, wanachezea mchakato wa kuleta Katiba mpya, wanachezea mchakato ambao utatupelekea kufanya mabadiliko ya mustakabali mzima wa kimfumo wa kuongoza nchi yetu, tunawaacha wanachezea; ni upuuzi na tutahukumiwa kwa upuuzi huu. Leo hii tunawaacha watu wanafanya matukio mbalimbali ya kuvunja amani katika nchi yetu, wanafanya maandamano kucha kutwa, wanateka watu nyara, wanawaadhibu, vyombo vya ulinzi na usalama vipo, Serikali inasingiziwa imenyamaza tu! Haya mambo yanajulikana, ushahidi upo wazi na sisi tumenyamaza tu tunaacha tunasema tunalinda Umoja wa Kitaifa.

Tunaleta mustakabali wa pamoja, uongozi wa pamoja, *inclusive leadership;* hakuna *inclusive leadership* bila kuwa na utawala bora wa kisheria. Lazima kwanza watu waheshimu Sheria na Taratibu zilizowekwa ili tuweze kuona sasa kuna amani. Leo hii anasimama Kiongozi Mwandamizi wa Chama cha Siasa kwenye majukwaa na hata ndani ya Bunge, anasema hadharani kabisa kwamba, nchi haitatawalika na anaachwa tu. Huo wote ni upuuzi na huu upuuzi unasababishwa na wale wenzetu waliokaa kwenye Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nawaomba hapa leo hii, muanze kuchukua hatua, watakapoingilia huu mchakato wa Katiba ambao tumeupitisha hapa Bungeni tukakubaliana wote hakuna aliyepinga, sasa leo hii wakatoka huko nje wakafanya mambo ya kipuuzi wakaachwa tutasema sasa na Serikali nayo inalea upuuzi. Basi sasa sisi tutashindwa kuwaelewa wengine, ndani yetu tutaamua kuchukua hatua. Kwa mfano, wakijaribu kufika Nzega, ninaahidi ndani ya Bunge hili Tukufu, nitawahamasisha Wananchi wa Nzega watawakamata kuanzia viongozi wao hadi wafuasi wao na nitawashughulikia mimi binafsi kama Serikali itashindwa kuwashughulikia. Hatuwezi kukubali upuuzi wa namna hii ukiendelea na sisi wengine tumenyamaza na Serikali imenyamaza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni kiongozi mpuuzi tu, anayeweza kuona hoja imeletwa kwenye Bunge imejadiliwa wakatoka nje ya mchakato, sasa baadaye wanarudi kinyumenyume wanapitia mlango wa uani wanaenda kuongea na Mheshimiwa Rais Ikulu, Mhashimiwa Rais anawakubalia tu kwa wema kabisa twendeni na yale mnayoyataka, inatengenezwa Tume ya Katiba ambayo ina Wajumbe miongoni mwao ni washauri wao kama Profesa Mwesiga Baregu, ni mshauri wao mkubwa na ni msomi mkubwa katika nchi hii, yumo ndani ya Tume. Leo hii Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni anachangia anasema, Katiba haina weledi. Katiba haina weledi wakati ndani yake kuna watu wazito kama Profesa Mwesiga Baregu, ambaye ni Mshauri Mkuu wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo; anasema hakuna dhamira kwamba, Tume ina upungufu ndani na nje. Sasa huu upungufu unatoka wapi wakati mchakato wa kutengeneza Tume mlishirikishwa na ninyi ni sehemu ya uamuzi huo wa kutengeneza hiyo Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa namna hiyo apuuzwe na Watanzania, apuuzwe yeye na Chama chake na Watanzania wakiwaona wasiwaunge mkono wawakatae kwa sababu hizo za upuuzi wao. Zaidi ya yote, Watanzania wasikubali kuburuzwa na Viongozi wa aina hii. Watanzania

nawasihi mwangalie matukio ya uvunjifu wa amani yanatokana na nini. Mojawapo kubwa ni kauli za Viongozi ambao ni wapuuzi wanapuuza mhimili wa amani, mshikamano na umoja wa Kitanzania. Wanatoa kauli ya kusema nchi haitatawalika, wanasema kila kitu wao wanapinga tu, falsafa inayowaongoza ni *oppose everything propose nothing.* Hawana wanacho-*propose*, wao ni kupinga kila kitu na ni kupinga kila siku, matokeo yake hawana hata kitu kimoja wanacholeta cha maendeleo kwa Watanzania. Watu wa namna hii ndugu zangu Watanzania ni wa kuwaogopa na kuwakataa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nijielekeze kwenye jambo moja tu ambalo ni la muhimu kwa wapigakura wa Jimbo la Nzega na hili ni la maji ya kutoka Ziwa Victoria kuja Mkoani Tabora. Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ninaomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, isipuuze ahadi ya Mheshimiwa Rais, itekeleze Mradi huu kadiri ilivyokuwa imeahidiwa ndani ya muda ili mwaka 2015 tuwe nalo la kusema kwenye majukwaa ya kisiasa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bila kusahau, naunga mkono hoja. Mwisho, nimalizie kwa kusema, wanaozomea wote ni wapuuzi na niwataarifu tu kwamba, upuuzi wa namna hii hauwezi kuwasaidia kuchukua nchi, upuuzi wa namna hii hauwezi kuwasaidia kuwapa umaarufu, upuuzi wa namna hii hauwezi kuwafikisha popote. Jifunzeni kuwa na *leadership,* jifunzeni kuongoza na siyo kufanya harakati na kutukana na kufanya vurugu na Watanzania watawaelewa, lakini mkiendelea namna hiyo, ninawahakikishia chama chenu kitakufa kabla hatujafika mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ngenzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Masele.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba uniruhusu niendelee kuishukuru Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, kwa kuendelea kufanya kazi ya kuunganisha nchi kwa ujenzi wa barabara, madaraja, kuunganisha nchi mikoa na vijiji. Nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipomshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuupenda Mkoa wa Kigoma. Namshukuru sana na naomba niendelee kusema ahsante kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Barabara zinaendelea kufunguka na tayari Daraja la Mto Malagarasi limeshakamilika kwa asilimia 85. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa barabara iliyobakia ya Kigoma - Nyakanazi nayo iweze kufikiriwa hatimaye iweze kujengwa kwa sababu barabara ile ndiyo mkombozi wa Wananchi wa Kigoma kwa wakati huu ambapo usafiri wa reli haujakamilika. Naomba barabara ile iangaliwe iweze kujengwa mapema iwezekanavyo. Tunafahamu kwamba, tayari mpango wa ujenzi wa barabara ile unaendelea, lakini tunaomba uwekwe mpango mkakati wa kuhakikisha barabara ile inakamilika kwa sababu barabara ile ndiyo inayosambaza pembejeo katika Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayoongozwa na CCM kwa kushirikiana na Wananchi, imeweza kujenga vituo vya afya, imeweza kujenga zanahati na sasa inaendelea na kazi hiyo, lakini kuna haja sasa ya kuboresha huduma kwa kuhakikisha kuwa waganga na wauguzi pamoja na vifaa tiba vinapatikana. Nafahamu Serikali yetu ni sikivu na ina mpango wa makusudi wa kuhakikisha vitu hivyo vinapatikana kwa sababu imejiwekea mipango mizuri ndiyo maana imeanza kujenga vituo na imejenga zahanati. Nafahamu kabisa kwamba, waganga na wauguzi wanaendelea kusomeshwa, kwa hiyo, naomba watakaomaliza shule waletwe katika Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Kasulu ina madaktari japokuwa siyo wengi lakini wapo, lakini hawana wasaidizi kwa maana ya waganga na wauguzi. Niiombe Serikali itusaidie kuwaleta waganga na wauguzi katika

Hospitali hiyo. Hospitali hiyo vilevile haina gari la kubebea wagonjwa *(ambulance),* naomba Serikali itusaidie kutuletea gari la kubebea wagonjwa. Vipo vituo vya afya, kwa mfano, Kituo cha Nyakintonto, Kituo cha Lusesa, navyo pia havina magari ya kubebea wagonjwa. Wapo Madaktari ambao hawana kazi wamebaki kama wahudumu kwa sababu hawana vyumba vya kufanyia upasuaji. Naiomba Serikali itusaidie kupeleka pesa ili tuweze kujenga vyumba kwa ajili ya upasuaji kusudi Wananchi waendelee kupata huduma hiyo katika vijiji hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya msingi na sekondari; elimu ya msingi, walimu wapo lakini hawatoshi. Mara nyingi tunapofanya ziara vijijini, kilio cha Wananchi ni walimu katika shule za msingi na hasa katika shule za sekondari hakuna walimu, shule za msingi vyoo ni tatizo; naomba Serikali iliangalie hili. Vilevile ninawaombea walimu wapate stahiki zao ili wasivunjike moyo. Nami ni mwalimu, ninawapenda walimu wenzangu na nisipowasemea nitakuwa sijipendi mimi mwenyewe, naomba waangaliwe ili waweze kufanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo yanayojitokeza kwa watoto kutokufanya vizuri, naomba niwaambie Watanzania wenzangu na watoto wetu wa siku hizi siyo wazuri, muda mwingi wanatumia kucheza na *internet,* muda mwingi wanatumiana *message,* ukienda muda wa jioni siku hizi watoto hawana tabia ya kujisomea. Sasa mtoto kama hataki kujisomea; hii nayo ni Serikali inayofanya mtoto afeli? Pamoja na matatizo hayo, watoto nao wajenge tabia ya kujisomea ili waweze kufanya vizuri wanapokuwa wanafanya mitihani yao.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la umeme katika Wilaya ya Kasulu, jenereta ziliIetwa, umeme kidogo ulipatikana lakini baadhi ya watu hawajaweza kupatiwa umeme kwa sababu ya baadhi ya watendaji ambao hawatekelezi maagizo wanayopewa na Viongozi wao. Wizara inaagiza lakini watendaji wa kule wilayani hawatekelezi maagizo waliyopewa na Viongozi wao.

Ninaomba nyaya zipelekwe sambamba na nguzo ili Wananchi ambao hawajapatiwa umeme waweze kusambaziwa umeme.

Mheshimiwa Spika, pembejeo bado ni tatizo hazitoshi. Ruzuku ya pembejeo vilevile nayo ni tatizo. Pembejeo zinapelekwa kule lakini Wananchi bado wana malalamiko, naiomba Serikali iliangalie hili. Naomba Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, naomba niwaombe Watanzania wenzangu kudumisha amani, upendo utulivu na mshikamano. Tunapoenda kuwahamasisha kuanzisha vikundi kama hakuna upendo na mshikamano na tukianza kubaguana kwa maana ya dini hii na dini hii, hata vile vikundi tunavyoenda kuvianzisha hatutaweza kufaulu kwa sababu wataanza kubaguana wale watu tunaowafuata kule. Nawaomba Watanzania wenzangu na hasa akina mama, tuuenzi utamaduni wetu wa kudumisha amani, upendo na mshikamano, kwa sababu tukichezea amani sisi akina mama ndiyo tutakaoathirika. Sisi ndiyo tutakaokimbia na watoto, sisi ndiyo tutakaohangaika na watoto, wakati mwingine akina baba vita ikimkuta yuko mbali anachukua begi lake anakimbia anakuacha mama na watoto watano unahangaika. Nawaomba wanawake wenzangu tusisikie mambo ya kuambiwa, akili za kuambiwa changanya na za kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, tusione haya kusema mazuri yaliyofanywa na chama chetu. Tutembee kifua mbele kuisemea Serikali yetu, hakuna mtu mwingine atakayekwenda kusema kama siyo sisi tunaosema. Watu tuliozaliwa miaka ya 1960 kama mimi na wazazi wetu, wanafahamu tumetoka wapi na tunakwenda wapi. Watoto waliozaliwa siku hizi ndiyo hao wanaodanganywa, hawaelewi barabara zamani zilikuwaje. Leo ukitoka Kasulu kwenda Kigoma Mjini, zamani ulikuwa unatoka saa kumi na mbili unafika saa nane mchana, leo ukitoka Kigoma saa mbili, saa nne unaingia Kasulu na

unakwenda na kurudi. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Batenga.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo ndiyo inaweka msingi mahususi wa mijadala yote ambayo itaendelea kuwepo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja ya kwamba Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ipite. Nchi hii imetoka mbali, nchi hii inapitia katika vipindi mbalimbali, tumepata uhuru, tukawa na mfumo wa chama kimoja, hivi sasa tupo kwenye Mfumo wa Vyama Vingi, ni Watanzania hawahawa tunaelekea sehemu ya kukomaza demokrasia. Demokrasia siyo fujo. *(Makofi)*

Ndugu zangu Watanzania, niseme jambo moja tu; nchi hii inafanana na ziwa la maji au bahari, ndani yake kuna viumbe mbalimbali. Ziwani kuna viboko, kuna mamba, wote wanategemea maji yaleyale. Mamba atatoka atasema bwana wee kiboko toka, kiboko atatoka, baadaye jua likiwaka anarudi majini tena. Maji yakiendelea kuvurugika wote wataathirika. Kwa maana hiyo, nataka niseme hivi; Vyama vya Siasa tujifunze kufanya siasa za kistaarabu, kwa sababu tunakwenda kuzungumza na Watanzania wenye uelewa tofauti tofauti. Kwa maana hiyo, tunapokuwa kwenye demokrasia changa kama hivi, tunatakiwa sasa sisi ambao tunaelewa namna ya kufanya siasa tuwaelekeze wafuasi wetu njia mwafaka ya kufikia yale malengo ambayo tunakusudia. Vinginevyo, tutajikuta tunaivunja nchi hii na kufanana na nchi kama ya Somalia, ambayo ilikuwa na amani baadaye ikaipoteza na imewachukua zaidi ya miaka

20 kurejea katika hali ya utulivu, lakini napo mpaka wanasaidiwa na watu wengine; tusifike huko.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuamua kutenga maeneo mapya ya utawala, mikoa na wilaya zake. Kwa maana hiyo, niombe sasa, kwa sababu tumeanzisha maeneo mapya ya utawala ni sawasawa na mtoto anapozaliwa; mtoto anapozaliwa anahitaji msaada wa wale waliomtangulia na wazazi wake. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali sasa iwe na jicho la huruma kwenye maeneo haya mapya ya utawala. Mikoa mipya ipewe upendeleo ili iweze kusimama nayo iweze kuchukua hatua za maendeleo kwa haraka kama Mikoa mingine iliyotangulia.

Mheshimiwa Spika, tunapopitisha bajeti ni kitu kimoja na utekelezaji ni kitu kingine. Kumekuwa na matatizo ya mtiririko wa utoaji wa pesa kutoka Hazina kuja kwenye Halmashauri zetu. Kutokana na hali hiyo, kama utaratibu huu utaendelea wa kuchelewesha pesa kuja kwenye maeneo ya Halmshauri zetu ambako ndiko kwenye watendaji wengi na Wananchi wengi, tutakwaza shughuli za maendeleo katika maeneo yetu. Kwa maana hiyo, ninaishauri Serikali kwamba, tutakapokuwa tumemaliza mjadala wetu twende moja kwa moja kuhakikisha kwamba, yale ambayo tunakubaliana tuyatekeleze kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda katika kipindi cha mpito, tumejikuta katika wakati mmoja mgumu wa kutokuwa na umeme wa uhakika; lakini naishukuru Serikali kwa sababu imeendelea kuchukua hatua za kuuendeleza Mradi wa kuchukua gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam ili tuweze kuzalisha umeme wa bei nafuu na tuwe na umeme unaokidhi haja. Niombe tu hali iliyojitokeza Mtwara tuidhibiti ili kuleta umoja wa nchi hii, maana tukianza kugawana maeneo nchi hii haitakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila mmoja akitaka ziwa Victoria; watu wa Mwanza, Geita, Bukoba liwe la kwao na maliasili zote zilizoko huko na watu wa Dar es Salaam nao wakabaki peke yao, nchi hii tutakuwa katika mazingira magumu sana. Kwa maana hiyo, niombe kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama ambavyo imekuwa sikivu, inasimamia Miradi yake ya Maendeleo vizuri, imejenga barabara za kutosha na sasa inaenda kuendelea na mpango wake wa kuwa na chanzo cha kueleweka cha umeme, ninaamini ya kwamba tutafika salama.

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa na nguvu za umeme wa uhakika, uwekezaji hautakuwepo, wawekezaji hawataweza kuja kuwekeza viwanda vikubwa ambavyo vinaweza kuzalisha bidhaa ambazo zitauzwa kwa bei nafuu hapa nchini na kutoa ajira kwa vijana wetu ambao mpaka sasa wanapokosa ajira wanajiunga katika makundi ya kuandamana na kuipinga Serikali.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la ongezeko la watu; Tanzania inaonekana kuwa watu wanaendelea kuwa wengi, ardhi inakuwa ni shida na kuongezeka kwetu kama kutaendelea kama kulivyo, ina maana kuwa mbele ya safari tuna hatari ya kudumaza uchumi wetu kwani tutajikuta tunazozana na kuanza mapigano, kwa mfano, wanyama wanahitaji chakula, Wananchi pia wanahitaji chakula.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake, kama kutakuwa na tatizo la malisho kwa maana ya kuwa Wananchi wameongezeka na wanahitaji chakula, inakuwa ni kwamba sisi sote tutakuwa tukigombea ardhi moja ambayo ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Batenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia maneno machache katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Ukurasa wa 12 wa Kitabu cha Maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, imeeleza namna Wananchi watakavyoadhibiwa kwa kunyimwa fedha za maendeleo. Mimi nimeshangaa sana na kuumia sana kuamua kutotoa fedha za maendeleo kwenye Halmashauri ambazo zitapata Hati Chafu; ninajiulliza hivi Wananchi ndiyo wanaandika vitabu vya mahesabu? Hao wataalamu waliofundishwa na wakapewa kazi hiyo ya kutunza hesabu kwa nini wao wasiadhibiwe badala yake mnawaadhibu Wananchi?

Mheshimiwa Spika, hii haikubaliki na wala haieleweki na hii imeendelea kwa muda mrefu na Bunge limekemea kwa muda mrefu. Ningeshauri tufike mahali tuone kuwa unapozuia fedha za maendeleo ina maana Wananchi ndiyo walioadhibiwa, lakini Watendaji wao wanakaa wanatingisha miguu. Pia unakuwa unawadhalilisha sana Madiwani na mimi nikiwemo, tunapokaa katika vikao vya Halmashauri katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Halmashauri, kwa sababu wewe na Wananchi wako mnakuwa mmeadhibiwa kwa kukosa zile fedha za maendeleo kutokana na Hati Chafu.

Pamoja na hayo, Hati Chafu na Hati Safi, ningependa zote zioneshe thamani ya fedha zilizotumika katika Miradi mbalimbali, kwa sababu inaweza kuwa Hati Safi lakini kiutekelezaji, Miradi iliyotekelezwa wala hailingani na fedha iliyotumika. Naiomba sana Serikali ilione hili, kutopeleka fedha za maendeleo au kupunguza, unawaadhibu Wananchi. Sasa tunapenda ile adhabu badala ya kupewa Wananchi wapewe Watendaji waliovurunda kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni posho kwa ajili wa Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa. Hawa watu ni Viongozi ambao wanaongoza Serikali ngazi za msingi, ngazi za chini walipo Wananchi, wana majukumu mazito sana, wanasimamia Ulinzi na Usalama katika maeneo yao, wanasuluhisha ugomvi na migogoro midogomidogo inayojitokeza, kama siyo wao pengine kwenye mahakama na polisi kungekuwa hakupitiki, watu wangekuwa wanapeleka migogoro mingi kule. Wanasimamia shughuli za maendeleo, lakini pia wana

majukumu ya kutambua wakazi wa eneo lao na kuwatambulisha katika sehemu mbalimbali ambapo mwananchi anahitaji utambulisho kama Benki, Polisi na Mahakamani. Kwa hiyo, kwa majukumu hayo, Kiongozi huyu hapati muda mzuri wa kufanya shughuli zake binafsi za kumletea maendeleo au mahitaji yake na familia yake. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ifikirie kuweka kiwango cha posho ili iweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, napenda Serikali iangalie namna nzuri ya kugawa rasilimali za Taifa na kwa kutumia takwimu. Sasa, mimi huwa sielewi kama Mikoa iliyo pembezoni huwa inajulikana kuwa nayo ingepaswa kupewa rasilimali zaidi kwa ajili ya kuzingatia umbali huo. Kwa sababu ya usafiri na usafirishaji, bidhaa nyingi katika Mikoa ile ya mbali hasa Mkoa wa Kagera na Wilaya zake, gharama ni kubwa sana, lakini zinapotolewa fedha za Miradi wanahesabu kwamba bei ya bati Dar es Salaam na Ngara vinalingana au katika Wilaya zingine za Mikoa ya Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Hata Wakuu wa Mikoa wetu wako hapa, gharama za usafiri za Mkuu wa Mkoa kutoka Kagera kuja hapa siyo sawa na kutoka Morogoro kuja hapa. Kwa hiyo, hayo yote yawe yanazingatiwa wakati wa kugawa fedha za maendeleo na hata fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mambo mafupi hayo, nina uhakika kuwa yameeleweka na ninaomba yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ashsante. Mheshimiwa Mwanjale, atafuatiwa na Mheshimiwa Mansoor Hiran.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa nafasi hii, lakini ninataka nianze moja kwa moja na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ukurasa wa 31 ameelezea kwa kina kuhusu mwenendo wa bei za mazao makuu hasa ya biashara, korosho na pareto.

Kwa upande wangu ninaomba kuzungumzia kidogo kuhusu mambo ya pareto. Zao la pareto ni zao ambalo linalimwa katika maeneo mengi ya Jimbo langu la Mbeya Vijijini hasa Tarafa ya Isangati, Tarafa ya Itembela, Makete, Njombe na Ileje na huko Arusha. Tatizo la zao hili ni bei na ununuzi limesumbua sana. Mwaka jana alichaguliwa mnunuzi mmoja kwamba anunue zao la pareto, lakini kwa bahati mbaya bei yake ikawa ni ndogo sana kwa Wananchi.

Kwa hiyo, Wananchi waligoma na baadaye wakaingizwa wanunuzi wengine wa zao hili. Leo hii nilikuwa ninapigiwa simu kuwa bado kuna mnunuzi mmoja ameruhusiwa kununua pareto, inayolimwa katika maeneo niliyoyataja, lakini bei kateremsha tena na ameweka mabango kila sehemu, akielezea bei ya pareto itakuwa shilingi 1,800 badala ya shilingi elfu mbili na kitu ambayo ilikuwepo wakati ule. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iwaruhusu wanunuzi wengine binafsi ambao hawana viwanda na hawawezi kununua viwanda kwa sababu ni watu ambao wanataka kujipatia biashara. Tukisema mnunuzi mmoja wa kiwanda anunue pareto, bei yake inakuwa ya chini sana kiasi ambacho hata Wananchi wamethubutu kusema kama huyu ndiye atakuwa peke yake ananunua pareto, basi pareto haina haja ya kulimwa tena.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba, wako tayari kung'oa pareto kuliko mtu mmoja anunue. Ninaomba Serikali iruhusu wanunuzi wawe wengi maana ni soko huria. Kwa nini mtu mmoja aruhusiwe kununua pareto na hawezi kulipa bei nzuri? Ninaomba sana hili lisikilizwe hawa watu waruhusiwe na waanze kununua pareto hiyo ambayo inalimwa na Wananchi hao. Ninafikiri Jimbo langu ni la kwanza kulima pareto kwa wingi katika nchi hii na ni zao pekee la biashara katika maeneo ambayo nimeyataja, kuna sehemu zingine wanalima kahawa lakini kwenye maeneo hayo pareto ndiyo zao la biashara na viazi.

Nilikuwa ninaomba hawa wanunuzi binafsi waruhusiwe kununua pareto hiyo ili kuwavuta Wananchi

waweze kulima pareto kwa wingi, kama kweli tuna dhamira nzuri ya kutaka kuboresha au kulikuza zao la pareto.

La pili, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 40 ameeleza anasema, Serikali imeandaa mpango mkakati wa kuifanya Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Tanga, kuwa ndiyo Mikoa yenye Utalii wa Fukwe. Ninaomba niseme neno hili kuwa, Mbeya ndiyo kiwanja cha ndege kimeisha na kimekwisha maana ndege zimeanza kutua na tuna maeneo mengi ambayo tungeweza kuyaboresha au kuya-*promote* kuwa maeneo ya utalii; kwa mfano, ukienda Kitulo, ukatengeneza barabara nzuri kutoka Isinje kwenda Kitulo, bila shaka utapata watalii wengi watakaokwenda pale. Ukichukulia eneo la kutoka Kyela Mjini ukapeleka mpaka Matema, ni eneo ambalo watu wengi wanapenda kutembelea kule lakini barabara zake ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watalii hao ambao tunategemea kwamba wakija Mbeya watatua na ndege waende huko wakapumzike, hakuna barabara. Serikali inasema nini juu ya suala hili, maana Dar es Salaam utalii umeanza miaka mingi, watu wanaenda huko lakini maeneo haya ambayo unaweza kusema kuwa kwa Kusini nako huku sasa kungekuwa na maeneo ya utalii na yapo maeneo ambayo yameainishwa. Ninaiomba Serikali ijaribu kutafakari na kuifanya Mbeya na Kusini yawe ni maeneo ya utalii. Kwa sababu fukwe zipo, maeneo yapo, kuna Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, ni maeneo ambayo ni *very potential* kwa shughuli za utalii, ninaomba miundombinu yake iboreshwe ili tuweze kupata watalii na hasa wasafiri watakaotua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mbeya. Kwa hiyo, tuboreshewe Barabara ya Matema na Barabara ya kwenda Makete.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 64 mpaka wa 66, Mheshimiwa Waziri Mkuu pia ameelezea kwa kina kuhusu mambo ya Ukimwi kwamba kwa sasa maambukizi ya Ukimwi yamepungua. Juzi tumetembelea katika Kituo cha Chalinze na tukaona kituo kile kimejengwa lakini tulipofika pale tukaelezwa kuwa, vituo hivyo viko sehemu nyingi; Mwanza

kipo, Mbeya kipo, Tunduma kipo na Makambako kipo. Ukiangalia hivyo vituo, sisi Wabunge tulioko hapa inawezekana hatufahamu; kwa nini hivi vituo haviboreshwi vikajengwa vizuri zaidi ili hawa wenye magari makubwa wanaosababisha wakati mwingine hata kuleta maambukizi kwa wingi, waweze kwenda pale na kujipatia huduma za aina mbalimbali kama tulivyoelezwa wakati ule. Kwa hiyo, ninaomba vituo hivi vitangazwe na viboreshwe, vijengwe kisasa zaidi ili watu waende na kupata huduma katika vituo hivi na kwa kufanya hivyo maana yake hata maambukizi yatapungua.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa maambukizi yamepungua, lakini bado tunahitaji bidii zaidi ili maambukizi yaweze kupungua zaidi.

Lingine, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilikuwa ni Mpango wa MMEM (III), ambao unakusudia kuboresha elimu nchini, hii ikiwa na maana ya kuongeza idadi ya walimu nchini, kuongeza idadi ya vitabu vya kiada na ziada, vifaa vya kujifunzia na kadhalika. Mimi nilikuwa ninafikiria kwa msingi huo basi hata madarasa na shule tukienda huko vijijini ukaangalia ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nilitaka kumalizia hilo lakini basi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mansoor, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngoye na Mheshimiwa Jafo ajiandae.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru na mimi kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, ninaunga mkono mia kwa mia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Ninaomba nitoe pole kwa Wananchi wangu wa Jimbo langu la Kwimba, kwa mafuriko makubwa yaliyotokea jana katika Tarafa ya Mwamashimba, Kata ya Kikubiji na Kata ya Shirembo, zimeathirika vibaya sana hususan Vijiji vya Mwamitinje, Mwabhayanda, Shilembo na Manganga. Wananchi zaidi ya 500 wamehifadhiwa kwenye zahanati na shule za msingi na nyumba zaidi ya 300 zimebomoka na mashamba yameharibika.

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na Mbunge mwenzangu wa Wilaya ya Kwimba, Mheshimiwa Ndassa, kwa kushirikiana na Mheshimiwa *DC* na Wananchi wa Ngudu Mjini, leo tumetoa mchango na kupeleka msaada wa dharura kwa Wananchi hawa ambao wameathirika. Pia barabara ya kutoka Mabuki kwenda Jojiro na kufika Ngudu Mjini imeharibika, daraja limebomoka na kusombwa na maji, Wananchi wa Ngudu Mjini wanazungukia Magu kwenda Mwanza Mjini, hiyo njia ni ndefu sana kwao. Pamoja na kupeleka misaada ambayo tumepeleka leo, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kutumia Mfuko wake wa Maafa, atuletee msaada haraka iwezekanavyo, kwani Wananchi wameathirika. Katika Kata ya Kikubiji na Kata ya Shirembo, maji yamejaa, Wananchi wako kwenye zahanati, hakuna madawa, chakula hawana, tunaomba wapelekewe mablanketi na mahema ili wasipate matatizo zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hilda Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Kandege.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, ninaomba niunge mkono Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pili, katika kuzungumzia Hotuba hii, naomba nigusie maeneo mawili, matatu, ambayo nafikiri labda yananikera sana ninapokuwa nikifanya kazi. Kwanza ni suala la kilimo. Mimi napenda niwapongeze sana wakulima

wa nchi hii, kwa jitihada kubwa wanayofanya katika kushughulikia mazao mbalimbali na wanatufanya tuwe hai kwa sababu wanatulisha kwa juhudi zao. Hii inaendana na juhudi za Serikali katika kuhimiza KILIMO KWANZA, juhudi hiyo naona ni kubwa lakini ina matatizo yake makubwa kama yalivyozungumziwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, suala la bei ya mazao ni gumu na Wananchi wetu wanapata matatizo makubwa. Suala la bei ya mazao limekuwa likizungumziwa kila mara na mazao ninayozungumzia ni mazao yote ya biashara na ya chakula.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nikimwangalia mkulima wa ndizi wa Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya na mkulima wa viazi huko huko Wilayani Rungwe Mkoani Mbeya, mkulima wa mahindi wa Mbozi, Ileje pamoja na Mbeya Vijijini, wakulima hawa wamekuwa wakilima miaka nenda rudi lakini hawabadiliki kabisa kiuchumi, hawabadiliki kabisa kimaslahi, kwa sababu bei ya mazao ni ndogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na suala la kuunda chombo hiki ambacho Serikali itajaribu ku-*regulate* masuala ya bei wakati bei inapokuwa inashuka, lakini najua pamoja na kwamba wata-*regulate* bei, haitatosheleza kabisa mchango wa mkulima anaotumia anapoandaa shamba mpaka anapotoa mavuno yake. Hamna namna yoyote hapa nchini tutakayomsaidia mkulima aweze kupata bei nzuri, ni kuanzisha viwanda vitakavyoongeza thamani ya mazao. Ukiongeza thamani ya mazao katika maeneo ambayo watu wanalima mazao mbalimbali tutakuwa tumemfanyia mkulima jitihada kubwa sana ili aweze kutajirika.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia viwanda vidogovidogo, nazungumzia vile vile viwanda vya kati; kuna viwanda ambavyo sasa hivi vinafanya kazi lakini ni vya kubabaisha babaisha tu; hakuna mtu anayefuatilia kutoka Serikalini kuona kama viwanda hivyo kweli vinafanya kazi kwa *standard* inayotakiwa, ndiyo maana tunapata mazao ambayo hayana thamani kubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nipongeze juhudi za *SIDO;* wanajitahidi kuelimisha wajasiriamali ili waweze kuzalisha vizuri, waweze kuweka viwanda. Hii haitoshi, nasisitiza Serikali ihimize kwa nguvu zake zote uanzishwaji wa viwanda katika maeneo ya wakulima kulingana na mazao wanayolima.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kwamba, nilipokuwa napitia Kitabu hiki cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sikuona mahali popote ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu au TAMISEMI, wameliwekea mkazo mkubwa suala la uharibifu wa mazingira hapa nchini, halipo. Pia sikuona jinsi ambavyo Ofisi ya Makamu wa Rais wanajipanga katika kuangalia uharibifu wa mazingira na kuiwekea mipango yake. Hilo limekuwa *skipped* sijaliona na nimewasiliana na Mawaziri wanaohusika nao wananishangaa. Kwa hiyo, nataka tu nisisitize hapa, mpaka sasa nchi yetu ipo hatarini kuwa jangwa, kwa sababu uelewa wa Wananchi katika suala zima la mazingira ni mdogo sana. Vile vile ukienda kuangalia wale ambao wanatakiwa kusimamia masuala haya ya mazingira ambayo ni Serikali za Mitaa, jamani hawajachukua hatua kubwa ambazo zinaonesha kuna juhudi yoyote ya kusimamia suala la mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana, nchi hii tunazungumzia masuala ya mabadiliko ya tabianchi kila siku na athari zake kwa kilimo, lakini kila wakati tumekazana kuzungumzia suala la kilimo cha umwagiliaji, suala la kilimo cha mvua, lakini hatuangalii huko tuendako; je, haya mambo ya kilimo yatakuwa endelevu kama masuala ya mazingira hatujayatilia mkazo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana tena sana, Serikali iingie kwa nguvu katika kulisimamia suala la mazingira na hotuba za Viongozi mbalimbali zijikite huko ili Wananchi nao washtuke waone kweli kuna umuhimu wa kusimamia masuala ya mazingira hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kuwa, hatujakuletea lakini hapa baadhi ya Wabunge tumeanzisha

Umoja wa Marafiki wa Mazingira, ambao tunataka tuendelee kupiga kelele kuhusu suala la mazingira hapa nchini, kwa sababu ya hali ilivyo na inavyokwenda ni mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu utawala wa mikoa. Nimefanya kazi katika nafasi hii ya utawala wa mikoa kwa miaka kama ishirini hivi katika uongozi kama Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa. Mimi nashangaa kidogo, kwa wale wanaosema watu hawa hawana kazi, ninashangaa sana kwa sababu hakuna kitu kinachokwenda huko mikoani kama hakuna msukumo wa Mkuu wa Mkoa wala msukumo wa Mkuu wa Wilaya! Mambo yanasimama vilevile ni mpaka Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya aingilie kati. Kama ni ulinzi wa amani ni Mkuu wa Mkoa, tunakaa kwa amani hapa na utulivu ni kwa sababu Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanadhibiti masuala ya ulinzi na usalama wa nchi hii, lakini na masuala ya maendeleo vilevile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *law and order has to be there.* Lazima iendelee kuwepo na hawa watu, lazima waendelee kuwepo. Ila jambo ambalo ningetazamia watu waseme ni kuwatetea watu hawa jinsi wanavyofanya kazi katika mazingira magumu; hawana fedha, hakuna bajeti ya kutosha, lakini majukumu anayopewa kwamba nenda pale, nenda kulia, kushoto, katikati na hakuna fedha! Sasa mtu mmoja sijui ni nani; ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Haaa! (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Jafo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenipa fursa jioni hii ya leo kuongea, lakini nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi jioni hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niwasihi sana ndugu zangu Watanzania, suala zima la amani halina mbadala, tuzungumze mambo yote kama Viongozi wa nchi, lakini suala zima la amani halina mbadala. Mara nyingi hata vitabu vya dini vimesema kwamba, kuna sifa maalum ya mtu anayeitwa mnafiki, mnafiki hata ukimwamini yeye anafanya hiyana na anapozungumza ni lazima atasema uwongo na akiweka ahadi basi hatimizi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipitisha mchakato mzima katika ajenda ya kwanza katika Sheria ya Mchakato wa Katiba, kuna watu walitoka humu ndani, bahati mbaya wakaenda kwa Mheshimiwa Rais kwa mlango wa nyuma, Mheshimiwa Rais akawakubalia, chai ikaanza. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri unayehusiana na mambo ya uhusiano, ikiwezekana hata staftahi nyingine wekeni pilipili siku hizi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea maslahi ya nchi, suala zima la Katiba siyo suala la Chama fulani, ni mustakabali wa Taifa la Tanzania. Leo hii tumekubaliana kwa pamoja, mchakato unakwenda wewe unasema hapana; nini nia yako? Nia yako maana yake una ajenda nyingine nyuma ya mlango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ndugu zangu Watanzania wote, katika Vyama vyetu tulikemee hili, ni lazima tushikamane kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, kama kifungua kinywa cha hotuba yangu hapa au mchango wangu, naomba kujikita sasa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kubwa zaidi, juzi tumeona jinsi gani Watanzania wanalalamikia kupanda kwa nauli, lakini kupanda kwa nauli maana yake nyuma kuna hoja nyingine inayofuata, *purchasing power* ya Watanzania ipo chini sana.

**MBUNGE FULANI:** Kiswahili!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, uwezo wa kwenda dukani kununua mahitaji, hii ni changamoto kubwa sana. Tatizo kubwa ni nini? Nashukuru sana Serikali imejitahidi kupandisha mishahara katika vipindi mbalimbali, lakini ndugu zangu naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba unisikilize, bahati nzuri bajeti ya Waziri wa Fedha itakuja mwishoni, naomba tuangalie suala zima la makato ya kodi kwa wafanyakazi wote. Makato ya kodi ni makubwa hata mshahara ukipanda, kodi inayokatwa ni kubzwa zaidi.

Kwa mtu wa kima cha chini anakatwa asilimia 14 na wale wa juu anayepata mshahara mkubwa zaidi anakatwa shilingi laki moja na ishirini *plus* asilimia 20 ya ongezeko la shilingi laki saba na ishirini, kiasi kwamba, hata mtu akipata shilingi milioni tano, kadiri unavyokatwa maana yake mwisho wa siku anarudi nyumbani akiwa hana kitu.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali iangalie kwa kina jinsi gani itafanya, kuboresha maisha ya wafanyakazi wote na hii tuangalie jinsi gani ya kuboresha suala zima katika *pay as you earn.* Katika Taifa letu tunajua jinsi gani wafanyakazi katika *pay as you earn;* kwa mfano, katika takwimu za mwaka 2010/11, ni sehemu peke yake ambayo imeongoza kuliko hata *corporate tax*. Michango ilikuwa karibu bilioni 934, asilimia 17 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie ni jinsi gani itaangalia kwa kina kulipa kodi vizuri katika sehemu mbalimbali zisizokusanya kodi na ninyi mnajua ni mashahidi, kulikuwa na sakata kubwa sana la jinsi gani vilabu vya mipira hapa nchini vilikuwa havilipi kodi mpaka klabu yetu na kaka yangu Ismail Aden Rage na Yanga, vilikuwa havilipi kodi. Ina maana kwamba, ukusanyaji wa kodi bado ni tatizo katika nchi yetu. Naiomba Serikali iangalie ni jinsi gani tutakusanya kodi ilimradi kuhakikisha tuna-*compensate* katika suala zima la kupunguza kodi kwa wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama nchi inaamini sasa hivi tuna vijana wetu wengi wapo mitaani hawana kazi, walioajiriwa ni wachache sana. Kuporomoka kwa suala zima la viwanda nchini kunasababisha janga kubwa la vijana wetu waliomaliza Vyuo Vikuu na wa kada mbalimbali wakakosa kazi. Naomba sana Serikali yetu ijielekeze zaidi katika suala zima la ufufuaji wa viwanda na kuhakikisha tunaboresha suala zima la ujenzi wa viwanda vipya, bila hivyo suala la ajira tutakuwa tunazungumza kila siku.

Mheshimiwa Spika, tulitembelea pale Mtwara, karibu viwanda vyote vya Korosho vimekufa, bila kurekebisha hilo tutakuja kupata matatizo makubwa. Kwa mfano, mimi kwangu Kisarawe kuna Kiwanda cha *STAMICO* kilibinafsishwa toka mwaka 2006, yule mwekezaji mpaka leo anahangaika katika Ofisi ya Waziri wa Ardhi kuweza kupata hati na jinsi gani aweze kuungana na wadau mbalimbali kuboresha kile kiwanda na vijana wangu wa Kisarawe wapate ajira. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulisimamie hili kwa karibu zaidi kwa ajili ya kuboresha maisha ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni suala zima la ajira. Toka mwaka jana tumepiga kelele sana, utaratibu wa Sekretarieti ya Ajira kuajiri mpaka Mtendaji wa Kijiji, jambo hili sisi haturidhiki nalo. Ukienda sehemu mbalimbali vijijini hakuna hata watendaji wa vijiji, hakuna watendaji wa kata, sababu kubwa ajira zote zifanywe na Sekretarieti ya Tume ya Ajira. Jambo hili haliwezekani. Kwa nini Halmashauri zisiajiri tuna vijana wengi katika Halmashauri zetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii inawezekana Mkuu wa Mkoa mpya ameajiriwa na dereva mpya ameajiriwa, wanaulizana wakipangiwa safari hata sehemu ya kwenda hawajui, dereva mpya hajui maeneo yenyewe. Tungepeleka ajira katika Halmashauri zetu, inawezekana ajira hizi zingetoka katika baadhi ya Halmashauri ambazo vijana wametoka maeneo yale. Naiomba Serikali iharakishe mchakato huu maana kila siku tutafanya kesho, kesho kutwa, tunawakera

Wananchi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili Waziri Mkuu lipo kwako halipo kwa mtu mwingine yeyote. Ninaamini katika kuhitimisha hotuba yako hii, nakuomba ikiwezekana tusikie Watanzania kwamba mchakato huu sasa unarudi katika Halmashauri zetu ilimradi vijana wetu wapate ajira katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, pale kwangu Hospitali yetu ya Wilaya ina matatizo makubwa sana, lakini ofisi yako imetuma wadau mbalimbali hasa katika ofisi yako, Naibu Katibu Mkuu amefika pale. Ninakumbuka kwa sababu mwaka jana niliuliza swali la msingi mwezi wa sita na bahati nzuri mmetuahidi kutufanyia ukarabati katika Hospitali yetu ya Wilaya pamoja na kuitengeneza *mortuary*. Nakushukuru sana, lakini naamini bajeti hii itasaidia kuleta mchakato mzuri ili Wilaya ya Kisarawe tuwe katika mazingira mazuri na kama mnavyojua, Kisarawe ina-*accommodate* baadhi ya wagonjwa wengi kutoka Dar es Salaam. Kiujumla, nikizungumzia hata Mkoa wetu wa Pwani pale Hospitali yetu ya Tumbi ni sehemu kubwa ambayo inapokea wagonjwa wengi hasa majeruhi. Hospitali hii tumeipandisha sasa hivi, watu wote pale Kibaha kwa ndugu yangu Mheshimiwa Koka, wanapata huduma katika Kituo cha Afya cha Mkoani, hakiwezi ku-*accommodate* akina mama ambao wanafika pale, akina mama wanadhalilika.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ofisi yako yenye jukumu hili iangalie jinsi gani itaboresha Kituo cha Afya cha Mkoani pale Kibaha, ambapo mimi ni Mjumbe katika Kamati yetu ya Mkoa, tunahudhuria Vikao vya RCC, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uangalie jinsi gani utatusaidia Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia sasa hivi Tanzania, juzi juzi niliienda kutembelea Mkoa wa Kigoma, watu wasiokuwa na shukrani ni lazima wazungumze; miundombinu ya barabara hivi sasa imeboreka. Tanzania yetu hii siyo ya siku za nyuma, sasa hivi hata watu wengine

*wanaohalabwanya* humu ndani, kwao kuna barabara ya lami wanakanyaga! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aingalie Kisarawe, ile barabara yetu ya kilomita 54 mwaka huu bahati nzuri imefanyiwa upembuzi yakinifu, tunaomba sasa tabaka la lami liweze kuja hapa. Siku Mheshimiwa Magufuli atakapokuja hapa, nataka nione ni jinsi gani Kisarawe inaguswa katika suala zima la ujenzi wa barabara ya lami.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba, Kisarawe kutatengenezwa *dry port,* kituo cha kuwekea mizigo inapotoka bandarini, ni vyema nakushukuru sana na ninaishukuru Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme kwamba, huyu ndiye msemaji wetu wa mwisho na utaratibu wetu bado umekwenda vizuri sana, jioni hii tulikuwa tumejipangia watu 17 lakini wamefika 22, nadhani tunaenda vizuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache; kwanza, nakumbushia ile semina ambayo itatupa sisi uelewa wa wenzetu wenye ugonjwa wa ngozi na mahitaji yao ya msingi na tabu waliyonayo. Semina hiyo itaanza saa tatu pale Ukumbi wa Msekwa, ni kwa Wabunge wote. Najua mnataka kupumzika lakini mjitahidi kuwahi, inapendeza watu mkianza wengi na mgeni wetu rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu; tunamshukuru kwa kukubali hilo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili sasa sijui hata nisemeje, zile fomu za kuomba namna unavyotaka kuchangia kuanzia sasa mpaka mwisho, kuna wenzetu kadhaa hapa wameandika lakini wakasahau kuandika

majina sasa tunafanyaje. Mimi hata sijui nisemeje maana hata kusema nimwite nani sijui! (*Kicheko*)

Kuna Waheshimiwa Wabunge watano, sasa naomba yule anayejifikiria kwamba labda alisahau apite pale ofisini kwetu akacheki kujua hali yake ni hiyo hiyo maana ni vigumu kabisa kujua. Mwingine amepiga *tick* kama kura za uchaguzi; tulisema muweke *priority* ya kwanza, ya pili, ya tatu, sasa wewe umepiga tu kama unapiga kura. Kwa hiyo, tuna watu watano na wengine kama mna mashaka na fomu mlijaza vipi tafadhali piteni pale ofisini watawasaidia.

Waheshimiwa Wabunge, jambo linguine ambalo ningependa kusema ni kwamba, jana kulikuwa na mwongozo ulioombwa na Waziri wa Nchi kuhusu maneno aliyozungumza Mheshimiwa Lugola, tukasema tusubiri Hansard. Baada ya kutafuta na kuangalia Sheria ama Kanuni yetu, Kanuni ya 63(2) inasema: "Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni, hatachukuliwa kuwa anasema uwongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa au lililoandikwa na Vyombo vya Habari."

Waheshimiwa Wabunge, *Hansard* ya Mheshimiwa Lugola jana inasema katikati kwamba, nilisoma kwenye gazeti moja, Kamishna wa Tume ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya, Ndugu Christopher Kyondo anasema, wanawafahamu kwa majina wanaohusika na madawa ya kulevya, lakini wameshindwa kuwakamata kwa sababu ya mbinu walizonazo. Hiyo ndiyo aliyosoma kwenye magazeti. Sasa yeye anaendelea anasema maana yake ni nini? Maana yake ni, kama siyo rushwa zinazosababishwa na Watendaji wa Serikali au hata wakiwemo baadhi ya Mawaziri ndiyo wanahusika na madawa ya kulevya.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasema kwamba, alisoma kwenye gazeti, naomba hili liishe hakuna sababu ya kuthibitisha kwa mujibu wa Kanuni zetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nawaomba mwende kwenye semina kesho na akina mama

kuna mkutano mkubwa sana wa akina mama kule juu *UDOM,* ni wa akina mama wa vyama vyote, kuna Mkutano unaendelea kule mkiweza kufika pia itakuwa vizuri, ni tarehe 13 na tarehe 14.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nawashukuru sana kwa *weekend* hii, ilikuwa *weekend* ya majaribu, tulikuwa tupo kwenye mchakato hata wa kuangalia tunakwendaje, lakini nawashukuru mmeshiriki toka kila hatua na hili ni jambo jema. Nasi tutakuwa tunaendelea kushauriana mara kwa mara ili tujaribu kurudisha hali ya kuwa pamoja wakati wote kuliko kuparaganyika. Taarifa tulizonazo kutoka kwa Wananchi ni kwamba, wamefurahi sana mnavyochangia, maana mnachangia habari zao. Kwa hiyo, nawashukuru sana, niwatakie *weekend* njema na yenye manufaa na mshiriki inavyopaswa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1. 40 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 15 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*